

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Tano – Tarehe 4 Februari, 2017**

**D U A**

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alisoma Dua

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

**NDG. CHARLES MLOKA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE – K.n.y. MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari, 2016 hadi Januari, 2017. Naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Katibu.

**NDG. CHARLES J. MLOKA - KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa Kipindi cha  
Januari, 2016 hadi Januari, 2017**

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti una muda usiozidi nusu saa kuwasilisha taarifa yako. Karibu!

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI:**

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kwa ajili ya muda naomba taarifa yote ipokelewe na kuingizwa kwenye Hansard na kuwa Kumbukumbu Rasmi za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kamati kuanzia mwezi Januari, 2016 hadi Januari, 2017 kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 pamoja na kuzingatia sheria na taratibu mbalimbali zilizowekwa kupitia Sheria za Fedha, Sera za Kodi na Sera za Fedha. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilikutana na Serikali na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali zikiwemo taasisi zisizo za kiserikali na sekta binafsi ambapo ushauri na maoni yao yalisaidia Kamati kuelewa vizuri changamoto wanazokabiliana nazo hasa katika masuala ya kodi na utekelezaji wa bajeti hivyo kuweza kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia iliweza kujadiliana na Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu mipango ya maendeleo na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Kimsingi, vikao hivyo vya majadiliano na mashauriano vililenga kuisaidia Serikali kuboresha usimamizi na utekelezaji wa Bajeti na mipango yake pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, zifuatazo ni kazi zilizotekelawa na Kamati ya Bajeti katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Disemba, 2016 na baadhi ya Taarifa za Kamati zilizowasilishwa Bungeni katika vipindi tofauti vya Bunge:-

(a) Kufuutilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2015/2016 kwa kipindi cha nusu mwaka na robo tatu mwaka;

(b) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2015/2016 na Kupitia na Kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2016/2017;

(c) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano 2011/2012 hadi 2015/2016 na Mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano 2016/2017 hadi 2020/2021;

(d) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2016/2017 yatokanayo na vyanzo vyatatu na vyanzo vya nje;

(e) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2015/2016; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

(f) Kuchambua na kushauri Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2016, *The Finance Act 2016* na Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa Mwaka 2016, *The Public Procurement Ammendment Act 2016*;

(g) Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria za kodi;

(h) Kamati ilipitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na hatimaye kutoa maoni na ushauri wake;

(i) Kamati ilipitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/2018 na hatimaye kutoa maoni na ushauri wake; na

(j) Kamati iliendelea kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vyatatu na mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilichambua na kutathimini utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/2016; kwa muhtasari utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2015/2016 unaonesha kuwa Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi bilioni 22,495.5 kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 13,475.6 ni mapato ya kodi na yasiyo ya kodi asilimia 14.3 ya Pato la Taifa. Shilingi bilioni 521.9 ni mapato ya halmashauri sawa na asilimia 0.6 ya Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, washirika wa maendeleo waliahidi kuendelea kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 2,322.5 mwaka 2015/2016. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 660.3 ilikuwa ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, shilingi bilioni 1,115.4 mikopo nafuu na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo, shilingi bilioni 347.8 ni fedha kwa ajili ya miradi iliyoko chini ya MCA na Mifuko ya Pamoja ya Kisekta ni shilingi bilioni 119.

Hadi kufikia Juni, 2016 kiasi cha shilingi bilioni 1,727.0 kilikuwa kimepokelewa sawa na asilimia 74 ya ahadi zote zilizotolewa. Mwenendo wa utoaji fedha za washirika wa maendeleo unaonyesha ni pungufu kwa asilimia 26 ya fedha yote iliyotarajiwa kutolewa. Kamati haikupata majibu ya kuridhisha kuhusu sababu za washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilipanga kukopa kutoka katika vyanzo vya ndani na nje shilingi bilioni 6,175.5. Kati ya fedha hizo, kiasi cha shilingi bilioni 2,142.5 kilipangwa kukopwa kutoka nje na kiasi cha shilingi bilioni 4,033 kilipangwa kukopwa kwenye soko la ndani. Hadi kufikia mwezi Juni 2016, Serikali ilikuwa imekopa mikopo ya ndani jumla ya shilingi bilioni 5,304.9. Hii ni sawa na asilimia 132 ya kiasi kilichopangwa kukopwa kwa mwaka 2015/2016. Kiasi hiki kimeongezeka kwa asilimia 32 zaidi ya kile kilichotarajiwa kukopwa na Serikali kutoka kwenye vyanzo vya ndani. Mwenendo huu unaonesha kuwa Serikali inakopa zaidi ya kile kilichoidhinishwa na Bunge bila kufuata Sheria ya Bajeti, na pia hatua hii ya kukopa zaidi ndani inaathiri ukuaji wa sekta binafsi hasa katika uhakika wa kupata mikopo katika Mabenki ya kibiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mwenendo wa matumizi ya Serikali, hadi kufikia mwezi Juni 2016, Serikali ilitoa mgao wa matumizi wenye thamani ya shilingi bilioni 21,108.9 sawa na asilimia 93.8 ya bajeti ya mwaka kwenda kwenye mafungu mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti. Kiasi hiki kilijumuisha shilingi bilioni 1,541.8 ambayo yalikuwa malipo yaliyokwama ya mwaka wa fedha 2014/2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa matumizi unaonesha kuwa katika Bajeti iliyopita ya mwaka 2015/2016, shilingi bilioni 16,017 zilikuwa ni matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara ya watumishi wa Serikali na taasisi; yaani shilingi bilioni 6,562.9 sawa na asilimia 101.5 ya bajeti ya mwaka; shilingi bilioni 6,480.9 kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Taifa sawa na asilimia 101 ya bajeti ya mwaka; shilingi bilioni 170.3 ni kwa ajili ya matumizi ya Halmashauri yaliyotokana na makusanyo yao na shilingi bilioni 2,803 za matumizi mengine kwa Wizara, Taasisi, Idara na Tawala za Serikali za Mitaa, sawa na asilimia 80 ya bajeti ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 4,552.3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 76.9 ya bajeti yote ya mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini kuwa moja ya sababu ambazo zilisababisha Serikali kushindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo kwa kiwango kilichokusudiwa ni kwa sababu Serikali ililipa malipo yaliyokwama mwaka wa fedha 2014/2015.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mapitio ya mwenendo wa mkuaji wa uchumi kwa mwaka 2015/2016. Pamoja na mafanikio yaliyoelezwa na Serikali kuhusu ukuaji wa uchumi na mwenendo mzuri wa mfumuko wa bei, Kamati inaona ukuaji wa uchumi huu bado haujaweza kumfikia mwananchi wa kawaida. Pato la mwananchi wa kawaida bado ni dogo sana na asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaishi kwa kipato cha chini ya dola moja ya Kimarekani kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiuhalisia kwa kuangalia gharama za maisha katika maeneo yetu, mfumuko wa bei za bidhaa ni zaidi ya huu unaoneshwa kwenye takwimu zinazotolewa na Serikali na hasa kwa bidhaa kama Sukari, Mchele pamoja na Mafuta ya kula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa upande wa deni la Taifa, hadi kufikia mwezi Juni 2016 ilikuwa ni Dola za Kimarekani bilioni 23.2 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni 19.96 Juni, 2015, hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 18. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali tathmini inaonyesha kuwa deni hili ni himilivu (*Debt Sustainability Assessment*) kwa kuzingatia viashiria vilivyowekwa. Hata hivyo Kamati imebaini kwamba ukuaji wa kasi ya Deni la Taifa kwa kiwango cha asilimia 18 kwa mwaka mmoja tu unaweza kusababisha deni hili kutokuwa himilivu na hivyo kuilazimu Serikali kutumia kiasi kikubwa cha mapato yake inayokusanya kwa ajili kulipia deni hilo kila mwezi, suala ambalo linaweza kusababisha Serikali kushindwa kugharamia bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango na Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 ilianisha tozo na kodi mbalimbali zilizokuwa na lengo la kuongeza au kupunguza viwango vya kodi kwenye maeneo mbalimbali pamoja na kupunguza misamaha ya kodi kwenye maeneo mengine, na hivyo kuongeza makisio ya mapato kutoka shilingi triliioni 22.49 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi shilingi triliioni 29.53 kwa mwaka wa fedha 2016/17. Ongezeko hilo la shilingi triliioni saba ni sawa na ongezeko la asilimia 31 ya bajeti kwa mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Kamati iliyowasilishwa hapa Bungeni tarehe 10 Juni, 2016 kuhusu Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/2017 ilionesa kuwa shilingi triliioni 17.7 sawa na asilimia 60 ya Bajeti yote zitatumika katika Matumizi ya Kawaida na shilingi triliioni 11.8 sawa na asilimia 40 ya Bajeti yote zitatumika kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hatua hii ilifikiwa baada ya Serikali kuongeza makadirio ya mapato ya ndani kwa asilimia 32, makadirio ya mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa kuongezeka kwa asilimia 28, makadirio ya misaada na mikopo kutoka nje kuongezeka kwa asilimia 55, makadirio ya mikopo ya ndani kuongezeka kwa asilimia 33, makadirio ya matumizi ya kawaida kuongezeka kwa asilimia saba na makadirio ya matumizi ya maendeleo kuongezeka kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja za Kamati za Bunge za Kisekta zenye maslahi ya Kitaifa, Kamati ilipokea hoja mbalimbali zenye maslahi ya kitaifa ambazo zilibainishwa na Kamati za Bunge za Kisekta zilipokuwa zikichambua utekelezaji wa Bajeti za Wizara wanazosimamia kwa mwaka wa fedha 2015/2016 na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilipokea hoja 35 zenye maslahi ya Kitaifa kutoka kwa Kamati za Bunge za Kisekta. Kati ya hoja hizo, hoja 27 zilihusu maombi ya fedha za nyongeza kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali kwa mwaka 2016/2017 na hoja nane zilihusu masuala mengine; mfano; maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/2016 na fedha za matumizi ya kawaida ambazo zilikuwa hazijatolewa. Hata hivyo, wakati wa majadiliano ya Wizara husika kwa mara ya kwanza Mawaziri wa Wizara husika waliihakikishia Kamati kuwa fedha walizokuwa wametengewa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 zitatosha kutekeleza majukumu ya Wizara zao na hivyo kupelekea hoja kupungua na kubaki hoja tano tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya mashauriano kuhusu hoja hizo tano zilizopitishwa na Kamati ya Uongozi na kisha kujadiliwa na Bunge yameainishwa katika jedwali hapa chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo haya ya kina, naomba nikiri kwamba mchakato wa maandalizi ya bajeti wa mwaka 2016/2017 ulikuwa na changamoto nyingi hasa katika maeneo la majadiliano na Serikali kuhusu kuongeza fedha kwa ajili ya matumizi ya baadhi ya mafungu ambayo Kamati iliona kuna umuhimu wa kuongezewa fedha, lakini kwa kupitia miongozo mbalimbali kutoka kwako pamoja na busara za Kamati, tulifanikiwa kutekeleza jukumu hili. Aidha, changamoto hizi zinachukuliwa kama chachu itakayoisaidia Kamati katika kutekeleza jukumu hili wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Serikali katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakumbukwa kwamba tarehe 8 Juni, 2016, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kupata mapato ya kugharamia Bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza suala hili, Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 na kushauriana na Serikali katika maeneo mbalimbali ya Muswada yaliyohitaji ufanuzi. Aidha, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kupata maoni yao kupitia kikao cha wadau (*Public Hearing*). Kupitia vikao hivi, Kamati iliweza kuona mantiki ya Serikali kuhusu mapendekezo iliyoyaleta yaliyokuwa na lengo la kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali.

Kamati ilikamilisha jukumu hili kwa kuwasilisha Bungeni maoni na mapendekezo yake kuhusu Muswada wa Fedha wa mwaka 2016, na baada ya majadiliano Bunge lako Tukufu liliidhinisha hatua mbalimbali za kodi; ada na tozo mbalimbali zilizoanza kukusanywa na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muhtasari Sheria zifuatazo zilifanyiwa marekebisho katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2016:-

- (i) Sheria ya Makampuni, Sura 212;
- (ii) Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura 306;

- (iii) Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332;
- (iv) Sheria ya Utawala wa Mahakama, Sura 237;
- (v) Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290;
- (vi) Jedwali la Kwanza la Sheria ya Magari (Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki);
- (vii) Sheria ya Utawala wa Bunge, Sura 115;
- (viii) Sheria ya Reli, Sura 170;
- (ix) Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura 399;
- (x) Sheria ya Utawala wa Kodi, Sura 438;
- (xi) Sheria ya Kodi ya Majengo Sura 289;
- (xii) Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148; na
- (xiii) Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu stadi, Sura 82.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 28 Juni, 2016 Kamati iliwasilisha Bungeni maoni na mapendekezo kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma. Bunge lilipitisha muswada huo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ununuzi wa Umma kwa kuondoa mapungufu yaliyopo katika Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2011 kwa kupunguza gharama na muda wa michakato ya manunuzi Serikalini.

Aidha, muswada huo mpya ulitegemewa kutoa mapendekezo kwa kampuni za ndani, vikundi maalum, malighafi na bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na kuweka viwango mahsus kwa bidhaa zitakazotumiwa na Serikali. Muswada huo ulisaini kuwa Sheria tarehe 7 Julai, 2016 na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla Sheria ya Ununuzi wa Umma kuitia muswada huo imefanyiwa marekebisho mambo yafuatayo:-

- (a) Kuweka sharti la kutenga kazi kwa ajili ya wakandarasi wa ndani kwa kuwahusisha wazabuni wa ndani katika manunuzi na kuwajumuisha au kuwashirikisha kwenye kazi hizo pamoja na wazabuni wa nje;
- (b) Kuweka kifungu cha dharura ili kuwezesha vitu vya kuokoa uhai na vinginevyo kununuliwa kwa dharura pindi inapobidi;
- (c) Kutoa fursa kwa Taasisi na Makampuni ya Umma yanayofanya biashara kuwa na utaratibu wake wa kufanya maamuzi ili yaweze kuijendesha kibiashara;

(d) Kuweka masharti ya kufanya manunuzi kwa kuzingatia thamani ya fedha kwa bidhaa mbalimbali zitakazotumika Serikalini ikiwepo ununuzi wa magari;

(e) Kuondoa sharti la kuwepo kwa mikataba baina ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na wazabuni iliyofungamanishwa na bei. Hatua hii itaondoa upangaji wa bei elekezi kwa watoa zabuni, kupunguza urasimu na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika manunuzi Serikalini;

(f) Kupunguza muda wa mchakato wa manunuzi pamoja na muda wa mzabuni kuwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli kutoka siku 28 hadi siku saba; na

(g) Kurekebisha kanuni ili kupunguza muda wa mchakato wa zabuni za ununuzi wa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma kutoka wastani wa siku 91 zilizobainishwa katika Kanuni hadi siku 49 kwa zabuni za kitaifa, na kutoka wastani wa siku 100 hadi siku 56 kwa zabuni za kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji ya Bajeti ya Serikali katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa Fedha 2016/2017; Mapato ya Serikali. Katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/2017 mapato ya kodi yalifikia shilingi bilioni 3,462.5, sawa na asilimia 99 ya lengo la kukusanya bilioni 3,509.1. Takwimu zinaonesha kodi zilizovuka lengo ni pamoja na ushuru wa forodha kwa asilimia 105, ushuru wa bidhaa nje asilimia 105 na kodi ya Ongezeko la Thamani ndani asilimia 117. Hata hivyo kodi ya ushuru wa bidhaa ndani asilimia 91, kodi ya Ongezeko la Thamani nje asilimia 88 na Kodi ya Mapato asilimia 95 hazikuweza kufikia malengo ya robo mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 362.5, sawa na asilimia 54 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 672.0. Aidha, mapato ya Halmashauri yalikuwa shilingi bilioni 117 sawa na asilimia 70 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 166.4. Mwenendo wa takwimu hizi unaonesha kuwa bado Serikali ina kazi zaidi ya kuhakikisha kwamba inafikia malengo iliojiwekea katika maeneo haya ili kuweza kugharamia bajeti yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/2017 Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 1,115 sawa na asilimia 83 ya lengo la shilingi bilioni 1,344.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu misaada na mikopo ya masharti nafuu na masharti ya kibiashara kutoka nje, kwa mwaka wa fedha 2016/2017

washirika wa maendeleo walihidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni 3,600.8. Kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 483 ni misaada na mikopo ya kibajeti, shilingi bilioni 372 ni mifuko ya pamoja ya kisekta na Shilingi bilioni 2,745 ni miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo takwimu zinaonyesha hadi kufikia mwezi Septemba 2016 kiasi kilichopokelewa ni shilingi bilioni 285, sawa na asilimia 16 tu ya lengo la robo mwaka. Kwa mchanganuo wa mikopo na misaada ya kibajeti shilingi bilioni 36 (sawa na asilimia 80), Mifuko ya Pamoja ya Kisekta bilioni 57 (sawa na asilimia 36) na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 192 (sawa na asilimia 12) ya lengo la robo mwaka. Aidha, kwa upande wa mikopo yenye masharti ya kibashara bado Serikali inaendelea kufanya majadiliano na taasisi za fedha za kimataifa pamoja na mabenki kuweza kupata mikopo hiyo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa kwenye bajeti ya mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015/2016 imeanza kutumika na kuonesha mwanga katika usimamizi wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali na kwa kuwa utaratibu mzuri unaohusu uwasilishwaji wa taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa bajeti umeainishwa kwenye Sheria hiyo na Kanuni zake, ambapo Wizara Taasisi na Mashirika zinapaswa kufuata, kwa hiyo basi Kamati inaishauri Serikali pamoja na Taasisi zake kuhakikisha kwamba inatekeleza kikamilifu masharti na kanuni za Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, ikiwa ni pamoja na Serikali kuhakikisha inawasilisha kwa wakati Bungeni taarifa zote zilizoainishwa kwenye sheria hiyo hususan taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa kila robo mwaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa utaratibu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali hupitishwa na Bunge lako kupitia Sheria ya Fedha inayotungwa kila mwaka wa fedha, na kwa kuwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 Sheria ya Fedha iliyotungwa iliruhusu Serikali kuanza ukusanyaji wa mapato mbali mbali ambayo yanaenga kuwezesha upatikanaji wa matumizi ya Serikali, kwa hiyo basi Kamati inasilitiza Serikali kuhakikisha inatekeleza Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kama ilivyoinishwa na Bunge hasa katika maeneo yafuatayo:-

(a) Sharti la kisheria kwa kampuni za mawasiliano kujisajili katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) na kuhakikisha Watanzania wanamiliki asilimia isiyopungua 25 ya mtaji wa kampuni zinazomiliki leseni za kujenga miundombinu ya mawasiliano (*network facilities*) na kutoa huduma za mawasiliano (*network services/application services*); na vilevile kuhakikisha watanzania wanamiliki asilimia isiyopungua 51 ya mtaji wa kampuni zinazomiliki leseni ya huduma ya utangazaji (*content services licensee*);

(b) Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) kuhakikisha inakamilisha haraka iwezekanavyo mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ili kuweza kuongeza ukusanyaji wa mapato husika, mathalani kodi ya majengo na kodi ya pango;

(c) Ukopaji wa mikopo ndani usizidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge na uzingatie hali uchumi na ukwasi wa mabenki katika vipindi husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usimamizi wa Deni la Taifa; kwa kuwa deni la Taifa ni malipo ya awali ni lazima Serikali ilipe kupitia mapato yake ya kila mwezi; na kwa kuwa pamoja na Serikali kubainisha kuwa deni hilo ni himilivu, bado inaonesha Serikali inatumia fedha nyngi za makusanyo ya ya kila mwezi. Kwa hiyo basi, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha ukopaji, ulipaji wa deni hilo hauathiri ugharamiaji wa bajeti ya Serikali, pia Serikali ihakikishe inakamilisha zoezi la tathmini ya uwezo wa nchi, kukopa na kulipa yaani (*Sovereign Credit Rating*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mipango ya maendeleo; kwa kuwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa umeainisha vipaumbele mbalimbali ambavyo Serikali inalenga kutekeleza katika kipindi cha miaka mitano na kwa kuwa mionganini mwa vipaumbele hivyo ni kukuza uchumi wa viwanda, uendelezaji wa miundombinu, maji, elimu na afya, kwa hiyo basi Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba inapeleka kwa wakati fedha za kugharamia miradi ya maendeleo; kufuatilia na kusimamia tathmini ya utekelezaji wa mipango husika; inatumia ipasavyo fursa za kiuchumi za ustawi; inawekeza ipasavyo katika nishati ya umeme; inashirikisha kikamilifu sekta binafsi na kuendelea kuandaa na kuboresha rasilimali watu wenye ujuzi na elimu ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu urasimishaji wa sekta isiyo rasmi; kwa kuwa sekta isiyo rasmi ni mionganini mwa maeneo ambayo kwa muda mrefu yamesababisha Serikali kutokuwa na takwimu sahihi za walipa kodi na kwa kuwa ukosekanaji wa takwimu hizo unasababishia Serikali kupoteza mapato mengi na hivyo kufanya Serikali kutokusanya mapato yake ipasavyo; kwa hiyo basi, Kamati inaendelea kuisisitizia Serikali kuhakikisha inaongeza juhudii zake katika zoezi la urasimishaji wa biashara na shughuli ndogo ndogo za kiuchumi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mapato na kudhibiti upotetu wa mapato. Sambamba na hili, Serikali ikamilishe haraka mfumo wa kuwatambua walipa kodi kwa kutumia *TIN* na vitambulisho vya kitaifa (*national IDs*), kuboresha utataratibu wa kuwasilisha *return* kwa sekta isiyo rasmi pamoja na kuimarisha

utawala na usimamizi wa kodi kwa kuwatambua walipa kodi kwenye vitalu (*Block Management System*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ukuaji wa sekta ya kilimo; kwa kuwa sekta ya kilimo inachangia ajira kwa takriban asilimia 70 ya Watanzania na kwa kuwa mwaka 2015 ukuaji wa sekta hiyo ni asilimia tatu tu; na kwa kuwa sekta hiyo kwa kiasi inategemewa kusaidia kufanikisha juhudzi za kupunguza umaskini hasa vijiji na kuchochea mapinduzi ya viwanda; kwa hiyo basi; Kamati inaishauri Serikali kuanza kutekeleza mikakati madhubuti ya kuinua sekta hii kwa kuboresha kilimo cha umwagiliaji; kuboresha teknolojia ya kilimo; kuweka masoko ya uhakika ya mazao ndani na nje ya nchi; kuwezesha uanzishaji wa viwanda vingi vya usindikaji wa mazao ya kilimo (*agro-processing industry*) na kusambaza maafisa ugani wa kutosha katika maeneo yote nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja za Kamati za Bunge za Kisekta zenyenye maslahi ya Kitaifa; kwa kuwa Bunge, kupitia Kanuni ya 98 na 101 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 limeweka utaratibu utakaoiwezesha Serikali kufanya majadiliano kuhusu hoja mahsusizi zinazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za Kisekta, wakati wa kuchambua bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha uliopo na unaofuata na kwa kuwa kupitia mashauriano hayo masuala mbalimbali ya kibajeti huweza kupatiwa ufumbuzi kabla ya kupitshwa kwa Bajeti ya Serikali inayotekelizwa katika mwaka wa fedha unaofuata; hivyo basi Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa ushirikiano wa kutosha kwa Bunge wakati wa kujadili, kushughulikia na kutekeleza hoja za Kamati za Bunge za Kisekta zenyenye maslahi ya kitaifa ili kuleta tija ya zoezi zima la kutathmini utekelezaji wa bajeti za Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha uliopita na kuchambua makadirio ya bajeti za Wizara na taasisi husika kwa mwaka wa fedha unaofuata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge ya kuongeza vyanzo vipyta vya mapato; kwa kuwa Wabunge kupitia Kamati yako maarufu Mheshimiwa Mwenyekiti Chenge iliyoundwa kwa ajili ya kupendekeza vyanzo vya mapato ilipendekeza vyanzo mbalimbali vya mapato kwa Serikali na kwa kuwa ripoti hiyo imewasilishwa Serikalini kwa ajili ya hatua za utekelezaji ambayo inaonekana baadhi ya vyanzo havijafanyiwa kazi, kwa hiyo basi, Kamati inaendelea kuisisitizia Serikali kukamilisha masuala yafuatayo:-

(a) Kukamilisha utafiti na tathmini ya ukusanyaji wa mapato kupitia bahari kuu;

(b) Kukamilisha Kanuni za Sheria za kusimamia mapato ya mafuta na gesi asilia ya mwaka 2015 na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia Tanzania ya mwaka 2015;

(c) Kulipia deni la TANESCO ambalo hadi mwezi Agosti, 2016 lilitifika takribani shilingi bilioni 794.9;

(d) Kukamilisha miradi mbalimbali ya nishati ya umeme ikiwemo Kinyerezi Awamu ya Pili na miradi miradi mingine ya nishati mbadala inayoendeshwa kwa nguvu za maji (*hydro*), joto ardhi (*geothermal*), upepo na umeme wa juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kuni pa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isidor Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijiji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalam wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na taasisi mbalimbali za fedha ambao wamefanya kazi na Kamati hii katika kipindi hiki.

Aidha, kwa namna ya pekee kabisa napenda nishukuru wadau mbalimbali wa masuala ya biashara na kodi ambao wameshirikiana na Kamati hii katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Wajumbe waalikwa kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo mbalimbali kwa Serikali kuititia taarifa ambazo Kamati ya Bajeti iliwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru pia Katibu wa Bunge - Dkt. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda niishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuhudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

**MWENYEKITI:** Ahsante, naomba utoe hoja.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI KAMATI YA BAJETI:**  
Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI KUHUSU UTEKELEZAJI WA  
SHUGHULI ZAKE KATIKA KIPINDI CHA KUANZIA MWEZI JANUARI, 2016 HADI  
JANUARI, 2017 KAMA ILIVYOWEKWA MEZANI**

## **1.0 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kuwasilisha Taarifa ya utekelezaji wa kazi za Kamati kuanzia mwezi Januari, 2016 hadi Januari, 2017, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016.

## **2.0 UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KAMATI**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015, Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016 pamoja na kuzingatia sheria na taratibu mbalimbali zilizowekwa kuititia Sheria za Fedha, Sera za Kodi na Sera za Fedha. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Kamati ilikutana na Serikali na Taasisi zake pamoja na wadau mbalimbali zikiwemo Taasisi zisizo za kiserikali na Sekta Binafsi ambapo ushauri na maoni yao yalisaidia Kamati kuelewa vizuri changamoto wanazokabiliana nazo hasa katika masuala ya kodi na hivyo kuweza kuishauri Serikali ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia iliweza kujadiliana na Wizara na Taasisi za Serikali kuhusu Mipango ya Maendeleo na utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Kimsingi, vikao hivyo vya majadiliano na mashauriano vililenga kuisaidia Serikali kuboresha usimamizi na utekelezaji wa Bajeti na mipango yake pamoja na kuboresha ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, zifuatazo ni kazi zilizotekelawa na Kamati ya Bajeti katika kipindi cha kuanzia mwezi Januari hadi Desemba, 2016 na baadhi ya Taarifa za Kamati zilizowasilishwa Bungeni katika vipindi tofauti vya Bunge:-

- a) Kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya mwaka 2015/16 kwa kipindi cha nusu mwaka na robo tatu mwaka
- b) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa katika kipindi cha mwaka 2015/16 na Kupitia na Kujadili Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka 2016/17;
- c) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano (2011/12 – 2015/16) na Mapendekezo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2016/17-2020/21);
- d) Kutathmini na kuchambua Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2016/17 yatokanayo na vyanzo vya ndani na vyanzo vya nje.
- e) Kupitia na kujadili Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2015/16; pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2016/17;
- f) Kuchambua na kushauri Muswada wa Sheria ya Fedha wa mwaka 2016 (*The Finance Act 2016*) na Muswada wa Sheria ya Manunuzi ya Umma wa Mwaka 2016 (*The Public Procurement (Ammendment) Act 2016*);
- g) Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kujadili changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika utekelezaji wa sheria za kodi;
- h) Kamati ilipitia na kujadili kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/18 na hatimaye kutoa maoni na ushauri wake;
- i) Kamati ilipitia na kujadili kuhusu Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 na hatimaye kutoa maoni na ushauri wake;
- j) Kamati iliendelea kufanya utafiti na uchambuzi wa vyanzo mbalimbali vya mapato.

## 2.1 TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA 2015/16 NA MAPENDEKEZO YA MAPATO NA MATUMIZI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kutathimini utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2015/16 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2016/17.

### a) Tathmini ya Utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2015/16

**Mheshimiwa Spika**, Kwa muhtasari utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa kipindi cha mwaka 2015/16 unaonyesha kuwa Serikali ilipanga kukusanya na kutumia jumla ya shilingi **bilioni 22,495.5** kutoka kwenye vyanzo vya ndani na nje. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 13,475.6 ni mapato ya kodi na yasiyo ya kodi (asilimia 14.3 ya Pato la Taifa); shilingi bilioni 521.9 ni mapato ya halmashauri (sawa na asilimia 0.6 ya Pato la Taifa). Aidha, Washirika wa Maendeleo waliahidi kuendelea kutupatia misaada na mikopo ya jumla ya **shilingi bilioni 2,322.5** mwaka 2015/16. Kati ya fedha hizo, **shilingi bilioni 660.3** ilikuwa ni misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, **shilingi bilioni 1,115.4** mikopo nafuu na misaada kwa ajili ya miradi ya maendeleo, **shilingi bilioni 347.8** ni fedha kwa ajili ya miradi iliyoko chini ya MCA (T) na Mifuko ya Pamoja ya Kisekta ni **shilingi bilioni 119**. Hadi kufikia June 2016 kiasi cha shilingi **trilioni 1.727.0** kilikuwa kimepokelewa sawa na asilimia 74 ya ahadi zote zilizotolewa. Mwenendo wa utoaji fedha za washirika wa maendeleo unaonyesha ni pungufu kwa **asilimia 26** ya fedha yote iliyotarajiwa kutolewa. Kamati haikupata majibu ya kuridhisha kuhusu sababu za Washirika wa Maendeleo kutotimiza ahadi zao kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilipanga kukopa kutoka katika vyanzo vya ndani na nje shilingi **bilioni 6,175.5**. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **shilingi bilioni 2,142.5** kilipangwa kukopwa kutoka nje na kiasi cha **shilingi bilioni 4,033** kilipangwa kukopwa kwenye soko la ndani. Hadi kufikia mwezi Juni 2016, Serikali ilikuwa imekopa mikopo ya ndani jumla ya **shilingi bilioni 5,304.9**. Hii ni sawa na **asilimia 132** ya kiasi kilichopangwa kukopwa kwa mwaka 2015/16. Kiasi hiki kimeongezeka kwa **asilimia 32** zaidi ya kile kilichotarajiwa kukopwa na Serikali kutoka kwenye vyanzo vya ndani. Mwenendo huu unaonyesha kuwa Serikali inakopa zaidi ya kile kilichoidhinishwa na Bunge bila kufuata Sheria ya Bajeti, pia hatua hii ya kukopa zaidi ndani inaathiri ukuaji wa sekta binafsi hasa katika uhakika wa kupata mikopo katika Benki za kibiashara.

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu mwenendo wa matumizi ya Serikali, hadi kufikia mwezi Juni 2016, Serikali ilitoa mgao wa matumizi wenyewe thamani ya **shilingi bilioni 21,108.9** sawa na asilimia 93.8 ya bajeti ya mwaka kwenda kwenye mafungu mbalimbali kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti. Kiasi hiki kilijumuisha **shilingi bilioni 1,541.8** ambayo yalikuwa malipo yaliyokwama ya mwaka 2014/15. Mchanganuo wa matumizi unaonyesha kuwa katika Bajeti iliyopita ya Mwaka 2015/16; **shilingi bilioni 16,017** zilikuwa ni matumizi ya kawaida ikijumuisha mishahara ya watumishi wa Serikali na Taasisi (**shilingi bilioni 6,562.9**) sawa na **asilimia 101.5** ya bajeti ya mwaka; **shilingi bilioni 6,480.9** kwa ajili ya ulipaji wa Deni la Taifa sawa na **asilimia 101** ya bajeti ya mwaka; **shilingi bilioni 170.3** ni kwa matumizi ya Halmashauri yaliyotokana na makusanyo yao na **shilingi bilioni 2,803** za matumizi mengineyo kwa Wizara, Taasisi, Idara na Tawala za Serikali za Mitaa sawa na **asilimia 80** ya bajeti ya mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali ilitoa kiasi cha shilingi bilioni 4,552.3 kwa ajili ya miradi ya maendeleo (sawa na asilimia 76.9 ya bajeti yote ya mwaka). Kamati ilibaini kuwa moja ya sababu ambazo zilisababisha Serikali kushindwa kutekeleza miradi yake ya maendeleo kwa kiwango kilichokusudiwa ni kwa sababu Serikali ilili pa malipo yaliyokwama **mwaka wa fedha 2014/15** (Trilioni 1.5). Kamati inaona umefika wakati sasa, Serikali inapoandaa Bajeti ya mwaka unaofuata ijumu ishe madeni/malipo ya mwaka unaoisha ambayo yatalipwa mwaka wa fedha wa kibajeti unaofuata. Vile vile kwa kuzingatia taarifa ilizotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango mbele ya Kamati, hali inaonyesha kuwa kwa ujumla hali halisi ya utoaji wa fedha kwenye miradi ya maendeleo kwa kuzingatia ratiba ya utekelezaji wa miradi haikuwa ya kuridhisha. Aidha, kuongezeka kwa kasi ya matumizi ya kawaida ya Serikali kumekuwa ni changamoto kubwa katika utekelezaji wa bajeti kwa upande wa miradi ya maendeleo ukizingatia kuwa fedha za makusanyo hugawanywa kulingana na matumizi ya wakati husika hivyo hakuna uwiano sawa kati ya matumizi ya kawaida na matumizi ya maendeleo.

## b) Mapitio ya Mwenendo wa ukuaji wa Uchumi kwa Mwaka 2015/16

**Mheshimiwa Spika**, takwimu zinaonyesha kuwa uchumi umeendelea kuimarika na ukuaji wa Pato la Taifa ulifika kiwango cha asilimia 7.0 kwa mwaka 2015 kama ilivyokuwa mwaka 2014. Kiwango hiki cha ukuaji wa Uchumi kimechangiwa kwa kiasi kikubwa na ukuaji wa mikopo ya sekta binafsi; kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya ujenzi na miundombini; kuongezeka kwa shughuli za habari na mawasiliano. Ukuaji huu pia ulichangiwa na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta ya uzalishaji umeme kulikosababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za viwandani na huduma nyingine.

Shughuli za kiuchumi zilizokuwa kwa kasi ya juu katika mwaka 2015 ni pamoja na habari na mawasiliano (asilimia 15); utawala wa umma (asilimia 12.6); ujenzi (asilimia 10.5); shughuli za fedha na bima (asilimia 10.4); na uchukuzi (asilimia 9.5).

**Mheshimiwa Spika**, ukuaji wa sekta ya kilimo haukua wa kuridhisha. Takwimu zinaonyesha kwamba katika mwaka 2015 sekta hii imekua kwa asilimia 3.0 ikilinganishwa na asilimia 3.4 kwa mwaka 2014. Ukuaji usioridhisha wa Sekta hii inayoajiri zaidi ya asilimia 70 ya Watanzania unazorotesha juhudzi za Serikali za kupunguza umaskini hasa maeneo ya vijijini.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa mwenendo wa bei unaonyesha kwamba Wastani wa mfumuko wa bei katika mwaka 2015 umeendelea kuwa katika kiwango cha tarakimu moja. Wastani wa mfumuko wa bei kwa mwaka 2015 ulipungua na kufikia asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 6.1 mwaka 2014. Katika kipindi cha Januari hadi Juni 2016, wastani wa mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 4.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2015. Mwezi Julai 2016, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 5.1 ukilinganisha na asilimia 6.4 Julai 2015. Aidha, katika kipindi kama hicho, mfumuko wa bei wa chakula ulikuwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na asilimia 10.5; mfumuko ambao haujumuishi chakula na nishati umekuwa asilimia 2.6 ikilinganishwa na asilimia 2.1 Julai 2015.

**Mheshimiwa Spika**, Pamoja na mafanikio yanayoelezwa na Serikali kuhusu ukuaji wa uchumi na mwenendo mzuri wa mfumuko wa bei, Kamati inaona ukuaji wa uchumi huu bado haujaweza kumfikia mwananchi wa kawaida. Pato la mwananchi wa kawaida bado ni dogo sana na asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaishi kwa kipato cha chini ya dola moja ya kimarekani kwa siku. Kiuhalisia kwa kuangalia gharama za maisha katika maeneo yetu, Mfumuko wa bei za bidhaa ni zaidi ya huu unaonyeshwa kwenye takwimu zinazotolewa na Serikali hasa kwa bidhaa kama sukari, mchele na mafuta ya kula.

**Mheshimiwa Spika**, aidha kwa upande wa Deni la Taifa hadi kufikia mwezi Juni, 2016 liliwa Dola za Kimarekani bilioni 23.2 ikilinganishwa na Dola za Kimarekani bilioni 19.69 Juni, 2015 hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 18. Kwa mujibu wa maelezo ya Serikali tathmini inaonyesha kuwa deni hili ni himilivu (Debt Sustainability Assessment) kwa kuzingatia viashiria vilivyowekwa, hata hivyo Kamati imebaini kwamba ukuaji wa kasi wa deni la Taifa kwa kiwango cha asilimia 18 kwa mwaka mmoja tu unaweza kusababisha deni hili kutokwa himilivu na hivyo kuilazimu Serikali kutumia kiasi kikubwa cha mapato yake inayokusanya kwa kila mwezi kulipia deni hilo, suala ambalo linaweza kusababisha Serikali kushindwa kugharamia bajeti yake.

**c) Mapendekezo ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/17**

**Mheshimiwa Spika**, Serikali kupitia hotuba ya Waziri wa Fedha na Mipango na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 iliainisha tozo na kodi mbalimbali zilizokuwa na lengo la kuongeza au kupunguza viwango vya kodi kwenye maeneo mbalimbali pamoja na kupunguza misamaha ya kodi kwenye maeneo mengine; na hivyo kuongeza makisio ya mapato kutoka **Shilingi trilioni 22.49** kwa mwaka wa fedha 2015/16 hadi Shilingi **trilioni 29.53** kwa mwaka wa fedha 2016/17. Ongezeko hilo la **Shilingi trilioni 7** ni sawa na ongezeko la asilimia 31 ya bajeti ya mwaka 2015/2016.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Kamati iliyowasilishwa hapa Bungeni tarehe 10 Juni 2016 kuhusu Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2016/17 ilionyesha kuwa **Shilingi trilioni 17.7**; sawa na **asilimia 60 ya Bajeti yote** zitatumika katika **Matumizi ya Kawaida** na **Shilingi trilioni 11.8**; sawa na **asilimia 40** ya Bajeti yote zitatumika kwa ajili ya **Matumizi ya Maendeleo**. Hatua hii ilifikiwa baada ya Serikali kuongeza makadirio ya mapato ya ndani kwa asilimia 32; makadirio ya mapato ya mamlaka za Serikali za Mitaa kuongezeka kwa asilimia 28; makadirio ya Misaada na mikopo toka nje kuongezeka kwa asilimia 55; makadirio ya mikopo ya ndani kuongezeka kwa asilimia 33; makadirio ya matumizi ya kawaida kuongezeka kwa asilimia 7 na makadirio ya matumizi ya maendeleo kuongezeka kwa asilimia 100.

**Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la Thamani(VAT) ya mwaka 2014 imewezesha Makusanyo ya VAT kuongezeka kwa **asilimia 11** kutoka **Shilingi milioni 2,210.1** kwa kipindi cha Julai 2014 hadi Machi 2015 na kuwa **Shilingi milioni 2,444.4** kwa kipindi cha Julai 2015 hadi machi 2016. Kwa upande wa misamaha ya kodi, takwimu zinaonesha kuwa katika kipindi cha mwaka **2000/01 hadi 2014/15** misamaha ya kodi ilikuwa ni wastani wa **asilimia 2.3** ya Pato la Taifa; na katika kipindi cha kuanzia Julai 2015 hadi Machi 2016 misamaha ya kodi imeshuka na kuwa **asilimia 0.84** ya Pato la Taifa.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali katika kipindi cha mwaka 2015/16 ilivuka lengo la ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi kwa kukusanya shilingi bilioni 1,188.15 sawa na asilimia 107 ya makadirio ya ukusanyaji wa shilingi bilioni 1,112.68. Hata hivyo, Serikali haikufikia lengo ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri kwa kukusanya shilingi bilioni 425.9 sawa na asilimia 82 ya makadirio ya kukusanya shilingi bilioni 521.9.

## 2.2 HOJA ZA KAMATI ZA BUNGE ZA KISEKTA ZENYE MASLAHI YA KITAIFA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea hoja mbalimbali zenyе maslahi ya kitaifa ambazo zilibainishwa na Kamati za Bunge za Kisekta zilipokuwa zikichambua utekelezaji wa Bajeti za Wizara wanazosimamia kwa mwaka wa fedha 2015/16 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea hoja thelathini na tano (35) zenyе maslahi ya Kitaifa kutoka kwa Kamati za Bunge za Kisekta. Kati ya hoja hizo, hoja ishirini na saba (27) zilihusu maombi ya fedha za nyongeza kwenye Wizara na Taasisi mbalimbali kwa mwaka 2016/17 na hoja 8 zilihusu masuala mengine, mfano maombi ya fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka 2015/16 na fedha za matumizi ya kawaida ambazo zilikuwa hazijatolewa. Hata hivyo, baada ya majadiliano ya Wizara husika kwa mara ya kwanza Mawaziri wa Wizara husika waliihakikishia Kamati kuwa fedha walizotengewa zitatosha kutekeleza majukumu ya Wizara zao na hivyo kupelekea hoja kupungua na kubaki hoja tano (5) tu.

**Mheshimiwa Spika**, matokeo ya mashauriano kuhusu hoja hizo tano zilizopitishwa na Kamati ya Uongozi na kisha kujadiliwa na Bunge yameainishwa katika jedwali Na. 1 hapo chini;

**Jedwali Na. 1: Matokeo ya Mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Wizara ya fedha na Mipango kuhusu Bajeti ya Serikali ya mwaka 2016/17**

<b>Na</b>	<b>FUNGU</b>	<b>HOJA</b>	<b>MATOKEO YA MASHAURIANO</b>
1	FUNGU 31: OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA	Kutenga fedha kwa ajili ya Mfuko wa Hifadhi ya Mazingira	Kamati ilijiridhisha kuwa Kiasi cha shilingi bilioni 2.1 kilitengwa kwa ajili ya upandaji wa miti chini ya Mfuko wa Mazingira.
2	FUNGU 49: WIZARA YA MAJI NA UMWAGILIAJI	Kuongeza tozo ya shilingi 50 kwa kila lita ya mafuta petrol/diesel na kufika shilingi 100 ili fedha itakayopatikana ipelekwe kwenye Mfuko wa Taifa wa Maji kwa ajili ya kutekeleza mradi wa maji vijiji	Kamati ya Bajeti na Serikali hawakufikia makubaliano.
3	FUNGU 56: OFISI YA RAIS – TAMISEMI	Ujenzi wa Zahanati na Vituo vya Afya ndani ya miaka 5 (2016 – 2020).	Kamati ilipendekeza kuwa kiasi cha shilingi bilioni 30 zitolewe kwa ajili ya utekelezaji wa Ujenzi wa Zahanati na vituo vya Afya nchini. Hata hivyo, Serikali ilionomba ikafanyie kazi suala hili ili kujua gharama halisi za utekelezaji wa pendekezo hilo.
4	FUNGU 96: WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO	Serikali itoe kwa Shirika la Taifa la Utangazaji (TBC) kiasi cha shilingi bilioni 18 katika mwaka huu wa Fedha ili uboreshaji wa Mradi wa Upanuzi wa Usikiu uanze mara moja na TBC iweze kusikika katika wilaya 81 zilizobaki.	Kamati ya Bajeti na Serikali hawakufikia makubaliano.
5	FUNGU 22: HAZINA	Mradi wa Milioni 50 kwa kila Kijiji. Mradi huu unalenga "Kutenga Kiasi cha Milioni 50 kila Kijiji kwa ajili ya kukopesha Vikundi vya Wajasiriamali kupitia Ushirika wa Kuweka na Kukopa (SACCOS) katika vijiji husika".	Kamati imeshauriana na kukubaliana na majibu ya Serikali kuhusiana na hoja hii. Kamati iliridhia kiwango cha shilingi bilioni 59.5 (asilimia 47 ya mahitaji kwa mwaka wa Fedha 2016/17) kilichotengwa kwa ajili ya kutumika kama Mpango wa Majoribio (Pilot Program) kwa Wilaya zote. Kamati ilisisitiza takwimu za idadi za vijiji na mitaa ziangaliwe vizuri ili kiasi kitakachotolewa kwa kila mwaka iwe 20% ya mahitaji halisi kwa kipindi chote cha utekelezaji wa Mpango huu.

**Mheshimiwa Spika**, Pia, katika kutatua changamoto ya kuchelewa upelekaji wa fedha kwa baadhi ya mafungu katika bajeti ya mwaka wa fedha 2015/16 Kamati ilishauriana na Serikali na kufanikiwa kupeleka fedha kwenye mafungu hayo ili yameze kukamilisha majukumu yao ya mwaka husika.

**Jedwali Na. 2: Matokeo ya Mashauriano kati ya Kamati ya Bajeti na Wizara ya fedha na Mipango kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Serikali ya Mwaka 2015/16**

Ia	Miradi	Fedha zilizotolewa/ Ahadi ya Serikali
.	Fedha za Maendeleo Shirika la Utangazaji TBC	Serikali ilitoa fedha za maendeleo za TBC Shilingi milioni 800 kati ya Shilingi 1 bilioni zilizoidhinishwa mwaka 2015/16.
.	Fidia ya Mradi wa Kurasini	Serikali ilitoa bilioni 3.2 za kulipa fidia kwa ajili ya Mradi wa Kurasini Logistic Hub.
.	Mradi wa Umeme Vijijini (REA)	Serikali ilitoa Shilingi bilioni 80 kati ya shilingi bilioni 161 zilizosalia kupelekwa mradi wa REA.
.	Mfuko wa Maji	Serikali iliahidi kutoa fedha zilizobaki za mfuko wa maji Shilingi bilioni 86. 811.
.	Railway Development Levy (1.5%)	Serikali iliahidi kupeleka fedha zilizokusanywa kati ya Desemba 2015 mpaka Machi 2016, kwenye mfuko wa Reli.
.	Fedha za Mfuko wa Mahakama	Serikali imetoa shilingi Bilioni 2.5 kwa ajili ya uanzishwaji wa Mahakama ya Rushwa na Makosa ya Uhujumu Uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo haya ya kina, naomba nikiri kwamba mchakato wa maandalizi ya bajeti ya mwaka 2016/17 ulikuwa na changamoto nyingi hasa katika eneo la majadiliano na Serikali kuhusu kuongeza fedha kwa ajili ya matumizi ya baadhi ya mafungu ambayo Kamati iliona kuna umuhimu wa kuongezewa fedha, lakini kwa kuptitia miongozo mbalimbali kutoka kwako pamoja na busara za Kamati, tulifanikiwa kutekeleza jukumu hili. Aidha, changamoto hizi zimechukuliwa kama chachu itakayoisaidia Kamati katika kutekeleza jukumu hili wakati wa uchambuzi wa Bajeti ya Serikali katika mwaka wa fedha 2017/18.

### **2.3 MAPENDEKEZO YA MPANGO WA PILI WA MAENDELEO WA TAIFA WA MIAKA MITANO (2016/17-2020/21) NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2016/17.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua na kujadiliana na Serikali kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2016/17 iliyowasilishwa Bungeni na Wizara ya Fedha na Mipango. Baada ya majadiliano hayo Kamati iliwasilisha Bungeni Taarifa zake zenye maoni na mapendekezo tarehe 01 Februari, 2016 na tarehe 20 Aprili, 2016 kama inavyoelekezwa katika Kanuni ya 94 (5) (a) na hatimaye Bunge liliridhia mapendekezo husika.

**Mheshimiwa Spika**, Kabla ya kutoa mapendekezo kuhusu Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka mitano (2016/17 – 2020/21), Kamati ilifanya mapitio ya tathimini ya Utekelezaji wa Mpango wa Kwanza wa Maendeleo wa Taifa wa miaka mitano (2011/12 - 2015/16) ambapo kimsingi utekelezaji wa Mpango huo ulikuwa ni asilimia 60 tu ya malengo yaliyowekwa. Sababu zilizotolewa na Serikali za kutfikia malengo ya utekelezaji wa Mpango huu ni ukosefu wa fedha za kugharamia mipango husika; ufuatiliaji na usimamizi hafifu wa tathmini ya utekelezaji; kutotumia fursa za kiuchumi kwa ustawi wa nchi; upatikanaji hafifu wa nishati ya umeme; kudumaa kwa ukuaji wa sekta binafsi pamoja na upatikanaji mdogo wa rasilimali watu wenye ujuzi na elimu ya kutosha.

Kamati ilijulishwa kwamba utekelezaji wa Mpango wa maendeleo wa miaka mitano unategemea kwa kiasi kikubwa ushiriki wa Sekta Binafsi. Sekta Binafsi ya ndani ambayo ndiyo ingetoa mchango ambao ungeleta manufaa zaidi kwa nchi bado ni changa na hivyo haina uwezo wa kushiriki kwa kiwango ambacho Serikali inakitegemea. Aidha, Kamati haijaweza kuthibitisha kama Serikali imeweza kukaa na Sekta Binafsi na kuweka mikakati itakayowezesha Sekta Binafsi kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mipango ya Serikali. Bado kuna umuhimu mkubwa wa Serikali kuitengenezea mazingira mazuri sekta binafsi ya

kufanya biashara na kushirikiana na Serikali katika utekelezaji wa miradi ya kimkakati ya maendeleo.

## 2.4 MISWADA YA SHERIA ILIYOPITISHWA NA KAMATI YA BAJETI

### 2.4.1 Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kwamba tarehe 08/06/2016, Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha Bungeni Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2016/17, na kuelezea hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo zitakazochukuliwa na Serikali kwa madhumuni ya kupata Mapato ya kugharamia Bajeti yake kwa mwaka wa fedha 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza suala hili, Kamati ilipitia na kujadili Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 na kushauriana na Serikali katika maeneo mbalimbali ya muswada yaliyohitaji ufanuzi. Aidha, Kamati ilikutana na wadau mbalimbali wa masuala ya kodi na kupata maoni yao kipitia kikao cha wadau (*Public Hearing*). Kipitia vikao hivi, Kamati iliweza kuona mantiki ya Serikali kuhusu mapendekezo iliyoyaleta yaliyokuwa na lengo la kubainisha kisheria hatua kadhaa za mfumo wa kodi na ushuru kwa kuweka, kurekebisha, kupunguza au kufuta viwango vya kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali. Kamati ilikamilisha jukumu hili kwa kuwasilisha Bungeni maoni na mapendekezo yake kuhusu Muswada wa Fedha wa mwaka 2016 na baada ya majadiliano Bunge lako Tukufu liliidhinisha hatua mbalimbali za kodi, ushuru, ada na tozo mbalimbali zilizoanza kukusanywa na Serikali kuanzia tarehe 1 Julai, 2016.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muhtasari Sheria zifuatazo zilifanyiwa marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016;

i      **Sheria ya Makampuni, Sura 212**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilirekebisha katika kifungu cha 458 ili kuweka sharti kwa Msajili wa Makampuni kuwasilisha kwa Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania taarifa zitakazowezesha utekelezaji wa Sheria mbalimbali za kodi.

ii      **Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, Sura 306**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilifanyiwa marekebisho kwa kufuta kifungu cha 26 na kukiandika upya ili;

- a) Makampuni ya mawasiliano yenyе leseni ya kujenga miundombinu ya mawasiliano (Network Facilities) na yenyе leseni ya kutoa huduma za mawasiliano ya simu ya kielektroniki (Network Services or Application Services) kuwa na umiliki wa watanzania usiopungua asilimia 25 ya mtaji wa Kampuni katika kipindi chote cha uhai wa leseni yake;
- b) Kwa makampuni yenyе leseni ya huduma ya utangazaji (Content Service Licensee) kuwa na umiliki wa kitanzania usiopungua asilimia 51 ya mtaji katika kipindi chote cha leseni;
- c) Kiwango cha chini cha asilimia 25 ya umiliki upatikane kupitia umiliki wa umma kwa mujibu wa Sheria ya Soko la Mitaji na Dhamana;
- d) Makampuni yaliyoainishwa hapo juu ambayo tayari yalikuwa yanafanya biashara nchini kabla ya tarehe 01 Julai, 2016, yanatakiwa yajisajili katika soko la Hisa ndani ya kipindi cha miezi 6 kuanzia tarehe 1 Julai, 2016.
- e) Makampuni ambayo yatasajiliwa kuanzia tarehe 01 Julai, 2016 yatatakiwa kujisajili katika soko la hisa na kuuza hisa ndani ya miaka 2 toka kuanzishwa kwake.

iii **Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilirekebishwa katika kifungu mbalimbali kwa malengo yafuatayo:-

- a) Marekebisho ya kifungu cha 124 kifungu kidogo cha 6A kwa lengo la kuzuia ukwepaji kodi kwa baadhi ya kampuni za simu zisizo waaminifu kwa kutoza ushuru wa bidhaa wa asilimia 10 kwenye ada zinazotozwa na watoa huduma ya simu katika kutuma na kupokea fedha badala ya ushuru huo kutozwa tu kwenye kutuma fedha pekee.
- b) Kuongeza ushuru kwenye samani zinazoagizwa kutoka nje kwa lengo la kuhamasisha matumizi ya samani zinazotengenezwa kwa kutumia malighafi zinazozalishwa hapa nchini, kuongeza ajira na kuongeza mapato ya Serikali.
- c) Kufanya marekebisho ya viwango maalum vya kodi (specific duty rates) vya bidhaa zisizo za petrol kwa kiwango cha mfumuko wa bei wa asilimia 5.

- d) Upigaji marufuku utengenezaji, uuzaji, ununuzi na matumizi ya mifuko ya plastiki yenyewe kipimo cha unene chini ya microns 50;
- e) Kuondolewa kwa misahama ya kodi kwa vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa kuwapa posho kwa ajili ya mahitaji muhimu. Posho hii kwa sasa inatolewa kwa vyombo vya ulinzi na usalama.

iv **Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilirekebishwa katika kifungu mbalimbali kwa malengo yafuatayo:-

- a) Kupunguza kiwango cha chini cha kutoza kodi ya mapato yanayotokana na ajira kutoka asilimia 11 hadi asilimia 9.
- b) Kuweka mfumo maalum wa kuzuia upotevu wa mapato kwenye sekta ya madini, gesi na mafuta. Mabadiliko haya yalifanyika kwa kurekebisha vifungu mbalimbali pamoja na kutoa tafsiri ya baadhi ya maneno ambayo yalikuwa yanatoa mwanya wa ukwepajji wa kodi katika sekta ya madini, gesi na mafuta.

v **Sheria ya Utawala wa Mahakama, Sura 237**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilifanyiwa marekebiso katika kifungu cha 53(3) ili kumpa mamlaka Waziri mwenye dhamana na masuala ya Mahakama kuwasilisha Bungeni bajeti ya Mfuko wa Mahakama, badala ya Waziri mwenye dhamana na masuala ya fedha kama ilivyo hivi sasa. Lengo la marekebiso ni kuleta usimamizi katika utekelezaji wa Bajeti ya Mfuko wa Mahakama.

vi **Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa Sura 290 Kwanza,**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilifanyiwa marekebiso ili kuondoa mgongano wa kisheria baina ya Sheria hii na marekebiso yanayopendekezwa chini ya Sheria ya Kodi za Majengo, Sura 289 ili kuiwezesha TRA kukusanya kodi ya majengo.

vii **Jedwali la Kwanza la Sheria ya Magari (Kodi ya Usajili na Uhamisho wa Umiliki)**

**Mheshimiwa Spika**, Jedwali hili lilirekebishwa katika Sura 124 ili kulinda thamani halisi ya fedha na kuongeza mapato ya Serikali kwa kurekebisha aya ndogo ya 3 ili kuongeza viwango vya usajili wa magari kutoka shilingi 150,000 hadi shilingi 250,000 kwa kila gari, kupandisha ada ya usajili wa namba binafsi za magari kutoka shilingi 5,000,000 hadi shilingi 10,000,000 kwa kila baada ya miaka mitatu

pamoja na kuongeza viwango vya usajili wa pikipiki kutoka shilingi 45,000 hadi shilingi 95,000 kwa kila pikipiki;

viii **Sheria ya Utawala wa Bunge, Sura 115**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 29 (3) kilirekebishwa ili kuwezesha bajeti ya mfuko wa Bunge kuwasilishwa Bungeni na Waziri mwenye dhamana na masuala ya Bunge badala ya Waziri wa fedha kama ilivyo hivi sasa. Lengo la marekebisco haya ni kuleta uwajibikaji katika usimamizi wa Bajeti ya Mfuko wa Bunge.

ix **Sheria ya Reli, Sura 170,**

**Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 20A kilirekebishwa ili kuongeza orodha ya bidhaa ambazo hazitatozwa tozo ya reli. Bidhaa hizo ni pamoja na madawa na vifaa vya madawa, mbolea na bidhaa zilizopewa msamaha wa ushuru wa forodha kwa mujibu wa Jedwali la Tano la Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la hatua hii ni kuondoa ukinzani uliopo baina ya Sheria hii na Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.

x **Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania Sura 399**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilifanyiwa marekebisco ili kuipa uwezo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kukusanya kodi ya majengo pamoja na mapato mengine yasiyo ya kodi yanayokusanya na Taasisi nyingine za Serikali.

xi **Sheria ya Utawala wa Kodi, Sura 438**

**Mheshimiwa Spika**, Sheria hii ilifanyiwa marekebisco, ili kuiwezesha TRA kutoza kodi sahihi kwenye mikataba ya kupangisha nyumba, katika maeneo mbalimbali hususan pale ambapo mikataba husika imeghushiwa ili kubainisha kiwango kidogo cha kodi ya pango kwa lengo la kukwepa kodi, kuweka sharti kwa kampuni zinazojishughulisha katika sekta ya ujenzi, madini, mafuta na gesi kuwasilisha taarifa ya wakandarasi wanaotoa huduma katika sekta hizo kwa Kamishna Mkoo wa Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Sheria hii pia ilimpa mamlaka Waziri wa Fedha baada ya kufanya mashauriano na Kamishna Mkoo wa Mamlaka ya Mapato, kusamehe riba inayotozwa kwa walipa kodi wanaochelewa kulipa kodi, iwapo ataona kuna sababu ya msingi ya kusamehe riba husika.

Sheria hii mpya pia inaweka adhabu kwa walipa kodi wanaochelewa kulipa kodi pamoja na kuweka adhabu dhidi ya makosa ya kutotumia mashine za kodi za kielektroniki (FFD). Lengo la mapendekezo haya ni kuongeza kiwango cha adhabu ili kutekeleza uamuzi wa Serikali wa kuhakikisha wafanyabiashara wanatumia mashine za kodi za kielektroniki.

xii     **Sheria ya Kodi ya Majengo Sura 289**

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ili kuweka utaratibu utakaotumiwa na Waziri mwenye dhamana ya Fedha kwa kushirikiana na Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa katika kukusanya kodi ya pango.

xiii    **Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura 148**

Mheshimiwa Spika, Sheria hii ilirekeblishwa kwa malengo yafuatayo:-

- a) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) pale ambapo bidhaa moja inakuwa imesamehewa kodi kwa kiasi fulani na kiasi inatozwa kodi. Pia
- b) Kuwezesha bidhaa zinazotengenezwa Tanzania Bara na kuuzwa Zanzibar zitozwe Kodi ya Ongezeko la Thamani upande wa Zanzibar. Lengo la hatua hii ni kuondoa utaratibu uliokuwepo hapo awali wa kufanya marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenda Zanzibar kwa kuwa Sheria ya Kodi hiyo inayotumika sasa haina kifungu kinachoruhusu marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenda Zanzibar kama ilivyokuwa kwenye sheria iliyofutwa. Kwa kuwa kila upande wa Muungano unayo Sheria yake ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, kodi hii itatozwa sehemu ambako bidhaa au huduma itatumika, yaani “destination principle”. Kwa msingi huo, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar itakuwa inakusanya kodi hii kwa bidhaa zinazozalishwa Tanzania Bara na kupelekwa Zanzibar.

**Marekebisho katika Sehemu ya Kwanza ya Jedwali la Msamaha wa VAT**

Marekebisho katika jedwari hili yalifanyika ili;

- a) Kuongeza vifaa vya kilimo vilivyosamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani;
- b) Kusamehe VAT kwenye maharage ya soya, mbogamboga zote na mazao ya mifugo yakiwa hayajasindikwa kama yanavyoonekana kwenye Sheria ya Ushuru wa Forodha ya Jumuia ya Afrika Mashariki.

- c) Kuongeza vitamini na virutubishi kwenye orodha ya vifaa na madawa muhimu yaliyoidhinishwa na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa ajili ya kupata msamaha wa kodi na pale vitakapouzwa au kuingizwa nchini na Taasisi za Serikali. Vitamini na virutubishi hivyo huongezwa kwenye vyakula ili kuboresha lishe kama njia mojawapo ya kuimarisha afya ya jamii;
- d) Kuondoa msamaha wa VAT kwenye vipuri vya ndege;
- e) Kuondoa msamaha wa VAT kwenye vyombo vyote vya ulinzi na usalama kwa kuwapa posho kwa ajili ya mahitaji muhimu;

**Marekebisho ya Jedwali hili yaliyopingwa kwa kiasi kikubwa na wafanyabiashara na baadhi ya wabunge**

- a) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye ada za huduma za kibenki zinazotozwa na benki hizo ili kupanua wigo wa kodi isipokuwa huduma zinazotolewa bila malipo ya ada.
- b) Kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye huduma za utalii hususan kuongoza watalii, kuendesha watalii, utalii wa majini, kuangalia wanyama na ndege wa porini, kutembelea hifadhi na usafirishaji wa watalii ardhini.

**xiv Sheria ya Elimu na Mafunzo ya Ufundis stadi, Sura 82**

Sheria hii ilifanyiwa marekebisho ili kupunguza tozo ya kuendeleza ufundis stadi kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 5 hadi asilimia 4.5. Lengo la hatua hii ni kuwapatia nafuu ya mzigotozo wa tozo waajiri na kuhamasisha ulipaji wa kodi kwa hiari pasipo shuruti.

**Maeneo mengine yaliyofanyiwa marekebisho kwenye Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016**

- a) Kuorodhesha Wakala na Taasisi zote za udhibiti na usimamizi zilizo chini ya Msajili wa Hazina kuchangia asilimia 15 ya mapato yake ghafi katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Aidha, Taasisi ya Arusha International Conference Centre iliondolewa katika orodha ya Taasisi zinazotakiwa kuchangia asilimia 15 ya mapato ghafi, badala yake iliorodheshwa katika orodha ya taasisi zinazotakiwa kutoa gawio (Dividend) kwa Serikali kwa sababu taasisi hii inafanya biashara.

### **Hatua imetekelozwa na Waziri wa Fedha na Mipango.**

- b) Kufuta baadhi ya ada na tozo zinazotozwa na Mamlaka ya Chakula na dawa. **Hatua hii imetekelozwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Afya.**
- c) Kufuta baadhi ya ada na tozo zinazotozwa na Bodi ya Pamba, Bodi ya Chai, Bodi ya Kahawa na Bodi ya Korosho. **Hatua hii imetekelozwa na Waziri mwenye dhamana ya masuala ya Kilimo.**

#### **2.4.2 Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma wa Mwaka 2016 (The Public Procurement (Ammendment) Act 2016)**

**Mheshimiwa Spika**, tarehe 28 Juni 2016 Kamati iliwasilisha Bungeni maoni na mapendekezo yake kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma. Bunge lilipitisha muswada huo kwa lengo la kuongeza ufanisi katika ununuzi wa Umma kwa kuondoa mapungufu yaliyopo katika Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 kwa kupunguza gharama na muda wa michakato ya manunuzi Serikalini. Aidha, Muswada huo mpya ulitegemewa kutoa upendeleo kwa kampuni za ndani, vikundi maalum, malighafi na bidhaa zinazozalishwa nchini pamoja na kuweka viwango mahsus kwa bidhaa zitakazotumiwa na Serikali. Muswada huo ulisaini kuwa Sheria tarehe 7 Julai, 2016 na Mheshimiwa Rais.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla Sheria ya Ununuzi wa Umma kuitia muswada huo imefanyiwa marekebisho yafuatayo:-

- a) Kuweka sharti la kutenga kazi kwa ajili ya wakandarasi wa ndani kwa kuhusisha wazabuni wa ndani katika manunuzi na kuwajumuisha au kuwashirikisha kwenye kazi hizo pamoja na wazabuni wa nje.
- b) Kuweka kifungu cha dharura ili kuwezesha vitu vya kuokoa uhai na vinginevyo kununuliwa kwa dharura pindi inapobidi.
- c) Kutoa fursa kwa Taasisi na Makampuni ya Umma yanayofanya biashara kuwa na utaratibu wake wa kufanya maamuzi ili yaweze kuijendesha kibiashara.
- d) Kuweka masharti ya kufanya manunuzi kwa kuzingatia thamani ya fedha kwa bidhaa mbalimbali zitakazotumika Serikalini ikiwemo ununuzi wa magari.

- e) Kuondoa sharti la kuwepo kwa mikataba baina ya Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) na wazabuni iliyofungamanishwa na bei. Hatua hii itaondoa upangaji wa bei elekezi kwa watoa zabuni, kupunguza urasimu na kuongeza uwazi na uwajibikaji katika manunuzi ya Serikali.
- f) Kupunguza muda wa mchakato wa manunuzi pamoja na muda wa mzabuni kuwasilisha malalamiko kwa Afisa Masuuli kutoka siku 28 hadi siku 7;
- g) Kurekebisha Kanuni ili kupunguza muda wa mchakato wa zabuni za ununuzi wa bidhaa, kandarasi za ujenzi na huduma kutoka wastani wa siku 91 zilizobainishwa katika Kanuni hadi siku 49 kwa zabuni za kimataifa na kutoka wastani wa siku 100 hadi siku 56 kwa zabuni za kimataifa.

## **2.5 UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KATIKA KIPINDI CHA ROBO YA KWANZA YA MWAKA WA FEDHA 2016/17**

### **2.5.1 Mapato ya Serikali**

#### **a) Mapato ya Ndani**

**Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha robo ya kwanza ya Mwaka wa fedha 2016/17 **mapato ya kodi** yalifikia shilingi bilioni 3,462.5 sawa na asilimia 99 ya lengo la kukusanya bilioni 3,509.1. takwimu zinaonyesha kodi zilizovuka lengo ni pamoja na ushuru wa forodha (asilimia 105), ushuru wa bidhaa nje (asilimia 105), na kodi ya Ongezeko la Thamani ndani (asilimia 117). Hata hivyo kodi ya ushuru wa bidhaa ndani (asilimia 91), kodi ya Ongezeko la Thamani nje(asilimia 88) na Kodi ya mapato (asilimia 95) hazikuweza kufikia malengo ya robo mwaka.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **mapato yasiyo ya kodi** yalifikia shilingi bilioni 362.5 sawa na asilimia 54 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 672.0. Aidha, **mapato ya Halmashauri** yalikuwa shilingi bilioni 117 sawa na asilimia 70 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 166.4. Mwenendo wa takwimu hizi unaonyesha kuwa bado Serikali ina kazi ya zaidi kuhakikisha inafikia malengo iliyojivekea katika maeneo haya ili kuweza kugharamia bajeti yake.

**Mheshimiwa Spika**, Serikali katika kipindi cha robo mwaka ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17 Serikali ilikopa jumla ya shilingi bilioni 1,115 sawa na asilimia 83 ya lengo la shilingi bilioni 1,344.

b) **Misaada na mikopo ya masharti nafuu na masharti ya kibashara kutoka nje**

**Mheshimiwa Spika**, mwaka wa fedha 2016/17 washirika wa maendeleo walihidi kutoa kiasi cha shilingi bilioni 3,600.8. Kati ya fedha hizi, shilingi bilioni 483 ni misaada na mikopo ya kibajeti, shilingi bilioni 372 ni Mifuko ya Pamoja ya Kisekta na shilingi bilioni 2,745 ni Miradi ya Maendeleo. Hata hivyo takwimu zinaonyesha hadi kufiki mwezi Septemba 2016 kiasi kilichopokelewa ni shilingi bilioni 285, sawa na asilimia 16 ya lengo la robo mwaka kwa mchanganuo wa mikopo na misaada ya kibajeti shilingi bilioni 36 (sawa na asilimia 80), Mifuko ya Pamoja ya Kisekta bilioni 57 (sawa na asilimia 36) na miradi ya maendeleo shilingi bilioni 192 (sawa na asilimia 12) ya lengo la robo mwaka. Aidha, kwa upande wa mikopo yenye masharti ya kibashara bado Serikali inaendelea kufanya majadiliano na taasisi za fedha za kimataifa pamoja na mabenki kuweza kupata mikopo hiyo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kama ilivyoidhinishwa kwenye bajeti ya Mwaka 2016/17.

**Mheshimiwa Spika**, sura hii inaonyesha bado tunachangamoto kubwa ya kuweza kugharamia bajeti yetu kwa kutegejemea fedha za wafadhili na hivyo kuna uwezekano mkubwa tusiweze kufikia malengo yetu hasa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

### 2.5.2 Matumizi ya Serikali

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa matumizi, Serikali imeendelea kuwanisha na mapato yanayopatikana katika kipindi cha robo mwaka na kipaumbele kimekuwa kwa matumizi yasiyoepukika hasa kwenye mishahara, matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo. Takwimu zinaonyesha kuwa katika kipindi cha robo kwanza ya Mwaka 2016/17, Serikali ilitoa mgawo wa fedha wa shilingi bilioni 5,624.6 (sawa na asilimia 92 ya lengo); ambapo kwa ajili ya matumizi ya kawaida Serikali ilitoa shilingi bilioni 4,388.2 (sawa na asilimia 101 ya lengo) na matumizi ya maendeleo shilingi bilioni 1,199.2 (sawa na asilimia 69 ya lengo).

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kwamba, pamoja na Serikali kuweza kuvuka lengo la kupeleka fedha za matumizi ya kawaida, hata hivyo Serikali haikupeleka fedha yoyote kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za utawala kwa Halmashauri zote nchini. Pia, Serikali ilipeleka asilimia 19 tu ya fedha za matumizi ya kawaida zilizotengwa kwa ajili ya kugharamia sekta ya afya. Hali hii imesababishwa na baadhi ya mafungu kupewa fedha nyingi zaidi ya zile zilizokuwa zimepangwa kutolewa katika kipindi husika.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na azma ya dhati ya Serikali ya kukamilisha miradi ya maendeleo, kamati haikuridhishwa na Serikali kutofikia lengo la upelekaji wa fedha za maendeleo katika robo ya kwanza ya bajeti ya Mwaka wa fedha 2016/17. Takwimu zinaonyesha kuwa ni mafungu yaliyoathirika zaidi ni pamoja na Ofisi ya Bunge (asilimia 0); Tume ya Taifa ya Umwagiliaji (asilimia 0); Wizara ya Mifugo (asilimia 0); Idara ya Zimamoto na uokoaji (asilimia 0); na Mamlaka za Serikali za Mitaa (wastani wa asilimia 57 tu).

## 2.6 MWONGOZO WA KUTAYARISHA MPANGO NA BAJETI YA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Bajeti ina jukumu la kujadili na kutoa maoni na ushauri kuhusu uandaaji wa mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kila mwaka. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kamati ilikutana na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kupitia na kujadili Taarifa ya Serikali kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2016/17. Kimsingi, Kamati iliridhika na maelekezo ya Serikali katika vyombo husika hasa kuhusu utaratibu wa utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini za Mipango na Bajeti zao ili kuhakikisha matumizi mazuri ya fedha za Serikali (*value for money*) kama miongozo ya kisheria inavyoelekeza, pamoja na namna bora ya ukusanyaji wa mapato na utengaji wa rasilimali fedha kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, mapendekezo ya mwongozo yalielekeza namna ya kutayarisha Mipango ya Maendeleo kwa Wizara, Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi na wadau wengine kwa kuzingatia utekelezaji wa sera za fedha na kodi tukielekea mwaka wa fedha 2017/18.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na mapitio hayo, Kamati iliishauri Serikali kuhusu uhuhishaji wa Mfumo wa Programu wa kibajeti na vipaumbele vilivyowekwa ili kuhakikisha tunatanzua vikwazo vya ukuaji wa uchumi na tunajenga uchumi wa viwanda na maendeleo ya rasilimali watu '*Nurturing Industrialization for Economic Transformation and Human Development*'. Pia Kamati iliishauri Serikali kuhusu kuongeza wigo wa kukusanya kodi kwa kuzingatia ubunifu wa vyanzo vipyta vya mapato; kutafuta namna bora ya upatikanaji wa fedha kupitia sekta binafsi kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo; pamoja na usimamizi, ufuatiliaji na utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya majadiliano na Serikali, Kamati iliwasilisha taarifa yake kuhusu maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu Mwongozo wa kutayarisha Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2017/18, ambayo iliwasilishwa na kuridhiwa na Bunge tarehe 02 Novemba 2016.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko tuliloainisha kwenye Bajeti ya Serikali tunayoitekeleza sasa bado kuna changamoto kubwa katika upelekaji wa fedha kwa wakati kwa mafungu husika kama zilivyoidhinishwa na Bunge na hivyo kusababisha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kuwa sio wa kuridhisha kwenye baadhi ya mafungu ukilinganisha na taarifa za makusanyo ya fedha zinazotolewa. Ni vema Serikali ikaangalia kwa umakini suala hili na kutafuta ufumbuzi mapema iwezekanavyo.

## 2.7 UTAFITI NA UCHAMBUZI KWA AJILI YA KAZI ZA KAMATI

### 2.7.1 Maelezo ya ujumla

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu kufanya utafiti na uchambuzi wa Sera za Kodi, Sera za Fedha na Sera za kiuhasibu zilizopendekezwa na Serikali, Kamati ilijitahidi kutekeleza jukumu hili kwa kushirikiana na wataalamu mbalimbali wa masuala ya fedha na kodi ambao wameisaidia Kamati katika kutoa uelewa kuhusiana na masuala husika.

**Mheshimiwa Spika**, Suala la kufanya utafiti na uchambuzi ni pana na endelevu linalohitaji ushirikishwaji wa wadau mbalimbali wenyewe taaluma na weledi wa masuala husika. Kamati itaendelea kutumia wataalamu wake wa Ofisi ya Bunge pamoja na wataalamu mbalimbali kutoka Serikalini na Sekta Binafsi ili kuhakikisha inakabiliana na changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Aidha, bado kuna umuhimu mkubwa wa kuendelea kuimarisha Idara ya Bajeti ya Ofisi ya Bunge ili iweze kuendelea kufanya tafiti na chambuzi nzuri zaidi kulingana na mabadiliko ya maendeleo ya kiuchumi na kisheria yanayoendelea kutokea nchini na duniani kwa ujumla.

### 2.7.2 Mapitio ya utekelezaji wa Kamati Maalum ya Spika ya mwaka 2012 (Chenge I)

**Mheshimiwa Spika**, itakumbukwa kuwa tarehe 26 Juni, 2012, Mheshimiwa Spika Mstaafu Anne Makinda aliunda Kamati Maalum kwa madhumuni ya kulishirikisha Bunge kikamilifu katika kuishauri Serikali kuhusu namna bora zaidi ambayo Serikali itaongeza mapato yake na kuyatumia ipasavyo kwa manufaa ya Taifa. Hivyo, Kamati ilijielekeza kuangalia ufanisi wa Serikali katika ukusanyaji wa Mapato kutoka kwenye vyanzo vilivyopo; Kuangalia na kuainisha vyanzo vipyta vya mapato ili kuishauri Serikali; Kuangalia vyanzo vinavyoweza kufanyiwa kazi katika Mwaka huu wa Fedha; Kuangalia vyanzo vitakavyoweza kufanyiwa kazi katika Mwaka mwingine wa Fedha pamoja na Kuangalia Jambo lingine lolote lile ambalo Kamati iliona linafaa kulifanyia kazi

**Mheshimiwa Spika**, Kamati Maalum iliwasilisha Taarifa yake Mwezi Februari 2013 kwa Mhe. Spika ili aweze kuishauri Serikali ipasavyo. Kwa mantiki hiyo, Kamati ya Bajeti iliweka utaratibu wa kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo hayo kwa kushauriana na Serikali na Sekta Binafsi ili kupata picha halisi ya mapendekezo yaliyofanyiwa kazi, yanayoendelea kufanyiwa kazi na ambayo hayajafanyiwa kazi kabisa; na hivyo Bunge lako tukufu kujua sababu za utekelezaji wa hatua hizi katika kipindi cha miaka mitatu (2013-2016).

**Mheshimiwa Spika**, Tarehe 01 Septemba, 2016 Waziri wa Fedha na Mipango aliwasilisha mbele ya Kamati, Taarifa ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati Maalum ya Bunge kuhusu Mapato na Matumizi (Chenge 1). Taarifa ya Waziri wa Fedha na Mipango ilionyesha kwamba kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza mapendendekezo husika.

**Mheshimiwa Spika**, kwa muhtasari tuu Kamati imeridhika na maelezo ya Serikali katika baadhi ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa katika Taarifa ya Chenge I. Maeneo hayo ni yafuatayo:-

**a) Kuongeza ukusanyaji wa mapato kwa kila mwaka ukilinganisha na pato la taifa pamoja na kupunguza misamaha ya kodi;** Bunge lilitunga Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 pamoja na kufanya marekebisho mbalimbali kwenye Sheria za Fedha na Kodi zikiwemo Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (2015), Sheria ya Utawala wa Kodi (2014), Sheria ya Ununuzi wa Umma (2016) na Sheria ya Fedha ambazo kimsingi zimeweza kusaidia kupunguza misamaha ya kodi pamoja na kusimamia matumizi ya serikali kwa kiasi kukubwa. Aidha mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa kodi na malipo imeweza kufanyiwa marekebisho ili kuhakikisha mapato yanaendelea kuongezeka mfano matumizi ya ‘Electronic Fiscal Device’ (EFD), TANCIS, EPICOR-IFMs na TISS, pamoja na uboreshaji wa utayarishaji wa hesabu kwa viwango vya kimataifa (IPSAS Accrual).

**b) Sekta Nishati ya Umeme, mafuta na gesi;** Serikali imefanikiwa kuboresha usimamizi wa Sekta ya Nishati kwa kutunga Sera ya Taifa ya Nishati ya Mwaka 2015 (*The National Energy Policy 2015*); Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015 (*The Petroleum Act 2015*); Sheria ya Kusimamia Mapato ya Mafuta na Gesi Asilia ya Mwaka 2015 (*The Oil and Gas Revenue Management Act, 2015*); na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika Rasilimali za Madini, Mafuta na Gesi Asilia Tanzania ya Mwaka 2015 (*The Tanzania Extractive Industries (Transparency and Accountability) Act, 2015*); na Mkataba Kifani wa Uzalishaji na Ugawanaji wa Mapato ya Mafuta na Gesi wa Mwaka 2013 (*Model Production Sharing Agreement 2013*). Rasimu za Kanuni za sheria hizo zinaendelea kukamilishwa. Aidha, Serikali imeendelea kufanya mazungumzo kati yake na makampuni

mbalimbali yaliyowekeza katika uzalishaji wa gesi ili kuwezesha uchimbaji wa visima vipyta na hivyo kuweza kukidhi mahitaji ya ujazo wa bomba la gesi;

**c) Huduma za Viwanja vya Ndege;** Viwango vipyta vya ada za leseni ya usafiri wa anga, leseni za ground handling na air services vya mwaka 2003 vimehuishwa na kuanza kutumika 2013, mradi wa ukarabati na upanuzi wa jengo la pili la abiria (Terminal II) unaendelea; ukarabati na upanuzi wa viwanja mbalimbali vikiwemo vya mwanza, Dodoma, na Dar es Salaam unaendelea. Aidha, Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanikiwa kununua Ndege kubwa mbili aina ya (Bombardier) pamoja na mpango wake wakuongeza ndege nyingine tano siku za usoni lakini inaendelea kusisitiza umuhimu wa kusimamia vizuri ndege hizo ili Serikali iweze kutoa huduma na kuongeza mapato kupitia ndege hizo;

**d) Bandari, barabara na reli;** mradi wa kuwaunganisha pamoja watoa huduma kwa njia ya mtandao (Single Window System) umekamilika na sasa unauhishwa pamoja na mradi wa TANCIS uliowekwa na Mamlaka ya Mapato (TRA), mizigo yote ya nchini (local import) inapelekwa ICD isipokuwa ile ambayo iko katika makontena yanayotakiwa kubaki bandarini (LCL), Mamlaka ya Bandari imeboresha miundo na mifumo yake kiutendaji. Pia, Serikali imeendelea kukarabati na kujenga barabara mbalimbali nchini katika kiwango cha lami pamoja na kuendelea kukarabati miundombinu ya reli.

**e) Mawasiliano ya simu za mkononi;** mabadiliko yaliyofanyika kwenye Sheria mpya ya VAT ya mwaka 2014 ilioanza kutumika Julai 2015, imejumuisha utozaji wa kodi wa huduma zote za simu zilizopendekezwa na Kamati. Aidha, Serikali bado inaboresha mtambo wa Telecommunication Traffic Monitoring System (TTMS) ili kuweza kutambua mapato ya miamala ya simu za ndani na huduma nyinginezo (on-net); Hata hivyo, pamoja na hatua iliyofikiwa na Serikali katika eneo hili, Kamati haikupata taarifa ya ukamilishaji wa uboreshaji wa mtambo wa huo ili uweze kukamata miamala ya mawasiliano ya simu za ndani.

**f) Miradi ya chuma na makaa ya mawe ya Liganga na Mchuchuma;** Mradi huu ni wa ubia kati ya Serikali kupitia NDC na Sichuan Hongda Group Company kutoka China. Uwekezaji katika miradi hii miwili ni takribani Dola za Marekani Bilioni 3.0. Aidha, hisa za Serikali ni asilimia 20 na Sichuan Hongda Group Company asilimia 80. Ujenzi wa mgodi na kituo cha kufua umeme kutohana na makaa ya mawe unatarajiwa kuanza robo ya kwanzu ya mwaka 2017 na uzalishaji wa umeme unategemewa kuanza mwaka 2019/20.

- g) Maliasili na Utalii;** Serikali imeimarisha usimamizi wa mazao misitu kwa kufanya marekebisho ya miongozo ya Uvunaji endelevu wa mazao ya misitu (katika misitu ya asili, mikoko na mashamba ya miti) pamoja na tozo kwa huduma na mazao ya misitu (GN 324 ya Agosti, 2015). Miongozo hiyo inahimiza udhibiti wa uvunaji na usafirishaji wa mazao ya misitu kwa kuzingatia masharti na taratibu zilizoainishwa. Serikali imeanzisha Tozo ya maendeleo ya Utalii (TDL), ili baadhi ya fedha za Tozo hiyo zitumike kugharamia shughuli ya Utangazaji; aidha, Wizara kupitia mashirika yake kama TANAPA, NCAA na TTB imekuwa ikihamasisha utalii wa ndani kwa kuratibu matamasha na kupunguza bei kwenye tozo za vivutio vya utalii.
- h) Ardhi;** Serikali imeimarisha upigaji wa picha katika maeneo mbalimbali kwa kujenga kituo cha kupokea picha za anga (*direct satellite receiving station*) na hivyo kurahisisha uthaminishaji na upimaji ardhi. aidha, serikali imetenga mipango yake katika muda mfupi, kati na mrefu ili kuhakikisha inaimarisha upimaji wa ardhi na kupunguza migogoro ya ardhi ili kuongeza mapato ya Serikali kupitia sekta hii.
- i) Uvuvu;** imanza kufanya marekebisho ya kanuni za Mamlaka ya Kusimamia Uvuvu wa Bahari Kuu ya 2009 kwa kuongeza ada za leseni na ada za huduma kwa meli za uvuvu na meli zinazosaidia uvuvu, Vessel Monitoring System (VMS) na Masharti ya Leseni ya uvuvu wa Ukanda wa Uchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone-EEZ). Uvuvu wa Bahari kuu ni eneo ambalo Serikali imekuwa ikipoteza mapato mengi kwa kutolisimamia ipasavyo.
- j) Madini;** Suala la '**super profit tax**' limeshaanza kufanyiwa kazi na Serikali kwa kuangalia Makubaliano ya Namna ya Kugawana Mapato ya Uzalishaji ambayo Serikali huingia na makampuni ya madini kwenye kipengele cha kutoza kodi kwenye faida kubwa ya ziada (additional profit tax-APT) kama ilivyoelekezwa na "Model Production Sharing Agreement"; Ukaguzi wa hesabu za fedha na kodi za migodi mikubwa ya dhahabu umeendelea chini ya TMAA.
- Mheshimiwa Spika;** Hata hivyo bado yapo mapendekezo kadhaa ambayo hayajafanyiwa kazi na Serikali kwa sababu mbalimbali. Baadhi ya mapendekezo hayo ni kukamilisha utafiti na tathmini ya ukusanyaji wa mapato kupitia vyanzo vya bahari kuu; Kukamilisha kanuni za sheria za kusimamia mapato ya mafuta na gesi asilia ya Mwaka 2015 na Sheria ya Uwazi na uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia Tanzania ya mwaka 2015; Kulipa deni la TANESCO ambalo hadi mwezi Agosti 2016 lilifikia takribani shilingi bilioni 794.9; na Kukamilisha miradi mbalimbali ya nishati ya umeme ikiwemo kinyerezi na miradi miradi mingine ya nishati mbadala inayoendeshwa

kwa nguvu ya maji (hydro), jotoardhi (geothermal), upepo (wind power) na umeme wa juu (solar power).

## 2.8 MAFUNZO NA SEMINA KWA KAMATI YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Mwezi Januari – Desemba 2016, wajumbe wa Kamati walipata mafunzo machache ya ndani (local training) kuhusu usimamizi na utekelezaji wa Sheria ya Bajeti, Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na masuala mbalimbali ya kibajeti na kiuchumi yanayohusu sekta binafsi ambayo kwa kiasi fulani yalisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, Kamati haikupata fursa ya kupata mafunzo ya nje ambayo yangeweza wajumbe wa Kamati kuongeza ujuzi na uwezo wa kusimamia ipasavyo masuala ya kibajeti na uchumi.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuimarisha uwezo wa Kamati na Bunge lako ili liweze kusimamia ipasavyo Sheria ya Bajeti na kuisadia Serikali katika kutatua changamoto ya upatikanaji wa Mapato, Kamati inahitaji kupata mafunzo na uzoefu kutoka katika Mabunge mengine ambayo yana Kamati za Bajeti au Kamati zenyenye majukumu yanayofanana na Kamati hii, mathalani katika Mabunge ya nchi za Kenya, Uganda, Nigeria, Ghana au Australia ambayo yamepiga hatua kubwa katika usimamizi wa utekelezaji wa Bajeti zao.

## 2.9 VIKAO VYA KAMATI NA WADAU MBALIMBALI WA MASUALA YA BAJETI

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ingependa kuwatambua wadau wa masuala ya bajeti na uchumi ambao wameshirikiana na Kamati kikamilifu katika utekelezaji wa majukumu yake kwenye kipindi husika: -

- a) Serikali na baadhi ya taasisi zake kama Wizara ya Fedha na Mipango, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT), Ofisi ya Msajili wa Hazina (Treasury Register), Mamlaka ya Soko la Mitaji na Dhamana (CMSA);
- b) Sekta Binafsi, chini ya umoja wao (*Tanzania Private sector Foundation*) ambao Kamati ilikutana nao mara kadhaa kupata maoni yao kuhusu hatua na utekelezaji wa kodi nchini;
- c) Shirikisho la watoa Huduma za Utalii nchini (*Tourism Confederation of Tanzania*) ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia sekta ya utalii;

- d) Umoja wa watoa huduma za simu nchini (*Mobile Operators Association of Tanzania*) ambao walijadiliana na Kamati kuhusu namna bora ya kuongeza mapato ya Serikali kupitia sekta ya mawasiliano;
- e) Umoja wa wenyewe mabenki nchini (*Bankers Association of Tanzania*) ambao walijadiliana na Kamati masuala kadhaa ya kibenki na namna bora ya Serikali kupata mapato ya Serikali kupitia njia mbalimbali za kibenki;
- f) Umoja wa watoa huduma za Bima nchini (*Tanzania Insurers Association*) ambao walishauriana na Kamati kuhusu uwezekano wa kupanua huduma za bima hususan katika shughuli za bima ya uchimbaji wa gesi na madini; na
- g) *Tanzania Chamber of Minerals and Energy* ambao walishauriana na Kamati kuhusu kodi mbalimbali zinazotozwa kwa Kampuni za Madini na Nishati nchini.
- h) Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kujadili Taarifa kuhusu masuala ya usimamizi na uwekezaji katika biashara na masuala yanayohusu sera na sheria mbalimbali zinazosimamia utekelezaji wa majukumu yao.
- i) Presidential Delivery Bureau (PDB) kwa ajili ya kupokea na kujadili Taarifa kuhusu mwenendo wa upatikanaji wa vyanzo vipya vyia mapato (*Resource mobilization*)
- j) Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kwa ajili ya kupokea Taarifa kuhusu Hali ya Uchumi kwa mwaka 2015; na mwenendo wa riba ya dhamana za Serikali na mwenendo wa riba za mikopo (*loans*) na amana (*deposits*) kwenye mabenki ya biashara kwa kipindi cha miaka mitano (2011/12 - 2014/15).
- k) Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kujadili kuhusu Taarifa ya Mwenendo wa mikopo na misaada kutoka kwa wahisani kwa kipindi cha miaka mitano (2011/12-2014/15); Taarifa ya tathmini na mchanganuo wa Deni la Taifa na Uhimiliwu wake (*Taratibu za ukopaji wa ndani, taratibu za ukopaji wa nje, mchanganuo wa malipo ya ndani, mchanganua wa malipo ya nje*); na Mchanganuo wa miradi iliyofadhiliwa kutokana na Deni la Taifa.
- l) Asasi ya Kiraia (*Tanzania Coalition on Debt and Development - TCDD*) inayojihusisha na masuala ya Deni la Taifa na Maendeleo ambayo iliwaongezea wajumbe wa Kamati kuhusu masuala ya Deni la Taifa.

m) Wakala wa Ukaguzi wa Madini Tanzania (TMAA) kwa ajili ya kujadili kuhusu Taarifa za ukaguzi wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika Sekta ya Madini nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inawapongeza na kuwashukuru wadau na taasisi zote zilizoshirikiana na Kamati. Hata hivyo, Kamati inatoa angalizo kuwa haitajishughulisha na maoni au mapendekezo yasiyokuwa na tija na maslahi ya kitaifa.

### **3.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA KATIKA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA MWAKA 2015/16 NA ROBO YA KWANZA YA MWAKA 2016/17**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka wa fedha 2015/2016 na utekelezaji wa Bajeti ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17. Katika tathmini hiyo Kamati ilibaini masuala na changamoto kadhaa katika utekelezaji wa bajeti kama ifuatavyo:-

- a) Changamoto katika utekelezaji wa Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015 hususani kwa upande wa Serikali kuwasilisha kwa wakati Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa kipindi cha robo Mwaka na ushirikishwa wa wadau kwenye hatua za kibajeti zinazotekelzwa na Serikali.
- b) Ucheleweshaji wa kutolewa fedha na Hazina pamoja na upatikanaji kidogo wa mapato kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo;
- c) Washirika wa Maendeleo (Development Partners) kutokutoa kwa wakati au kutoa kwa kiwango pungufu cha fedha walizoahidi wakati wa maandalizi ya Bajeti na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- d) Ukuaji wa kasi wa Deni la Taifa ambao unaweza kusababisha Serikali kushindwa kugharamia utekelezaji wa bajeti yake;
- e) Urasimu mkubwa katika taratibu za manunuzi na uwezo mdogo wa wakandarasi wa ndani na hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa wakati;
- f) Serikali kutokuwa na ubunifu katika kufanya utafiti wa kupata vyanzo vypya vya mapato na pia kutochukua uamuzi wa haraka kutumia vyanzo vypya vya mapato vinavyopendekezwa na wadau wa masuala ya kodi;

- g) Ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Serikali kwa baadhi ya Wizara, Taasisi za Serikali na Halmashauri. Aidha, ukusanyaji mdogo wa kodi ya majengo hususan kwa maeneo ya Halmashauri ambayo Mamlaka ya Mapato (TRA) ilipaswa kukusanya kwa kuzingatia marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 umesababishwa na kuchelewa kukamilika kwa mifumo ya ukusanyaji kodi za Halmashuri unaoandaliwa na TRA.
- h) Serikali kutowasilisha kwa wakati Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya robo kwanza ya mwaka wa fedha 2016/17.
- i) Kuwepo kwa mwitikio mdogo wa matumizi ya mashine za kielektroniki (EFDs) kwa baadhi ya wateja na walipakodi.
- j) Uwepo wa watumishi hewa na wanafunzi huwa na hivyo kuigharimu Serikali fedha nyingi katika kulipa mishahara na kutoa mikopo ya elimu ya juu kwa watumishi na wanafunzi wasiostahili.
- k) Wigo mdogo wa Kodi unaosababishwa na kutofanyika kwa maboresho ya mfuko wa kodi ili uwe rafiki zaidi kwa wafanyabiashara wadogo; kutorasimishwa kwa sehemu kubwa ya shughuli za kiuchumi hususan wafanyabiashara wadogo ambao hawajasajili biashara zao.
- l) Serikali bado haijaweza kukamilisha zoezi la kutathmini uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni (*Sovereign credit ratings*) ili Serikali iweze kukopa mikopo yenye masharti nafuu katika soko la kimataifa kwa ajili ya kugharamia nakisi ya Bajeti.

#### **4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

##### **4.1  Utekelezaji wa Sheria ya Bajeti;**

**KWA KUWA** Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 imeanza kutumika na kuonesha mwanga katika usimamizi wa utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;

**NA KWA KUWA** Utaratibu mzuri unaohusu uwasilishwaji wa taarifa mbalimbali zinazohusu utekelezaji wa bajeti umeanishwa kwenye Sheria hiyo na Kanuni zake ambapo Wizara, Taasisi na Mashirika zinapaswa kuufuata;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali pamoja na taasisi zake kuhakikisha inatekeleza kikamilifu masharti na Kanuni za Sheria ya Bajeti ya Mwaka 2015 ikiwa ni pamoja na Serikali kuhakikisha inawasilisha kwa wakati Bungeni taarifa

zote zilizoainishwa kwenye sheria hiyo hususani taarifa za utekelezaji wa bajeti kwa kila robo mwaka.

#### 4.2 **Utekelezaji wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016;**

**KWA KUWA**, utaratibu wa ukusanyaji wa mapato ya Serikali hupitishwa na Bunge lako kupitia sheria ya Fedha inayotungwa kila mwaka wa fedha;

**NA KWA KUWA**, katika mwaka wa fedha 2016/17 Sheria ya Fedha iliyotungwa iliruhusu Serikali kuanza ukusanyaji wa mapato mbalimbali ambayo yamelenga kuwezesha kupatikana kwa matumizi ya Serikali;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha inatekeleza Sheria ya Fedha ya mwaka 2016 kama ilivyopitishwa na Bunge hasa katika maeneo yafuatayo:-

- a) Sharti la kisheria kwa kampuni za mawasiliano kujisajili katika soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) na kuhakikisha watanzania wanamiliki asilimia isiyopungua 25 ya mtaji wa kampuni zinazomiliki leseni za kujenga miundombinu ya mawasiliano (network facilities) na kutoa huduma za mawasiliano (network services/application services); na vilevile kuhakikisha watanzania wanamiliki asilimia isiyopungua 51 ya mtaji wa kampuni zinazomiliki leseni ya huduma ya utangazaji (content services licensee);
- b) Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kuhakikisha inakamilisha haraka iwezekanavyo mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri ili kuweza kuongeza ukusanyaji wa mapato husika mathalani kodi ya majengo na kodi ya pango;
- c) Ukopaji wa mikopo ya ndani usizidi kiwango kilichoidhinishwa na Bunge na uzingatie hali uchumi na ukwasi wa mabenki katika vipindi husika;

#### 4.3 **Usimamizi wa Deni la Taifa**

**KWA KUWA** Deni la Taifa ni malipo ya awali na lazima ambayo Serikali inapaswa kuyalipa kupitia mapato ya kila mwezi,

**NA KWA KUWA** pamoja na Serikali kubainisha kuwa deni hilo ni himilivu bado limeonesha kutumia fedha nyingi za makusanyo ya Serikali ya kila mwezi;

**KWA HIYO BASI;** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha ukopaji na ulipaji wa Deni hilo hauathiri ugharamiaji wa bajeti ya Serikali. Pia, Serikali ihakikishe inakamilisha zoezi la tathmini ya uwezo wa nchi kukopa na kulipa madeni (*Sovereign Credit Rating*)

#### **4.4 Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo**

**KWA KUWA,** Mpango wa maendeleo wa taifa umeainisha vipaumbele mbalimbali ambavyo Serikali imelenga kutekeleza katika kipindi cha Miaka mitano;

**NA KWAKUWA,** Miongoni mwa vipaumble hivyo ni kukuza uchumi wa viwanda, uendelezaji wa miundo mbinu, maji elimu na afya;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inapeleka kwa wakati fedha za kugharamia miradi ya maendeleo; kufuatilia na kusimamia tathmini ya utekelezaji wa mipango husika; inatumia ipasavyo fursa za kiuchumi za ustawi; inawekeza ipasavyo katika nishati ya umeme; inashirikisha kikamilifu sekta binafsi na kuendelea kuandaa na kuboresha rasilimali watu wenye ujuzi na elimu ya kutosha.

#### **4.5 Urasimishaji wa Sekta isiyo rasmi**

**KWA KUWA,** Sekta isiyo rasmi ni miongoni mwa maeneo ambayo kwa muda mrefu yameisababishia Serikali kuptokuwa na takwimu sahihi za walipa kodi;

**NA KWA KUWA,** ukosekanaji wa takwimu hizo umesabibishiwa Serikali kupoteza mapato mengi na hivyo kuifanya Serikali kutokukusanya mapato yale ipasavyo;

**KWA HIYO BASI,** Kamati inaendelea kuisitizia Serikali kuhakikisha inaongeza juhudi katika zoezi la urasimishaji wa biashara na shughuli ndogondogo za kiuchumi ili kuongeza wigo wa upatikanaji wa mapato na kudhibiti upotetu wa mapato. Sambamba na hili, Serikali ikamilishe haraka mfumo wa kuwatambua walipa Kodi kwa kutumia TIN na vitambulisho vya kitaifa (National IDs.); kuboresha utataratibu wa kuwasilisha ritani kwa sekta isiyo rasmi pamoja na kuimarisha utawala na usimamizi wa kodi kwa kuwatambua walipa kodi kwenye vitalu (Block Management System).

#### **4.6 Ukuaji wa sekta ya kilimo**

**KWA KUWA,** Sekta ya Kilimo inachangia ajira takriban asilimia 70 ya Watanzania na kwa mwaka 2015 ukuaji wa sekta hiyo ni asilimia 3.0;

**NA KWA KUWA**, sekta hiyo kwa kiasi inategemewa kusaidia kufanikisha juhudzi za kupunguza umaskini hasa vijiji na kuchochea mapinduzi ya viwanda;

**KWA HIYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuanza kutekeleza mikakati madhubuti ya kuinua sekta hii kwa kuboresha kilimo cha umwagiliaji; kuboresha teknolojia ya kilimo; kuweka masoko ya uhakika ya mazao ndani na nje ya nchi; kuwezesha uanzishaji wa viwanda vingi vya usindikaji wa mazao ya kilimo (agro-processing industry) na kusambaza maafisa ugani wa kutosha katika maeneo yote nchini.

#### **4.7 Hoja za Kamati za Bunge za kisekta zenyenye maslahi ya kitaifa**

**KWA KUWA**, Bunge kupitia Kanuni ya 98 na 101 ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 imeweka utaratibu utakaowezesha Serikali kufanya majadiliano kuhusu Hoja mahsusizi zinazojitokeza kwenye Kamati za Bunge za kisekta wakati wa kuchambua Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha uliopo na unaofuata;

**NA KWA KUWA**, Kupitia mashauriano hayo masuala mbalimbali ya kibajeti huweza kupatiwa ufumbuzi kabla ya kupitishwa kwa bajeti ya Serikali itakayo tekelezwa katika mwaka wa fedha unaofuata;

**HIVYO BASI**, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inatoa ushirikiano wa kutosha kwa Bunge wakati wa kujadili, kushughulikia na kutekeleza hoja za Kamati za Bunge za Kisekta zenyenye maslahi ya kitaifa ili kuleta tija ya zoezi zima la kutathmini utekelezaji wa bajeti za Wizara na taasisi zake kwa mwaka wa fedha uliopita na kuchambua makadirio ya bajeti za Wizara na taasisi husika kwa mwaka wa fedha unaofuata.

#### **4.8 Utekelezaji wa mapendekezo ya Bunge ya kuongeza vyanzo vipyaa vya mapato**

**KWA KUWA**, Bunge kupitia Kamati ya Chenge iliyoundwa kwa ajili ya kupendekeza vyanzo vya Mapato ilipendekeza vyanzo mbalimbali vya mapato kwa Serikali;

**NA KWA KUWA**, ripoti hiyo iliwasilishwa Serikalini kwa jaili ya hatua za utekelezaji ambao imeonekana baadhi ya vyanzo havijafanyiwa kazi,

**KWA HISYO BASI**, Kamati inaendelea kuisisitizia Serikali kukamilisha masuala yafuatayo:-

- a) Kukamilisha utafiti na tathmini ya ukusanyaji wa mapato kupitia bahari kuu;
- b) Kukamilisha Kanuni za Sheria za kusimamia mapato ya mafuta na gesi asilia ya Mwaka 2015 na Sheria ya Uwazi na Uwajibikaji katika rasilimali za madini, mafuta na gesi asilia Tanzania ya mwaka 2015;
- c) Kulipa deni la TANESCO ambalo hadi mwezi Agosti 2016 lilifikia takribani shilingi bilioni 794.9;
- d) Kukamilisha miradi mbalimbali ya nishati ya umeme ikiwemo Kinyerezi II na miradi miradi mingine ya nishati mbadala inayoendeshwa kwa nguvu ya maji (hydro), jotoardhi (geothermal), upepo (wind power) na umeme wa juu (solar power).

#### **4.9 Mafunzo ya Kamati ya Bajeti**

**KWA KUWA,** Kamati ya Bajeti inaundwa na wajumbe wengi walio wapya;

**NA KWA KUWA,** Wajumbe hao wanahitaji kupatiwa mafunzo yatakaowajengea uwezo kwenye masuala ya uchambuzi wa bajeti na uchumi kwa ujumla,

**KWAHIYO BASI,** Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kupata mafunzo ya mara kwa mara hasa ya nje ili yaweze kuwajengea uwezo na ujuzi wajumbe pamoja na sekretarieti ya Kamati ambao utaiwezesha Kamati ya Bajeti kuisimamia ipasavyo Sheria ya Bajeti na Sheria zingine za fedha na kuisaidia Serikali katika kutatua changamoto za upatikanaji wa mapato ya kutosha kuweza kugharamia bajeti yake.

#### **5.0. HITIMISHO**

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kukushuruku kwa mara nyingine kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Napenda nimshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isidori Mpango (Mb), Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijiji (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano walizoutoa kwa Kamati. Nawashukuru pia wataalamu wote kutoka Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi mbalimbali za Fedha ambao wamefanya kazi na Kamati hii katika kipindi hiki. Aidha, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru wadau mbalimbali wa masuala ya biashara na kodi ambao wameshirikiana na Kamati hii katika hatua mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Wajumbe Waalikwa kwa umakini wao katika kujadili na kutoa mapendekezo

mbalimbali kwa Serikali kuitia taarifa ambazo Kamati ya Bajeti iliwasilisha Bungeni. Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Hawa Abdulrahman Ghasia, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb – M/Mwenyekiti
3. Mhe. Hamida Mohamedi Abdallah, Mb
4. Mhe. Jerome Bwanausi, Mb
5. Mhe. Mbaraka Kitwana Dau, Mb
6. Mhe. Mendrad Lutengano Kigola, Mb
7. Mhe. Maria Ndilla Kangoye, Mb
8. Mhe. Susan Peter Maselle, Mb
9. Mhe. Agustino Manyanda Masele, Mb
10. Mhe. Janet Zebedayo Mbene, Mb
11. Mhe. Freeman Aikael Mbowe, Mb
12. Mhe. Flatei Gregory Massay, Mb
13. Mhe. Makame Kassim Makame, Mb
14. Mhe. Cecil David Mwambe, Mb
15. Mhe. Susana Chogidaso Mgonukulima, Mb
16. Mhe. Subira Khamis Mgusu, Mb
17. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
18. Mhe. Ali Hassan Omari, Mb
19. Mhe. Martha Jachi Umbulla, Mb
20. Mhe. David Ernest Silinde, Mb
21. Mhe. Jitu Vrajlal Soni, Mb
22. Mhe. Andrew John Chenge, Mb
23. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
24. Mhe. Dalaly Peter Kafumu, Mb
25. Mhe. Japhet Ngalilonga Hasunga, Mb
26. Mhe. Albert Obama Ntabaliba, Mb
27. Mhe. Mussa A. Zungu, Mb

**Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru pia Katibu wa Bunge Dr. Thomas Kashililah na watumishi wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake vizuri. Aidha, napenda kuishukuru Sekretarieti ya Kamati kwa kuihudumia vema Kamati hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja na naomba kuwasilisha.

Hawa A. Ghasia, Mb

**MWENYEKITI**  
**KAMATI YA BUNGE YA BAJETI**  
04 Februari, 2017

**MWENYEKITI:** Hoja imeungwa mkono. Ahsante sana Mheshimiwa Kandege. Hoja hiyo tutaiamua baadae. Waheshimiwa Wabunge, lakini kabla hatujaendelea ngoja nitoe matangazo tu.

Waheshimiwa Wabunge ninaambiwa tuna wageni waliopo na sisi asubuhi hii lakini haikuainishwa kwa maana ya makundi. Niliseme hili la jumla kwamba tunao wageni wa Waheshimiwa Wabunge pamoja na wageni waliokuja kutembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo Bungeni. Wote mliopo hapa, wageni wa Wabunge na wale mliokuja kwenye mafunzo karibuni sana. (makofi)

Tunaendelea, sasa Waheshimiwa Wabunge hoja hii tunapaswa tuikamilishe leo ikiwezekana kabla ya saa nane, lakini mjadala tutauruhusu uendelee mpaka saa saba na nusu, si lazima lakini kwa hoja nzito kama hii ambayo ndiyo inayobeba sura ya utekelezaji wa shughuli za Serikali mimi nadhani ingelipendeza kama tutaifanyia haki. Kwa hiyo, nina orodha ya wachangiaji hapa, sidhani kama nafungwa moja kwa moja na hii niliyonayo hapa, lakini kwa kuanzia kwa sababu sijapata orodha kwa upande wa kwangu wa kulia nategemea kwamba labda wanataka kufanya ile kwa kiingereza tunaita *a free for all* kwamba kila mmoja anaweza akachangia anavyoona. Sasa mimi nitaanza na Mheshimiwa Cecil Mwambe.

**MHE. CECIL D. MWAMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia kwenye hoja iliyoko mbele yetu taarifa ya Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi kuanzia mwezi Januari, 2016 mpaka Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza mimi ni Mjumbe wa Kamati hiyo ya Bajeti na kwa kipindi hiki chote tulikuwa tukifanya kazi pamoja kuhakikisha bajeti yetu inakwenda vizuri hasa zaidi katika jukumu letu la kutaka kuisimamia Serikali katika utekelezaji wa majukumu yake. Kwanza kabisa Kamati yetu imekutana na changamoto nyingi sana; na Mheshimiwa Mwenyekiti wakati anawasilisha taarifa yake tumeona na karibu Kamati zote zilizokuwa zinatoa hapa taarifa zake wamekuwa wakilalamikia kuhusu jambo hili, kukosekana kwa mafunzo kwa visingizio kwamba hatuna bajeti ya kutosha kwenye kufanya shughuli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali ya kushangaza kabisa, Kamati ya Bajeti kama ulivyosema ndio kubwa hasa na inayosimamia mustakabali mzima

wa nchi yetu hasa zaidi kwenye mapato na matumizi, lakini tunakosa mafunzo ya kutosha, Ofisi ya Katibu, pia Ofisi ya Spika haijaipa Kamati hii kipaumbele kuhakikisha kwamba tunajua majukumu yetu ya msingi, kwa kuwa exposed kwenye maeneo mbalimbali na ukizingatia tulio wengi kule ndani ni wageni ambao tunahitaji hasa na sisi siyo wataalam wa mahesabu katika hali kubwa. Kwa hiyo, Bunge hili lione sasa kuna haja ya lazima kabisa ya kuhakikisha Wajumbe wa hii Kamati wanapata mafunzo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, tuna changamoto kubwa sana kutoka kwenye Wizara mbalimbali hata Wizara ya Fedha yenyewe, kumekuwa na usiri mkubwa sana wa kupatiwa hizi taarifa. Utakuta tunakwenda kwenye vikao, tumebakisha muda mchache kuanza vikao vyetu ndipo taarifa zinapokuja ambazo wanataka sisi tuweze kuchangia na kutoa mapendelekezo kwa Serikali. Kwa hiyo, tuombe tuwe tunapata taarifa kwa wakati ili tuweze na sisi kuzipitia vizuri tuweze kutoa mapendelekezo yetu kwa Serikali. Kama unavyofahamu jukumu letu ni pamoja na kusimamia suala zima la Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa inajadiliwa kwamba kuna ukuaji mkubwa sana wa Deni la Taifa. Siyo siri kwamba Deni la Taifa linakuwa na hasa zaidi deni la ndani limekuwa likikuwa kila mara, hii inadhoofisha sana sekta binafsi kwenye kupata mikopo. Kwa sababu Serikali nayo sasa imekuwa ikishindana na wafanyabiashara wadogo wadogo, Serikali imekuwa ikishindana na wamachinga na watu wengine kuweza kupata mikopo katika mabenki yetu ya kibiashara. Kwa sababu Serikali wana nguvu kubwa sana, wao ndiyo hasa wanaopendelewa na inaonekana hili jambo linafanywa kama maagizo maalum kwamba Serikali ipewe kipaumbele cha kukopeshwa.

Hivyo, tunazuia mzunguko wa pesa wa kawaida kabisa hapa ndani kwetu na ndiyo maana sasa tunaanza kuona *inflation* zinapanda. Wafanyabishara wanashindwa kulipa madeni yao, kwa sababu sasa hivi hawakopeshwi tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunaona wanafilisiwa kama tulivyosikia kuna wafanyabiashara wazabuni wa Serikali, kuna Wazabuni ambao walikuwa wamekopa na wanafanya shughuli na majeshi, tunaona watu hawa wanashindwa kulipa madeni yao kimsingi na hawawezi kukopesheka tena. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeacha jukumu lake, Serikali ni jambo kubwa sana, ilitakiwa itoe mikopo yao nje ya nchi kuja kuleta Tanzania, kuja kuongeza mzunguko wa pesa katika nchi yetu na katika mzunguko wetu wa

kawaida kabisa wa pesa. Sasa hivi tumeona nao kwa sababu ya kutokutekeleza majukumu yao ya msingi, kutokufuata masuala ya utawala bora na sheria wameamua nao wawe wanakopa hapa ndani, kiasi kwamba wanazuia mzunguko wa pesa, na kufanya pesa iwe na mzunguko mdogo (*circulation of money*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunaona wanakwenda kukopa au kuchukua pesa kwenye mifuko, kiasi kwamba wastaafu wanashindwa kulipwa pesa zao kwa wakati. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamekuwa wakizungushwa, tunafahamu hapa katikati kuna ma- DAS, kuna ma-DED ambao kabisa ni Watumishi wa Serikali wanashindwa kupata pension zao. Mifuko ya PPF, NSSF tumeanza kuona sasa wanashindwa kuwalipa watumishi kwa sababu tu pesa nyingi zimechukuliwa tena na Serikali, Serikali inashindwa kuzirudisha pesa zile kwenye mzunguko, matokeo yake wanakwenda kugharamia vitu ambavyo viko nje ya bajeti. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi pesa hazitoki mfukoni kwa mtu mmoja, hazitoki mfukoni kwa Mheshimiwa Rais, hizi pesa ni zile ambazo sisi tunazikusanya, badala ya kwenda kufanya majukumu tuliyoyapangia kibajeti, zinakwenda kufanya kadri ya mahitaji ya Mheshimiwa Rais, na kwenda kufanya kadri ya mahitaji wa viongozi mbalimbali. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuziachie pesa zizunguke, watu waliostaafu wapewe sasa haki yao, kwa sababu tunajua baada ya kustaafu watu wana muda mfupi tu wa kuweza kuishi hapa duniani, basi wapewe pesa zao kwa wakati wazitumie wanavyotaka wao, badala ya kwenda kugharamia miradi ambayo siyo ya kibajeti. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pia kuna madeni ya majeshi, watumishi wa jeshi tuliondoa hapa masuala ya kodi kwenye vifaa mbalimbali wanavyotumia kwenye maduka ya majeshi, lakini wakasema pesa hizo wataongezewa kwenye masurufu yao, pesa hizo wataongezewa kwenye mishahara yao. Sina uhakika mpaka kufikia leo ni shilingi ngapi zimepelekwa kwenye majeshi kwa ajili ya ku-subsidize ile kodi ambayo ilikuwepo walikuwa wanalipiwa mwanzo na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati Mwenyekiti wa Kamati anatoa taarifa hapa na wote tunafahamu kwamba Serikali iliamua kujikita kutoa asilimia 40 yote iende kwenye shughuli za maendeleo, lakini hapa tumesikia katika ripoti na

hii kila mtu anaifahamu, hakuna *reflection* hauwezi kuona hali halisi ya kilichofanyika sasa hivi. Hakuna tofauti wakati huo asilimia 40 ya maendeleo iliyopo sasa hivi na asilimia zile ndogo ambazo zilikuwepo siku za nyuma. Pesa za maendeleo hazifiki kwa wakati kwenye maeneo yanakotakiwa kwenda. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashindwa kuelewa tunajitangazia kwamba tunakusanya pesa nyingi sana kwa ajili ya shughuli za maendeleo, nchi yetu iweze kufanikiwa kuvunja hapa rekodi, ukiangalia hapa kwenye baadhi ya kurasa inaonyesha kabisa wazi kwamba zimekusanya pesa nyingi sana, lakini kimsingi pesa hizi haziendi *ku-reflect* maisha halisi ya wananchi wanayoyaishi mitaani. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaanza kuhisi kwamba hata *inflation* inapanda mzunguko wa pesa umekuwa mdogo. Serikali inasema inapeleka pesa za maendeleo, maendeleo hayo kwa sasa hivi kwa kweli hatuyaoni. Halmashauri zimekuwa zikilia njaa, hakuna mtu anayeweza kutekeleza wajibu wake, miradi mingi imesimama, pesa nyingi ndiyo tunatambua inakwenda kulipa madeni mbalimbali lakini kimsingi mzunguko wa pesa umeondoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye ukurasa wa 43 wa hii taarifa tuliyonayo hapa, mpaka leo Serikali bado inang'ang'ana na vyanzo vilevile vyatya mapato vyatya asili wakati ilifanyika tafiti na Mheshimiwa Chenge wewe ndiye ulikuwa Mwenyekiti wa tafiti hizo, ukapendekeza vyanzo vipyatya mapato Serikalini, lakini Serikali hii tunayoiiita sikivu mpaka sasa hivi bado imeshindwa kutumia vyanzo vipyatya mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunategemea tuendeshe nchi yetu kwa kulipia kodi au kuongeza kodi za sigara kila mara, si ajabu utakuja kuona bajeti ijayo sigara inapandishwa tena bei, soda, bia zinakwenda kupandishwa bei na vinywaji vingine lakini huu siyo msingi wa kweli, kama nchi inataka kusimama, kama nchi kweli inataka kuendelea tutegemee vyanzo hivi kila mara. Kulikuwa kuna mapendeleko mazuri kabisa ya vyanzo vipyatya mapato, lakini Serikali imeendelea kudharau.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulifikiri sasa Serikali hii itaamua kuchukua vile vyanzo na kuamua kuvifanyia kazi, lakini tunaona hapa Kamati inaleta taarifa yao. Tunatakiwa sasa kukamilisha tathmini ya ukusanyaji wa mapato kuitia Bahari Kuu, hiki chanzo ni kizuri sana cha mapato lakini hakijaanza kutumika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunafahamu kabisa tunatakiwa tuanze sasa hivi kuongeza vyanzo vypa vya mapato. Tuseme kwamba Shirika la Umeme halizalishi vizuri umeme wake, kwa hiyo tuende tuanze kuipa nguvu zile sehemu mbalimbali ambazo zinataka kuzalisha umeme. Kwa mfano, watu geothermal, kuna umeme wa upepo, kuna watu wanataka kutumia hizi solar energies, tuanze kuona sasa hivi viwe vyanzo vingine vya kuweza kuongezea Serikali mapato na TANESCO iende kulipa deni lake sasa ili kimsingi watu uzalishaji uongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona tatizo kubwa sana la umeme hapa Mkao wa Mtwara sasa hivi linatoka na hili jambo linatoka ni kwa sababu ya kung'ang'ania chanzo kimoja cha umeme. Wilaya nzima au Mkao zima wa Mtwara kuna tatizo kubwa sana la umeme tuwaongezee wale watu nguvu ili waweze kuzalisha sasa na waweze kuchangia vizuri kwenye pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa sana niseme tu kwamba pamoja na Kamati kuleta taarifa zake hapa mbele, lakini siyo kila mara Kamati hii haionekani kuwa ni kipaumbele, wakati ina jukumu kubwa la kusimamia mchakato mzima wa bajeti toka mwanzo wake mpaka pale tutakapomalizia. Kwa hiyo, kifupi niseme tunaomba tafdhali kwamba sasa hivi mependekezo yale yaliyotolewa na Kamati ya Chenge, vyanzo mbalimbali vya mapato vianze kuwa adopted. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona hapa karibuni kuna utaratibu umeanza wa kukata pesa kwenye miamala, hili jambo linaumiza sana Watanzania, hili jambo linaumiza wananchi wote tulifkirie tena upya ili kuwe kuna thamani halisi ya matumizi ya zile pesa shilingi 1,000 basi ipate thamani yake, shilingi 500 basi ipate thamani yake. Lakini tunakwenda kwenye miamala ya kibenki tuona gharama zimeongezeka, tunakwenda kwenye miamala ya simu, tunaona kule gharama zimeongezeka, hivi vitu vyote havileti picha nzuri kwa wananchi. Kwa hiyo, tufikirie vyanzo vingine vya mapato, kwa sababu vyanzo vya kawaida hivi vya kodi vimeshindwa kabisa na vimeduwa kama ni traditional sources of income to the government. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaona sasa hivi mpaka polisi tunaanza kuwaingiza na wenyewe ili waanze nao kuwa ni source of income ya Serikali, hili jambo siyo jema tufikirie vyanzo vile ambavyo Mheshimiwa Chenge wewe kwa nafasi yako ulishauri kabisa Serikali. Kama walikuwa hawana haja ya kutaka kulisikia kusingkuwa na haja ya kutumia pesa nyingi kuipa ile Kamati iliyoanza kufikiri kuhusu hivi vyanzo. Asante kwa kunipa nafasi.(Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante! Ninakushukuru sana Mheshimiwa Mwambe. Tunaendelea Mheshimiwa Juma Hamad Omar, atafuatiwa na Mheshimiwa Stanslaus Nyongo ajiandae.

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka kuchukua nafasi hii kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuchangia taarifa hii muhimu, taarifa ya Kamati ya Bajeti, katika kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti, nadhani Mheshimiwa Mwambe amezungumza mengi sana na taarifa yenyewe ina mambo mengi sana na muhimu, sasa mimi nitachukua nafasi hii kukazia tu baadhi ya sehemu ambazo nadhani zina umuhimu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yoyote duniani inapata sifa sana ya maendeleo ya kiuchumi ikiwa itakuwa na mambo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwanza nchi hiyo inatakiwa iwe na sera sahihi ya uchumi (*Prudent Economic Policy*); pili, nchi hiyo iwe na sera sahihi ya utozaji kodi (*Taxation Policy*); tatu, iwe na sera sahihi ya fedha (*Prudent Fiscal and Monetary Policy*). Sasa mambo hayo matatu yapo katika kapu ambalo linaitwa *good governance and political stability*. Maana hata hayo mambo matatu kama unayo, lakini kama huna *good governance* na *political stability* basi huwezi kuendelea kiuchumi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani mtakubaliana na mimi kwamba ziko nchi nyngi sana duniani, ambazo zimepiga sana hatua za kiuchumi. Kwa mfano, tuchukulie nchi za mashariki ya mbali (*far east*) nchi zile zimepiga sana hatua. Tukichukua kwa mfano utawala wa Mahathir Mohamad katika nchi ya Malaysia; Mahathir Mohamad alikuwa ni *Fourth Prime Minister* wa Malaysia, na nina hakika mtakubaliana na mimi kwamba kama kuna mtu alihuisha uchumi wa Malaysia au kama kuna mtu alijengwa uchumi wa Malaysia wa kuja na *prudent economic policies, prudent of fiscal and monetary policy, prudent taxation policy* basi alikuwa ni Mahathir Mohamad. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Malaysia ya leo ni nchi moja ambayo imepiga a very big economic strive, hivyo nchi nyngine za mbali ya Mashariki. Tuje hapa kwetu Afrika, Botswana ni nchi ambayo ina-enjoy the highest per capital development. Nchi ile haina resource nyngi kuliko Tanzania, nadhani kama sikosei resources zao zaidi wanazotegemea ni madini kidogo na mifugo, lakini

leo Botswana ina *the highest per capital income*, lakini kwa nini? Botswana imefikia pale kwa sababu ya *good governance and stability*. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani hata ukichukua ile award ambayo ametoa Mo Ibrahim award ile imetolewa kwa Marais wastaafu ambao wamekuwa na a very good governance and good political stability. Rais wa Botswana mwaka 2008, Mheshimiwa Festus Mogae alipata zawadi ile ya dola 5000. Rais Kikwete amestaafu juzi nadhani atapata, lakini sasa kama hii imemaliza 2016 hajapata unaanza kujiuliza ni kwa nini? Kwa hiyo, good governance ni kitu muhimu sana katika yote haya. Botswana ukichukua kigezo cha uchumi cha *foreign exchange value*, Botswana ina *foreign exchange* ya kutosha kwa miezi 12. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Nigeria pamoja na kwamba ni old producing country lakini ana *foreign exchange* ya kutosha kwa miezi kumi kwa sababu kule ndani kumekuwa na political terms, tukija kwetu Tanzania tuna *foreign exchange* ya kutosha kwa miezi minne, tukija Zimbabwe rafiki yetu ambaye tunampenda sana na tunashirikiana naye sana because of lack of good governance ana *foreign exchange* siku saba *this is amazing!* Kwa hiyo, yote mifano inamaanisha kwamba haya mambo matatu, lazima yawe katika kapu la good governance, without good governance you can not make strong economic strives. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuje kwenye Pato la Taifa na tunaambwa linaongezeka, mwaka 2016/2017 Pato la Taifa tulitegemea kwamba litakuwa asilimia saba lakini tukienda mwaka 2017/2018 itakuwa asilimia 7.2. Swali la kujiuliza *infact* katika hii region yetu sisi ndiyo tunaongoza kwa Pato la Taifa wanafuatia Rwanda, wanafuatia Kenya. Rwanda katika mwaka 2015 walikuwa na Pato la Taifa la asilimia 6.9; mwaka 2016 matarajio ni kwamba watakuwa na asilimia sita. Kenya ni ya tatu lakini nchi nyingine hizi kama Burundi, Uganda, Zambia, Malawi, Congo DRC zote tunazipita sana.

Kwa hiyo, *the first economy in our region* ni Tanzania, ni asilimia Saba lakini tunategemea kupata asilimia 7.2. Swali la kujiuliza kama Pato la Taifa linaongezeka kiasi hicho hivi kwa nini hali za wananchi wetu zimekuwa duni? (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nasema nikingalia tu, ni kwa sababu sekta inayo-employ watu wengi katika Tanzania ni sekta ya kilimo; na Government yetu haijafanya a big investment katika sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo inachangia only 2.1 percent ya Pato la Taifa, sekta ya mawasiliano nadhani

kama sikosei inachangia asilimia 15.5, sekta ya uchimbaji madini ndiyo kubwa inachangia asilimi 15.8, lakini sekta ya uchimbaji madini inaaajiri watu wa nje. Sekta ya mawasiliano na uchukuzi sawa lakini haina *direct impact* na mkulima, lakini kwa sababu Serikali haija-mark *very big investment over areas* katika sekta ya kilimo ndiyo ukakuta leo sekta ya kilimo ambayo imaaajiri watu wengi, inachangia *only 2.1 percent*. Hapa inaonesha kwamba hatuna a *prudent economic policies* kupanga ni kuchagua. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija hapo hapo kwenye Pato la Taifa, mimi nakubali *fine Tanzania is a fast growing economics in terms of GDP*, lakini *that is a nominal terms*. *In real terms* tunakwenda chini; wakati tunazungumza Pato la Taifa linaongezeka lakini pato la kila Mtanzania linapungua *in real term*. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2014 kwa mfano pato la Mtanzania kwa wastani alikuwa anapata dola 1,047, lakini mwaka 2015 imeshuka anapata dola 966.

**MBUNGE FULANI:** Mhh!

**MHE. JUMA HAMAD OMAR:** Ndiyo! Hii ni kwa sababu sekta ya kilimo ambayo kwa kweli ilikuwa tuweke *priority* na ambayo inaaajiri watu wengi *but government has done nothing when it comes to investment*.

Sasa kama hatuja-invest kwenye sekta ya kilimo ambayo inaaajiri watu wengi nakuhakikishieni *in real term fine*, wataalam wanatuambia Pato la Taifa linaongezeka but in *nominal terms* pato haliongezeki. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye mapato (*taxation policy*); hakuna Serikali yeyote duniani ambayo inaongozwa.... (Makofii)

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea! Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, atafuatiwa na Mheshimiwa Hasna Mwilima.

**MHE. STANSLAUS H. NYONGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi kuchangia katika taarifa hii ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa shughuli zake katika kipindi cha kuanzia mwezi wa Januari, 2016 hadi Januari, 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kupongeza Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya, tunawapongeza kwa ufuatiliaji mzuri na ukweli waliouzungumza katika ripoti yao. Na mimi nashukuru kwamba Serikali imefanya kazi nzuri ya kukusanya mapato. Naishukuru vilevile Serikali na kuipongeza kwa kuweza kulipa madeni kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumza haya kwa sababu tumeona ripoti inaeleza wazi kabisa kwamba ulipaji wa madeni umelipwa kwa kiwango cha juu kabisa na hii ni dalili nzuri kwamba ulipaji huu wa madeni unaweza kutusaidia hata kwa wafadhili kuendelea kutuamini na kuweza kutupa pesa nyingi ili kuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa imeeleza vizuri japokuwa tu mimi nina wasiwasi kidogo kwa baadhi ya mambo ambayo nafikiri tungehitaji uangalizi wa ndani zaidi au wa macho makali zaidi mawili. Kwa maana ya kwamba tunapoandaa bajeti ni lazima tuzingatie mambo ambayo yanatokana na bajeti ile. Tunaona kabisa kwamba bajeti hii haikuweza kutekelezwa kwenye baadhi ya miradi ya maendeleo kwa sababu nchi ilikwenda kulipa madeni. Tunakubali kulipa madeni ni wajibu, lakini tuna wajibu wa kuangalia bajeti zetu tunavyozipanga ni lazima wataalam watusaidie ku-forecast yale madeni ambayo Serikali inatakiwa iyalipe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitoka kwenye bajeti ya trilioni 22 tukaenda kwenye bajeti ya trilioni 29 kwa mwaka 2016/2017. Tulikwenda kwenye bajeti kubwa, kinachonishangaza ni kwamba, kumbe kulikuwa kuna madeni ambayo yako *matured*. Kama kungekuwa kuna madeni yako *matured* ambayo yamekuwa ni kikwazo cha Serikali kupeleka pesa kwenye miradi na kulipa madeni ya ndani na ya nje, basi inabidi wataalam wachunguze na waangalie wawe tayari kuisaidia Serikali, kutusaidia Wabunge tunapokwenda kupitisha bajeti basi tuweze ku-consider yale madeni ambayo Serikali inakwenda kuyalipa. Bila kufanya hivyo tutapanga bajeti, tutakutana na madeni katikati, tutalipa madeni, tutashindwa kupeleka pesa kwenye miradi ya maendeleo. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukitizama katika miradi ya maendeleo Serikali imepeleka fedha kwenye miradi ya maendeleo kidogo sana. Mfano mzuri ukiangalia kwenye kipaumbele cha Serikali ambayo tunasema Serikali ya viwanda, bajeti iliyopelekwa katika Wizara ya Biashara na Viwanda ni asilimia 10 tu ya bajeti iliyokusudiwa. Ukitizama kwenye Wizara inayohusiana na masuala ya mazingira chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais, pesa ya maendeleo ni asilimia sifuri, haijaenda pesa yoyote. Sasa hivi ni vikwazo vinatukwamisha, inabidi kweli

Serikali tujizatiti tuhakikishe tunapeleka pesa za maendeleo kwa wakati kama ilivyopangwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuongelea vilevile masuala ya vyanzo vya mapato. Suala la kodi, kuna kodi hapa ambazo zililalamikiwa sana, mfano kodi ya VAT kwenye utalii. Mimi nafikiri Serikali ijipime, Wabunge tunapozungumza na yenyewe Serikali itusikilize, siyo kukaa mnasikiliza tunaandika halafu tunakwenda kutoza kodi kwenye utalii. Utaendaje kuwatoza watu kwenda kuangalia nyumbu na swala unawawekea VAT! Mtu anayekwenda kuangalia nyumbu na swala hakuna haja ya kumuwekea VAT. Tuondoe VAT tuweze ku-invites watalii wengi waweze kutembelea katika nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeona pato linavyozidi kuongezeka kwenye utalii tukiwaondolea kodi ya VAT tutakaribisha watalii wengi, *wata-flow* kwa wingi. Tuangalie na nchi ambazo tunashindana nazo kama Kenya wao wanafanya nini? Tujifunze kutoka kule ili na sisi tuweze kufanya inavyostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kodi hiyo kuna suala la VAT kwenye *capital investment*. Tunasisitiza watu tuondoe kodi kwenye kilimo, tunasisitiza tuondoe kodi kwenye vifaa vya kilimo kwa maana ya kwamba watu tulime zaidi tupate mazao mengi. Kwa mfano, mtu amelima akaenda kuuza mazao yale kwa wale watu ambao wanachakata mazao yetu, unakuta kwa mfano mtambo wa kutengeneza juice au mtambo wa kusaga unga, ile *investment* anayoileta Mwekezaji, kwa mfano, Ndugu Bakhresa pale alitaka kuleta mtambo wa dola milioni 100, lakini akauktana na VAT! Hebu piga asilimia 18 ya VAT ya milioni 100 ni shilingi ngapi! Ndipo alipoamua kuondoa mtambo huu na kuupeleka nchi jirani ambako hawana hiyo kodi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ni lazima tu-harmonize hizi *strategy* zetu. Kama tumeamua kuondoa VAT kwenye vifaa vya kilimo basi tuondoe kodi kwenye msururu mzima ambao hadi kwenye uchakataji wa bidhaa zile. Sasa kama wewe umeondoa kodi umemu-encourage mtu alime akalima mahindi, unamuwekea kodi mtu anaye-invest anayeweza kwenda kusaga unga na kupack, maana yake ni nini? Tunapoamua kuondoa basi tuangalie *flow* nzima ili tuweze ku-encourage wawekezaji waweze ku-produce zaidi na kuweza kupata kipato cha kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kodi hiyo kuna kitu kinaitwa *single customer territory*, mikataba ya *single custom*, tume pigia kelele. Ni kweli Tanzania sisi ni wanachama wa East African na tumekubaliana nchi zote za East

Africa kuwa na *single customer territory* kwa maana ya kutoza kodi, kwa niaba ya nchi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, huu mkataba uko kwa nchi za East Africa, kwa nchi ya Kongo haupo, ilna maana Mkenya anaweza akafanya biashara na Mkongo bila kumtoza kodi. Ina maana sisi tunamtoza kodi mfanyakia biashara wa Kongo Dar es Salaam, tukimtoza kodi ina maana kwamba huyu mfanyakia biashara tunamu-encourage aende kwenye bandari za pembeni. Wamekwenda Beira, wamekwenda Durban, wanakwenda Mombasa, wametukwepa katika bandari yetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tuyatizame kwa kina, tunapoamua kutafuta vyanzo vya mapato tusione aibu. Tusiingie mikataba ambayo haina tija! Huu Mkataba wa *single customer territory* kati ya Tanzania na Kongo naomba muutizame upya, ikibidi muuondoe. Kwa nini tuwakusanyie Kongo zile pesa? Kuna malalamiko wameshaanza kusema kwamba, kumbe hata pesa zenyewe zinapokwenda kwenye mikono ya Serikali ya Kongo haifiki kwa wananchi! Sasa sisi tunawasaidia nini? Ina maana badala ya kuwasaidia Wakongo wote tunawasaidia Wakongo wachache!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini tuingie kwenye mkataba kama huo na unakimbiza wateja wetu wasije katika bandari yetu! Tuuondoe huo mkataba, ikiwezekana hata kesho tuuondoe ili kusudi tu-encourage biashara ya kongo na Tanzania ili bandari yetu irudishe uwezo wake. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naongelea kuhusu vyanzo vipyaa. Katika kuongelea vyanzo vipyaa vya kodi ni lazima tujali viwanda vyetu na viwanda vipo vikubwa na viwanda vidogo. Viwanda hivi haviwezi kufanya kazi kama hatuna umeme wa uhakika, hatuna umeme wenye bei nafuu. Umeme wetu bado ni tatizo kubwa katika uchumi wa nchi yetu. Tunauza umeme kwa bei kubwa mno na bado umeme wenye hauna quality nzuri, unakatika mara kwa mara. Umeme unapokatika ni hasara kubwa sana kwa wawekezaji. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulitembelea EPZA pale kuna jamaa wanatengeneza hizi *smart card*, kadi za benki na nini, wanatengeneza kwa ajili ya kuwauzia makampuni ya simu, wanauzia mabenki, hizi unaziona visa card zinatengenezwa pale EPZ Dar es Salaam. Wanatumia system kubwa ya computer and very sophisticated. Ukiukata umeme mara moja wana-recover ile system kwa siku saba. Kesho akiona kuna nchi nyingine ina umeme wenye quality nzuri huyu mtu atatuhamu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya ni matatizo makubwa. Ilipeni TANESCO deni lake, walipeni waweze kuweka *infrastructure* nzuri. Tunaipongeza Serikali mmepeleka umeme hadi vijiji sawa kabisa mmepeleka umeme hadi vijiji, lakini *quality* ya umeme bado ni tatizo katika nchi yetu. Umeme kwa kweli ni tatizo, tusipo-*improve* umeme hii Serikali tunasema tunaenda kwenye viwanda, tutashindwa kwa sababu bila energy ya kutosha ni tatizo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niende kwenye kilimo. Asilimia 70 ya Watanzania tumejajiri kwenye kilimo, lakini kilimo chetu hakina tija, kilimo na ufugaji ndiko kwenye ajira kubwa katika nchi yetu. Hebu tuangalie namna gani ya kuwasaidia wakulima, sasa hivi bei ya mbegu ya mahindi inauzwa shilingi 13,000 mfuko wa kilo mbili! Shilingi 13,000 mwananchi wa kawaida mbegu kununua shilingi 5,000 kwa kilo, karibu shilingi 6,000 ni shida kununua, hawezikununua. Ni bora Serikali mka-subsidize hizi mbegu mkatoa na mkawalipia wakulima wakanunua mbegu kwa bei nafuu ili waweze kupanda na kupata mazao mengi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachokifanya sisi kwetu kule Usukumani mtu akilima mwaka huu anahifadhi na madebe mawili/matafu ya mbegu, zile mbegu hazina ubora! Tunataka *special* mbegu ambazo mtu ukipanda unapata mavuno ya kutosha, sasa zile mbegu ni bei juu mno. Kama mnataka kweli wananchi waweze kulima wapate mazao ya kutosha punguzeni bei ya mbegu, Serikali iingilie kati i-intervene m-subsidize mzilipie kodi hizi mbegu. Wako watu wachache wanaozalisha hizi mbegu muwape mikataba wazalishé mbegu, muwasambazie wananchi kwa bei nafuu waweze kupata mazao mazuri. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kwa wanyama ng'ombe tulionao hatuna ng'ombe wa maziwa wala hatuna ng'ombe wa nyama. Tuna *indigenous* ng'ombe wetu ambao ukimwangalia amekondeana, tuna ng'ombe wengi na ukame huu wengi wanakufa sasa hivi. Hatuna ng'ombe ambao wana *good quality* kwa maana ya kula nyama, hatuna ng'ombe kwa maana ya kupata maziwa bora. Tunaomba mbegu mpya, tunazungumza kila siku Serikali iingilie kati mleta mbegu za ng'ombe wapya wenye kuweza kutoa nyama nyingi, ng'ombe wapya wenye kuweza kutoa maziwa mengi ya kutosha ndipo tutaweza kuwainua wananchi wetu na kuweza kuwaingiza katika uchumi wa kati. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba bado Serikali ina kazi kubwa ya kufanya. Nawashukuru kwa kazi kubwa mnayoifanya kwa kweli,

tumeangalia kwenye elimu, elimu bure, pesa zinakwenda, hivyo vitu tunasema tunatoa pongezi za dhati kabisa, muendelee kufanya kazi nzuri. Tunaona miradi mingine inakwenda ya barabara, tunajengewa barabara, lakini miradi ya maendeleo tunaomba Serikali iwalipe watu wanaoidai ili kusudi mzunguko wa pesa urudi na tuweze kupata mzunguko wa kutosha na watu waweze kulipa kodi na Serikali iweze kupata mapato ya kutosha. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Nyongo. Tunaendelea, Mheshimiwa Hasna Mwilima, atafuatiwa na Mheshimiwa Innocent Bashungwa.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi pia naomba niungane kuchangia kwenye hii kamati ya Bajeti. Kwanza nililokuwa nataka nichangie baada ya kupitia hii taarifa nimeona tumejikita sana kuzungumzia robo ya kwanza ya bajeti ya mwaka 2016/2017, lakini sote tunatambua kwamba pesa za maendeleo zimechelewa sana huko vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ninaangalia kwenye bajeti yetu ya mwaka 2016/2017 tulipanga shilingi bilioni tisa kutekeleza miradi ya maendeleo kwenye Halmashauri yetu ya Uvinza, lakini hadi sasa tunavyoongea mwaka jana mwezi Disemba tumepokea shilingi bilioni mbili, sawa na asilimia 22. Sasa ninajiuliza maswali, hivi kweli tutatekeleza vipi hii miradi ya maendeleo maana sasa tumeinga mwaka wa pili tangu tuchaguliwe huko na tuliahidi mambo mengi. Kwa hiyo, ninaomba kwenye Kamati hii ya Bajeti nimeona imeshauri sana, lakini haijafikia makubaliano na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, nilikuwa naangalia ukurasa wa 10. Ukiangalia ukurasa wa 10, Fungu Namba 49, Wizara ya Maji na Umwagiliaji unaona kabisa kwamba kulikuwa na hoja ya kuongeza tozo kwa kila lita ya mafuta, petroli na dizeli, kuongeza 50 ili ifike 100. Lakini lengo la Kamati ilikuwa ni kwamba fedha hizi zipelekwe kwenye Mfuko wa Miradi ya Maendeleo ya Maji Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia matokeo ya ushauriano Kamati inasema haijafikia makubaliano na Serikali. Sasa naanza kujuliza kama hatujafikia makubaliano na Serikali, hii miradi ya maji ambayo mingi imeanzishwa tangu kwenye bajeti ya mwaka 2012/2013 mpaka leo miradi ya maji haijafikia hata asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa pia, ninaangalia kwenye ukurasa huohuo, tunazungumzia kwamba, ujenzi wa zahanati na vituo vya afya kwa mwaka 2016/2020. Ukienda kwenye hoja Kamati ilipendekeza shilingi bilioni 30 ziende kwenye utekelezaji wa ujenzi wa zahanati na ujenzi wa vituo vya afya, lakini hadi sasa Serikali inasema bado haijapata itatumia shilingi ngapi katika utekelezaji wa hiyo miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe sana tumepitisha bajeti na tunaendelea na mwaka huu tena tutapitisha bajeti. Sasa hivi tunavyoongea tuko kwenye robo ya tatu ya bajeti ya mwaka 2016/2017, pesa kule chini zinaenda kwa asilimia ndogo sana. Kwa hiyo, tuombe Serikali iwe sikivu na tunafahamu Serikali yetu ni sikivu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi iweze kusikia na kuona ni jinsi gani tunapeleka pesa za maendeleo huko chini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia, nizungumzie zile milioni 50 kupeleka kule vijiji. Ukiangalia kwenye ukurasa wa 11 unaona kwamba Kamati imeshauriana na kukubaliana na majibu wa Serikali kuwa imeridhia shilingi bilioni 59.5 sawa na asilimia 45 ili iweze kutumika katika kupeleka vijiji na kutafuta zile pilot area. Sasa mimi nikawa naangalia hii pilot program hivi ni Wilaya zipi ambazo zimekuwa specifically kwamba zimekuwa ni pilot area kwa ajili ya utekelezaji wa hizi shilingi milioni 50!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nilikuwa ninaomba, najua kabisa tuna changamoto nyingi, lakini pia nimeona ukusanyaji wa mapato umekwenda kwa kasi. Ukiangalia kuna Mbunge mmoja amezungumzia kwamba, hata polisi imeingilia kwenye upande wa makusanyo. Polisi ina haki ya kuingilia upande wa makusanyo kwa sababu yale makosa yanayofanyika barabarani, polisi ikikusanya ndiyo pesa zinaingia huko katika miradi ya maendeleo mbalimbali nchini. Kwa hiyo, hatuwezi kubeza jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali yetu, hususan kuitia Wizara ya Mambo ya Ndani kwa Polisi kukusanya kodi mbalimbali za makosa. Kwa hiyo, niwatie moyo polisi, nimitie moyo IGP, nimitie moyo pia Waziri wa Mambo ya Ndani kwamba aendelee na ukusanyaji huo wa kodi ili tuweze kufanya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la kilimo; mwenzangu aliyekaa amesema zaidi ya asilimia 73, mimi ninavyofahamu ni asilimia 82 inajihuisha na suala la kilimo Tanzania, lakini pembejeo zimechelewa huko vijiji. Watu wamelima, watu wamepanda, pembejeo hazijafika. Ukipita vijiji ni malalamiko. Sasa tunajiuliza kama pembejeo zinachelewa, wakulima wataweza kuvuna vipi? Makusanyo ya Halmashauri nyingi nchini zinapata makusanyo yake kuitia mazao mbalimbali yanayolimwa kule vijiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaomba sana kwenye bajeti hii inayokuja tuweze kutenga pesa nyngi kwenye Wizara ya Kilimo. Wizara ya Kilimo ni Wizara nyeti, tunalima tumbaku, tunalima pamba, tunalima alizeti, lakini tunahitaji pembejeo za kutosha. Tunahitaji ruzuku iongezwe zaidi kama mwenzangu alivyosema kwenye mbegu.(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia nchi ya viwanda, lakini hali ya umeme ni mbaya sana. Kwa mfano, mimi naongelea Jimbo langu, katika vijiji 61 nina vijiji vitatu tu vyenye umeme, lakini Wilaya ile ndiyo tuna ozalisha mchikichi. Tunazungumzia hapa tuanzishe viwanda vya mawese, tunaanzishaje viwanda wakati umeme wenyewe hakuna. Tunafaya sensitization kwa wananchi waone umuhimu wa kulima zao la mchikichi, umuhimu wa kulima mazao mbalimbali ili tuweze kupata *raw materials* ya kuweza ku-maintain hivi viwanda. Ninaomba pia kwenye mradi, kama alivyozungumza mwenzangu, lile deni la TANESCO lilipwe, tulipe deni la TANESCO ili miradi ya umeme vijiji iendelee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo pia, tuiombe Wizara husika iweze kupunguza bei. Wananchi wengi walioko vijiji hawana uwezo wa kulipia umeme kama ambavyo sasa hivi wanavyotaka hiyo pesa tulipie. Naomba Wizara yenye dhamana ione ni jinsi gani itaweza kupunguza bei ya umeme ili basi wananchi waweze kukidhi haja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba pia kuchangia kwenye miradi ya barabara, hali ya huko vijiji tunatofautiana, sisi miundombinu yetu ni mibaya sana. Niombe katika bajeti tuweze basi zile pesa zilizotengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya barabara mbalimbali vijiji ziweze kupelekwa ili miradi hii iweze kutekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa nizungumzie suala la TRA (ukusanyaji wa mapato). Najua dhamira ya Serikali ni njema, hali huko chini sio nzuri sana, unakuta mfanyakishara kwa mujibu wa Sheria ya TRA wanasema ile *turn over* ya mwaka kama ni *less than 14 million* hautakiwi kuwa na ile mashine ya kukatia risiti wateja. Lakini kwenye maeneo mengine kama Dar es Salaam unakuta mfanyakishara ameshafanyiwa assessment na akaambiwa kwamba labda biashara yako ni milioni tisa ndiyo *turn over* kwa mwaka, lakini bado baada ya miezi miwili wanarudi wanamwambia tukiiangalia biashara yako kwa macho, tunaona kwamba wewe unatakiwa uwe na risiti, aahhaa! Sasa umeshafanya, umemkadiria, umeona kwamba yuko *less than 14 million*. Kwa nini tena urudi umwambie kwa macho tu...(Makof)

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante!

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Kamati ya Bajeti kwa Taarifa yao nzuri, ahsante. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea Mheshimiwa Innocent Bashungwa atafuatiwa na Mheshimiwa Josephat Hasunga na Mheshimiwa Sixtus Mapunda ajiandae.

**MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA:** Mheshimwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia taarifa ya Kamati ya Bajeti.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba nianze kwa kuishukuru Kamati ya Bajeti kwa kutuletea taarifa nzuri ambayo imefanya uchambuzi mzuri juu ya hali ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba kwanza kuipongeza Serikali kwa malengo mazuri ya mwaka huu wa fedha wa 2016/2017 Serikali ilitenga asilimia 40 ya bajeti iweze kwenda kwenye miradi ya maendeleo. Mipango hii ni mizuri na imelenga kuwasaidia Watanzania waweze kupata maendeleo ambayo tuliwaahidi katika utekelezaji wa ilani ya Chama cha Mapinduzi. (Makofii)

Mheshimwa Mwenyekiti, zipo changamoto na ndiyo maana nimeishukuru Kamati ya Bajeti kwamba wamejitätahidi sana kutathmini changamoto hizi na sisi tuna wajibu wa kuzijadili na kuishauri Serikali, bahati nzuri tupo kwenye *midterm review* ya bajeti. Kwa hiyo, nina imani kwamba Serikali ni sikiu na mapendekezo haya ambayo Kamati imetoa na Waheshimiwa Wabunge watatoa yatafanyiwa kazi ili tunavyokwenda kwenye *second half* ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali hizi changamoto zifanyiwe kazi na baadhi ya changamoto ziwe carried over kwenye bajeti inayofuata.

Mheshimwa Mwenyekiti, naomba nianze na Deni la Taifa, nianze kwenye ukurasa wa tatu wa taarifa ya Kamati ya Bajeti, ninukuu kuhusu mwenendo wa miradi ya maendeleo hasa hasa michango ya washirika wa maendeleo. Kwenye ukurasa wa tatu mwisho kabisa; "mwenendo wa utoaji wa fedha za washirika wa maendeleo unaonesha ni upungufu kwa asilimia 26 ya fedha yote iliyotarajiwa kutolewa. Kamati haikupata majibu ya kuridhisha kuhusu sababu za washirika wa maendeleo kutotimiza ahadi zao kwa asilimia mia moja."

Mheshimwa Mwenyekiti, kusema ukweli na mimi nipo concerned sana; tumeweka malengo mazuri, tume-target asilimia 40 ya bajeti iende kwenye fedha za maendeleo na hivi sasa tumefika kwenye nusu ya mwaka wa bajeti kwa asilimia kubwa fedha za maendeleo tulitegemea hao wahisani watakapotoa fedha ndizo tutumie kwenye kufadhili miradi ya maendeleo. Ukiangalia ukusanyaji wa TRA, ukichukua ile trilioni takribani 1.2 kila mwezi ya TRA inayokusanya ukalipa mishahara ya watumishi (*wage bill*), ukalipa madeni ya Taifa, chenji inayobaki ni kidogo mno. Tulitegemea wahisani wakitoa fedha za maendeleo ule mchango wao tutaunganisha na ile chenji inayobaki kwenda kufanya kazi za maendeleo. Wahisani kwa vile hawatoi hizi fedha kwa kweli mimi naona tupo kwenye *state of emergency, its very alarming kwamba tupo kwenye midterm review* lakini hatujapata fedha ambayo tulitarajia wahisani watupatie ili tuweze kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimwa Mwenyekiti, nini kifanyike? Ukiangalia madeni ya Taifa hayaepukiki ni lazima yalipwe. Ukilipa Deni la Taifa kwa sababu asilimia kubwa tunalipa nje hii fedha tunayolipa inaenda kusaidia ku-stimulate uchumi wa kule. Kwa hiyo, ukienda mtaani ndiyo maana unakuta wananchi wanasema hali ya uchumi ni ngumu ni kwa sababu fedha nyingi tunazokusanya zinaenda kulipa madeni ya nje na ina-stimulate uchumi wa kule na siyo uchumi wa Tanzania. (Makofij)

Mheshimwa Mwenyekiti, hii ni changamoto kubwa, nipende kushauri Wizara ya Fedha labda sijui tufanye road show kwenda kuongea na taasisi za fedha za Kimataifa. Tuangalie ni namna gani tunaweza tukapata fedha za maendeleo kwa sababu *local revenue collection* ya TRA tayari ina *commitment* ya *wage bill* na madeni ya Taifa, sasa tunafanya je ili kuhakikisha miradi ya maendeleo inatekelezwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, siyo mbaya Wizara ya Fedha ikakaa ikaangalia realistically kulingana na picha iliyopo hivi sasa na bajeti ambayo tulipitisha tunafanya je ku-adjust ili utekelezaji wa hii bajeti uwe realistic na hali ilivyo ukizingatia wahisani wamekuwa wagumu katika kuchangia asilimia zao ambazo tunatakiwa kupata.

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri atakapokuja kufanya hitimisho tungependa kujua kwa upande wa Wizara ya Fedha tupate maelezo wanafanya nini ili kukabiliana na hii hali.

Mheshimwa Mwenyekiti, niende kwenye suala la makadirio ya Pato la Taifa. Ukiangalia drivers za mapato na changamoto za maafa ambazo

zimetupata, kwa mfano, kwa Halmashauri ambazo zilitegemea kukusanya mapato kwenye kilimo, hivi sasa kwa sababu ya ukame mapato yatapungua. Kwahiyo, hii pia inaendelea kuweka presha kwenye ukusanyaji wa mapato ya ndani ambayo tulikadiria kwamba yakipatikana ndiyo yasaidie katika kutekeleza bajeti. Kwa hiyo, unaona kwamba issue inazidi kuwa serious, yale mapato ya ndani kuna changamoto zake na mapato ambayo tulitegemea kutoka nje wahisani hawatoi, kwa hiyo hii changamoto *is a serious case.* (Makofii)

Mheshimwa Mwenyekiti, niende kwenye sekta ya kilimo; wote tunakubaliana kwamba sekta ya kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wetu hasa hasa kwa upande wa Watanzania wengi wanajishughulisha kwenye hii sekta. Kwenye mpango wa maendeleo wa miaka mitano tulichangia, Waheshimiwa Wabunge tukatoa mapendekezo yetu, lakini ikija kwenye utekelezaji bado naona kuna changamoto. Kwa sababu ukiangalia hata fedha ambazo zimeenda kwenye bajeti ya sekta ya kilimo ni kidogo. Ukiangalia ukuaji wa sekta ya kilimo mwaka wa fedha wa 2014/2015 sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 3.4; mwaka 2015/2016 asilimia tatu.

Sasa hivi changamoto ambazo tumezipata za ukame na mabadiliko ya tabianchi sitashangaa tukipata takwimu za mwaka wa fedha 2016/2017 sekta ya kilimo itakuwa imeshuka zaidi. Sasa kwa sababu tuna malengo ya kuwapeleka watanzania kwenye *middle income country status*, kuna kila haja katika *midterm review* ya bajeti hivi sasa kuangalia ni namna gani tunakwenda mbele. (Makofii)

Mheshimwa Mwenyekiti, asilimia 70 ya Watanzania wanategemea sekta ya kilimo; nilitegemea kwenye mpango wa Serikali tuangalie ni namna gani tunamsaidia mkulima. Kwenye upande wa pembejeo; pembejeo ambazo tumezipata katika Wilaya zetu ni kidogo mno. Ukiangalia maafisa ugani tuna shortage kubwa kwa kila kijiji, kila Wilaya Maafisa Ugani wa Kilimo ni wachache mno na Maafisa Ugani wa Mifugo ni wachache mno. Hiso ndiyo *indicators* ambazo tuki-focus nazo na tukazifanyia kazi sekta ya kilimo ikakua tutakuwa tumesaidia kuwainua asilimia kubwa ya Watanzania kwenda kwenye uchumi wa kati. (Makofii)

Mheshimwa Mwenyekiti, kwenye upande wa masoko; lazima ile *value chain* ya kilimo tuisaidie. Tumepata tatizo la ukame, nilitegemea kuona mipango ya Serikali ya ujengaji wa warehousing, kila Wilaya iwe na maghala ya kuhifadhi vyakula, wakati wa harvest vile vyakula ambavyo vinakuwa ni surplus tunakuwa tuna maghala vinahifadhiwa vizuri, *demand* na *supply* vinakuwa-balanced kulingana na serving za mazao kwa kila Wilaya. (Makofii)

Mheshimwa Mwenyekiti, bila hizi warehousing kila Wilaya unakuta wananchi wanalazimika kutumia kile wanachokipata kabla hakijaharibika kwa sababu *preservation method* za warehousing hatunazo katika Wilaya zetu. Sekta ya kilimo ni nyeti sana na nipende kuishauri Serikali hii *midterm review* tunayoifanya wajikite sana kwa kuangalia tunawasaidiaje Watanzania kuboresha sekta ya kilimo ambayo inaa jiri asilimia kubwa ya Watanzania. Nakushukuru! (Makofij)

**MWENYEKITI:** Nakushukuru. Mheshimiwa Japhet Hasunga atafuatiwa na Mheshimiwa Sixtus Mapunda.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kupata hii nafasi ili kuweza kuchangia katika taarifa hii ya Kamati. Kwanza naipongeza sana Kamati kwa taarifa nzuri ambayo wameiandaa ambayo na mimi pia ni Mjumbe wa hii Kamati, kwa hiyo nashukuru sana kwa taarifa nzuri hii.

Mheshimwa Mwenyekiti, tunapozungumzia maendeleo na tunapotaka maendeleo ya nchi lazima tuangalie ni vipaumbele gani ambavyo vitaashiria na vitafanya nchi ione kane imeendelea. Nasema hayo nikianzia na suala la kilimo. Katika kilimo asilimia zaidi ya 70 ya Watanzania wanategemea kilimo, nchi yetu hii tume sema tunataka sasa kujenga nchi ya viwanda, hatuwezi kujenga nchi ya viwanda, hatuwezi kukamilisha hilo kama hatutaimarisha kilimo. Viwanda vinategemea malighafi na malighafi hizo lazima zitoke kwenye kilimo. (Makofij)

Hata ukiangalia nchi za wenzetu, ukiangalia Ulaya *industrial revolution* ya Europe ilianzia kwanza na *agricultural revolution*, ilianzia kwanza na mapinduzi ya kilimo; mapinduzi yale ya kilimo yakaléta mapinduzi ya viwanda. Kwa hiyo, tunaposema maendeleo lazima tuweke tuzungumzie bayana kabisa, tuwe na mkakati wa makusudi wa kuimarisha kilimo chetu na ambacho ndicho kinatoa ajira kwa watu wengi, ambacho ndiyo kitatupatia malighafi za kutosha kwenda kwenye viwanda na kitachangia kwa kiwango kikubwa katika Pato la Taifa letu. (Makofij)

Mheshimwa Mwenyekiti, hivi sasa kilimo chetu kinategemea mtu mmoja mmoja kilimo kidogo, hii haitatupeleka mbele kama Taifa. Lazima pia tuweke mkakati wa makusudi wa kuanzisha mashamba makubwa ya kilimo yatakayosaidia katika kuimarisha Pato la Taifa.

Mheshimwa Mwenyekiti, hivi sasa tunavyozungumzia kilimo nchi yetu sasa inakabiliwa na ukame katika maeneo mengi ambao tunaamini itaathiri kwa kiwango kikubwa sana maendeleo yetu ya kilimo. Mikoa ya Nyanda za Juu kama kule kwetu Songwe sasa hivi bado mvua zinanyesha na tena zinanyesha vizuri sana na wananchi wamelima mazao yanakwenda vizuri, tatizo lipo kwenye pembejeo, pembejeo sasa hivi kule Mkoani Songwe zimepanda vibaya sana. Katika kipindi cha nyuma Serikali ilitamka kwamba kwa mfano mbolea ya kukuzia ingeuzwa shilingi 26,000 lakini hivi leo ninapoongea pembejeo zimepanda sana kule Mbozi, mbolea ya kukuzia ni zaidi ya shilingi 50,000, sasa hii itasaidiaje? Hatuwezi kuendelea kwa namna hiyo. Kwa hiyo, naiomba Serikali itafute uwezekano wa kusaidia kilimo ili angalau tuweze kuinua pato la Taifa na kutoa ajira kwa wananchi walio wengi, hilo ni suala la kwanza.

Mheshimwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa kuchangia ni kuhusu usimamizi wa bajeti na nidhamu ya bajeti. Mimi nashukuru uchambuzi wa Kamati ulivyofanywa, lakini naomba nitoe ushauri wangu, fedha nyingi zinatoka kwenye Wizara ya Fedha, zinapopelekwa kwenye Serikali za Mitaa na kwenye taasisi za umma ni namna gani Serikali inasimamia na kufuatilia kwamba hizo fedha zinatumika kama zilivyopangwa, hilo ni suala la msingi sana.

Mheshimwa Mwenyekiti, pia kumekuwa na tabia kwamba katika baadhi ya maeneo watu wamekuwa wakibadilisha matumizi ya bajeti kinyume na Sheria ya Bajeti, hii siyo sawasawa. Mimi naamini Bunge baada ya kuidhinisha bajeti, bajeti inatakiwa itumike kama ilivyo na kama kuna mabadiliko basi hatua zinazoweza kuchukuliwa zifuatwe, kuliko sasa hivi mabadiliko ya bajeti yanatokea, bajeti tunapanga hapa inakuwa sasa haitekelezeki, kwa kweli hiyo itakuwa haitusaiddii kama nchi, ni vema tukawa na msimamo na tukasimamia vizuri bajeti ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, lazima tuweke vipaumbele vichache vinavyoonekana kwamba kwa mwaka huu tunataka tuwe na kipaumbele gani? Tusichukue vipaumbele vingi, hiyo itatufanya kwamba fusionekane kama mwaka huu kipaumbele ni kusambaza maji tuhakikishe mwaka huu tunasimamia kusambaza maji. Kwa hiyo, bajeti ya maendeleo ilenge katika hayo maeneo, mwaka unaofuata tunaelekeza tena upande mwingine, hiyo, itatusaidia sana katika kuweza kuharakisha kuleta maendeleo na kuwa na nidhamu nzuri ya matumizi ya fedha.

Suala lingine ambalo ningependa kuchangia linahusu mapato yasiyotokana na kodi. Kwanza niipongeze Serikali kwa kuvuka malengo ya mapato yanayotokana na kodi kwa kweli naipongeza sana Serikali. Katika

mapato ambayo hayatokani na kodi yaani non-tax revenues tumeweza kufikia asilimia 54; sasa asilimia 54 ni ndogo. Lazima tuwe na mikakati ya kutosha, tuchukue hatua zinazowezekana kuhakikisha kwamba tunaimarisha hili eneo maana lina vyanzo vingi, tunaweza tukapata mapato mengi.

Mheshimwa Mwenyekiti, ninaamini kama tukisimamia vizuri mashirika ya umma yakafanya kazi yao inavyotakiwa, yakafanya kazi kwa ufanisi, mashirika kama EWURA ambao wanakusanya fedha nyingi, mashirika kama TCRA, Civil Aviation, Reli, Shirika la Ndege na Bandari. Tukisimamia haya mashirika vizuri yataisaidia sana nchi hii kuweza kupata fedha na kupata mapato mengine yasiyokuwa yana kodi. (Makofij)

Mheshimwa Mwenyekiti, nchi nyingi zinahitaji kuwa na bandari; sisi tuna bandari nzuri. Bandari yetu ile tukiimarisha nina uhakika kabisa tunaweza tukapata fedha nyingi sana na ikiwezekana mara mbili ya bajeti tuliyonayo, lazima tuweke mkakati wa kutosha katika kuhakikisha hilo eneo tunafikia malengo. (Makofij)

Mheshimwa Mwenyekiti, nichangie pia kwenye eneo la ulipaji mzima wa kodi. Mimi naamini Watanzania lazima tuwe ni wazalendo wa kweli. Sasa hivi elimu ya mlipa kodi bado haitoshi, wananchi walio wengi bado elimu haitoshi ya ulipaji kodi. Katika maeneo mengi mimi nimeona pamoja na jitihada za Serikali, pamoja na mkazo ambao umekuwa ukitiliwa katika kukusanya kodi na watu kuwashamisha maeneo mengi ukienda dukani mtu anakuuliza; nikupe risiti au nisikupe risiti? Risiti ni haki, risiti ni wajibu wa kila mtu kutoa na wanapopanga bei zao lazima wajue kwamba kuna wajibu wa kulipa kodi, kwa hiyo, lazima hilo lizingatiwe.

Mheshimwa Mwenyekiti, naiomba Wizara ya Fedha iweke mkakati kwamba, sisi Viongozi wa Siasa, Wizara ya Fedha na Serikali lazima tufanye jitihada za makusudi za kuhamasisha ili kuhakikisha kwamba wananchi wanapata elimu ya kulipa kodi, bila kulipa kodi hatuvezi kuleta maendeleo, tutakuwa tunaimba tu. Lazima wananchi wetu walipe kodi na lazima tuisimamie vizuri.

Mheshimwa Mwenyekiti, VAT (Value Added Tax) nina uhakika kama tutaisimamia vizuri itasaidia sana.....

**MWENYEKITI:** Ahsante.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sixtus Mapunda atafuatiwa na Mheshimiwa Platei Massay.

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa na mimi nafasi ya kuchangia kwenye taarifa ya Kamati. Awali ya yote niungane na walioipongeza Kamati kwa kazi nzuri walioifanya ya uchambuzi na kutupatia mwelekeo, huenda bajeti ijayo ikawa nzuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imefanya kazi kubwa ya kutuonesha maeneo gani tunapaswa kuyafanyia kazi kama nchi, Kamati imetusaidia kutuonesha hali halisi ya nchi yetu iko wapi katika masuala ya kiuchumi na vilevile kutuwekea mazingira mazuri ya kutuwezesha kufanya tathmini na kujipanga kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuipitia taarifa hii nimeona kuna mambo mawili, matatu tunapaswa kujifunza na wataalam wetu watusaidie. Sina hakika kama tumewahi kuijuliza swali kitu gani kinacho-run uchumi wa nchi yetu. Ukiangalia kwa umakini vipimo vinavyotumika kuielezea Tanzania inaendelea au haiendelei ukitafakari kwa makini unakuja kugundua tunaishi Kitanzania na tunafikiri Kiulaya. Mwisho wa siku tukitafsiri fikra za Ulaya kwenye maisha ya Kitanzania tunakuja na majibu kwamba uchumi unakua halafu tunaona idadi ya maskini inaongezeka. Kwa nini hili linatokea? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya World Bank inaeleza itakapofikia mwezi August *inflation rate* itashuka, inaweza ikafika 4.5 kutoka kwenye 6.5. Hata hivyo, katika kipindi hiki uchumi wa nchi yetu unaonekana unaendelea kuimarika na wakatoa sababu kwa nini tunaendelea kuimarika. La kwanza wananolisema ni kwamba Tanzania ina *political stability* nzuri yaani nchi yetu ina utulivu wa kisiasa kiasi kwamba tuna fursa zote za kufanya nchi yetu ikaendelea. La pili, nchi yetu ina fursa za kiuchumi nyingi za kutosha ambazo bado nyingine hazijatumiwa katika kiwango cha kusema hii nchi ni kuzimu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unaposema kiwango cha umaskini kimeshuka halafu taarifa hiyohiyo inakwambia maskini wanaongezeka unaweza ukasema hii hai-make sense, ni kwamba tumeshindwa kutafsiri maisha ya Watanzania. Hivi kuna utafiti gani umefanyika baada ya kujengwa kwa barabara ya Dodoma - Iringa kuititia Mteria ukafika katika vile vijiji vilivyojengwa

baada ya ile barabara wanaiza nyama za mbuzi pale, kuna mtu ameweza kujuia pato lao kwa siku ni shilingi ngapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu amewahi kufika Mbinga akakuta matuta kumi ya viazi yanayomfanya mwananchi pale aishi akienda dukani anakwenda kununua tu sabuni, chumvi na mafuta ya taa, akakaa Januari mpaka Desemba akaiza magunia yake mawili ya mahindi akampeleka mtoto wake shulenii akasoma halafu mwisho wa mwaka mnasema huyu kwa siku yuko chini ya dola, vipimo gani tunavyovitumia? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba wataalam wetu mtusaidie. Katika kipindi hiki nchi yetu imeendelea sana ndiyo maana wanasema uchumi wa nchi unakua. Anayesema maisha ya Watanzania hayakui ni kwamba hajakwenda *into details*, hajaenda kuangalia familia kwa familia tukoje. Hivi tuseme ule ukweli, kama kweli hapa ndani wote tuna familia na kuna watu tunawalea, kama tupo chini ya dola kweli tungeishi? Mnaelewa maana ya chini ya dola, maana yake tunaishi chini ya Sh. 2,000 kwa siku mtu ana familia ya watoto saba hakuna mtu anayekufa na njaa, does it make sense? Kuna vitu vingine mimi sivielewi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaombe wataalam, tukitaka tulingane na nchi nyingine zilizoendelea kama Asian Tigers, tukiwaufata tutapotea. Tukitaka tukajifunze Botswana kama wengine wanavyosema tutapotea. Mfumo wa Tanzania ni wa kipekee, unahitaji *study* yake ya kipekee utaleta matokeo tunayoyataka. Tukienda hivi, wachumi hawa wamesoma sana wamekuja na makabrasha na hawa si ndiyo walioshauri bajeti iliyopita, si ndiyo hawa wanaokuja na vyanzo vya mapato vilevile!

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niseme kabisa, tunahitaji a serious discussion, we need serious research kuhusu uchumi wa kipekee wa Kitanzania unapoishi na watu wanaoishi chini ya dola wakati huohuo wakaweza kusomesha, wakaweza kula, wakaweza kujenga, hii hali sio ya kawaida. Tutadanganyana tu na haya makaratasi hapa, tunasema uchumi umepanda, uchumi umeshuka, tutapelekwa kulia, tutapelekwa kushoto hatutafika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo maana nikasema, kinachotutesa sisi na narudia tena, ni kufikiri Kitanzania, kuishi Kitanzania lakini tunadhani kwamba mifumo ile ya Ulaya ya uchumi ndiyo inayofaa kutafsiri uchumi wetu. Mipango ya Ulaya ya kukuza uchumi na projection zao ndiyo tunadhani zinatufaa kwa

Watanzania, zimefeli na hazikuwahi kufanikiwa kutuletea majibu yanayotakiwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nenda kaangalie hali ya maisha ya kawaida ya Mtanzania, sawa, kuna vitu kama nchi lazima tuvifanye, tukivifanya hivyo tuna uhakika ile gap inayoonekana watu kuongezeka kuwa maskini kwenye maandishi ikapotea ni kwenye suala la *infrastructure*. Bajeti zijazo zijielekeze kwenye *infrastructure*, reli ya kati iimarike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi reli ya kati ilipokuwa inafanya kazi mtu wa maisha ya chini alikuwa anakula wale dagaa wanaotoka Kigoma, walikuwa wakifika Dar es Salaam ndiyo chakula kinachokuwезеша kuishi, unanunua kilo moja kwa Sh. 200, 300 leo hii kilo moja ya dagaa wa Kigoma anayeweza kula ni from royal family, kwa nini? Kwa sababu reli ya kati imeshindwa kuleta ule mitiririko uliokuwa una-cover matatizo mengine. Sasa tukiimarisha reli ya kati haya mambo mengine yote yatakwenda vizuri. Tukifungua barabara, kama nilivyosema, leo mimi nikitoka Dar es Salaam kwenda Mbanga sihitaji kupita Iringa, nitapita Masasi nitaongea na Ndugu yangu Mheshimiwa Mwambe dakika mbili nasonga mbele naingia Mbanga haraka. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hali kama hii, leo inapasuliwa barabara hii ya Arusha kwa kupitia Msalato unapunguza kilometra nyingi ambazo tulikuwa tunazitumia kwenda Singida. Hali kadhalika ukatoboa barabara ya Kigoma – Mpanda – Sumbawanga na ukatoka Sikonge – Mpanda ukaja Tabora utaratibu unakuwa mzuri. Haya ndiyo maendeleo, tusiende kwenye hizi figures ambazo zinaonesha namba, hazina uhalisia katika hali ya kawaida. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli nakubali maendeleo ni watu, hatuwezi kusema kuna maendeleo ya vitu tukayatofautisha na maendeleo ya watu. Tukawa na barabara, viwanda, watu wakawa wanasononeka hawana furaha wanaishi maisha ya hovyo, haya siyo maendeleo. Maendeleo ya nchi yetu ni maendeleo ya watu.

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MHE. SIXTUS R. MAPUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. (Makof)

**MWENYEKITI:** Tunaendelea na Mheshimiwa Platei Massay atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Mbogo.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ambayo Mwenyekiti ameitoa ya Kamati yetu hii. Nami niseme ni Mjumbe wa Kamati ya Bajeti na kimsingi nimetaka tu kusema machache ambayo wenzangu mengi wameyasema, nataka kukazia machache ambayo kimsingi hayaona katika Kamati yetu yamekuwa ni changamoto.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka hasa kuzungumzia kwenye sekta ya kilimo ambayo wengi wetu wamesema habari ya uchangiaji kwenye pato la Taifa. Ukiangalia sekta ya kilimo inategemewa na wananchi wetu wengi sana kwa kipato. Ni kweli Serikali imewekeza fedha katika eneo hili lakini kwa uchache sana. Ukiangalia sasa hivi, ukuaji wa sekta ya kilimo, mwaka wa fedha wa 2014 inaonekana ulikua kwa asilimia 3.4 lakini mwaka huu kwa robo hii ya kwanza ambayo tumeiona ina ukuaji mdogo sana wa asilimia tatu. Nashauri Serikali iwekeze zaidi katika kilimo na mifugo kwa sababu wananchi wetu wengi wanaitegemea sana sekta hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo maeneo machache ambayo Serikali imejitahidi hasa katika kupeleka pembejeo za kilimo katika maeneo yetu lakini ukiangalia pembejeo zile zina utata, zinachelewa sana kuwafikia wakulima mara nyingi zinafika wakati ambapo mvua zenyewe zimekwisha kunyesha. Nishauri kidogo Wizara hii ya Kilimo kuangalia maeneo ambayo wanapeleka pembejeo hizi kupeleka kabla ya mvua ili wananchi waweze kupata pembejeo hizi mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mwaka huu Serikali imepeleka asilimia kidogo sana kwa wananchi wetu hasa pembejeo hizi ambazo kimsingi kwa sasa zimekuwa zikipiganiwa sana, Mikoa mingi imepata pembejeo baada ya mvua kunyesha. Pamoja na haya yote mazao yanayopelekwa kule, kwa mfano mahindi, yanapelekwa ya muda mrefu wakati wananchi wanahitaji mahindi au mbegu za muda mfupi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niombe Wizara iangalie wakati wanapeleka pembejeo hizi wapeleke pembejeo ambazo zinafaa kwa maeneo husika. Wataalam watusaidie kufanya research ili wajue katika ukanda fulani kama ni Nyanda za Juu Kusini, Mashariki au Magharibi, ni mbegu gani hasa inapaswa kupelekwa katika kusaidia jamii yetu. Vinginevyo wakiwa wanapeleka kama sasa kwa mfano wanapeleka hybrid maeneo ambayo yanahitaji samsung, itakuwa haina tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niizungumzie moja kwa moja kwa undani kwa sababu kilimo tunakifahamu. Mara nyingi pembejeo zinazopelekwa mahali pale wakulima wanakuwa hawazipendi tena kwa sababu ni za muda mrefu na hazifai katika eneo hilo zinapopelekwa. Kwa hiyo, naomba kabisa Serikali iangalie upya suala hili la pembejeo tunazopelekwa katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa pembejeo zinapelekwa wakati ambapo wananchi hawazihitaji tena, Serikali iangalie kama inawezekana ilete Bungeni tuone namna nzuri ya kusaidia twende kwenye mfumo wa moja kwa moja ili pesa hizi zinazotumika katika kupeleka pembejeo zitumike katika kushusha mbegu za mazao haya kuliko kupeleka msaada ambao mara nyingi unakuwa hauna tija tena katika maeneo yetu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niende kwenye eneo hili la mikopo. Serikali au Chama cha Mapinduzi ukiangalia llani yetu tumeweza kuonesha kwamba tunaweza kuwapa mikopo hii ya shilingi milioni 50 kila kijiji. Katika maeneo haya Kamati imejadili kwa kina na niipongeze sana Kamati yetu kwa sababu tumeona na niipongeze Serikali wamejiandaa kwa pilot area. Sasa niombe zile *institutions* ambazo zinahusika na suala la fedha ziwe aware katika kuelekeza na kutoa elimu ambayo itasaidia katika vijiji vyetu wakati pesa hizi zikifika kule chini. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri haya kwa sababu unajifunza kutokana na makosa yanayotokea mara nyingi sana katika jamii yetu. Ukiangalia miaka iliyotangulia katika Awamu ya Nne kulikuwa na mabilioni ya pesa maarufu Mabilioni ya Jakaya. Pesa hizi hazikufanya vizuri kwa sababu hazikuwa na monitoring nzuri. Sasa niombe, ili kuwa na matokeo chanya fedha hizi zikifika katika maeneo yetu ya vijijini pawe na mpangilio mzuri na elimu itolewe kabla ya kupelekwa fedha hizi katika maeneo haya ili wananchi wajue kabisa fedha hizi ni za mikopo, wasione fedha hizi ni bakshihi wakazitumia bila kujua namna ya kuzirudisha. Kwa maana najua wazi pilot area hela zitapelekwa maeneo machache ili waweze kurudisha na maeneo mengine yaweze kupatiwa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka tena kuzungumzia suala la afya au Wizara yetu ya Afya. Ni wazi tumeona jinsi bajeti ya afya ilivyokuwa na changamoto hasa kwenye masuala ya dawa. Nataka niende katika maeneo mengine ambayo kimsingi wengi tumekuwa tukihitaji kujengewa zahanati na vituo vya afya. Tulikuwa na mpango wa kujengewa vituo vya afya na zahanati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mpango uliopo ni kujengewa zahanati, lakini kwenye maeneo yetu ya Halmashauri kuna maboma mengi sana ambayo hayajafikia kumalizika. Wananchi wengi wamejenga hospitali na zahanati na vituo vya afya ambazo zingine zipo kwenye lenta, madirisha na nyingine imebakia tu *finishing*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Wizara ya Afya katika bajeti ijayo ione namna gani ya kuleta bajeti ili angalau tuweze kujenga au kumalizia vituo vyetu. Kwa mfano, Wizara ya Afya ikiamua ikaleta bajeti ambayo angalau kila Halmashauri ikajengewa kituo kimoja cha afya kwa mwaka wa fedha hii itasaidia sana. Hakuna Halmashauri ambayo imo haina viporo hivi. Kwa maana hii basi tukiwa na Halmashauri 183 zikajengewa kituo kimoja cha afya kwa mwaka mmoja, kwa miaka mitano ukizidisha mara nne tutakuwa na vituo zaidi ya 800 ambavyo vimejengwa kwa mwaka mmoja. Kwa hiyo, kwa kufanya hivi katika miaka mitano kufikia 2020 tutakuwa tumejenga vituo vingi na vilivyomalizika. Kwa hiyo, huo ulikuwa ni ushauri wangu wa jumla katika Wizara hii ya Afya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende katika suala la umeme vijiji. Itakuwa ndoto sana kwa Tanzania ya viwanda kuweza kupatikana bila kuwa na umeme wa uhakika. Inaonekana kabisa kwamba fedha ambazo zimepelekwa katika umeme (*REA Vijiji*) ni asilimia chache na sasa hivi tunasema *REA III* na *REA II* ambayo kimsingi inategemea kumalizika, bado maeneo mengi *REA II* hajafikia ukamilifu wake. Niombe Wizara iweke msukumo ili ile *REA III* iweze kuanza mapema, najua kwamba inakwenda kuanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia Wizara iwaangalie wakandarasi hawa wanapopewa tenda wawe na uwezo wa kumaliza kazi mapema. Tangu Awamu ya Nne yapo maeneo ya *REA II* ambayo mpaka sasa hayajakamilika kabisa. Hali hii inaweza kutudumaza zaidi sisi Watanzania na kauli ya Mheshimiwa Rais ya kutegemea kupandisha Tanzania iwe katika uchumi wa kati itakuwa ndoto kama tusipoangalia maana kiwanda hakiwezi kuendelea bila umeme. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati huohuo niipongeze Wizara ya Maji inajitahidi sana katika maeneo haya ya kumalizia viporo vya maji. Kuna mpango ambao tunaendelea nao huu wa maji vijiji, niombe kabisa Wizara ya Maji na Waziri wa Fedha aone pia ipo miradi mingi ya maji ambayo kwa sasa ni viporo. Naomba sana Wizara ya Maji iangalie maeneo yale ili iweze kutoa fedha, hasa fedha ambazo naziona zinakuwa kizungumkuti...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, naomba tulisaidie Bunge sana, napenda sana michango yenu wote, ni mizuri tu lakini mfahamu kwamba taarifa hizi zote tulizoanza jana, leo mpaka siku ya Ijumaa zina maoni na mapendekezo ambayo baadaye ndiyo mnakuja kupitisha maazimio, yanakuwa ni maamuzi ya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge, najua changamoto tulizonazo ni nyingi hasa kwenye maeneo yetu, lakini tutakuwa tunalisaidia sana Bunge kama katika kila taarifa hizi za Kamati tunajielekeza kwenye yale maoni na mapendekezo yao kuona wamesema nini. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa hilo. (Makofi)

Sasa tunaendelea na Mheshimiwa Mbogo atafuatiwa na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nianze kumshukuru Mungu wote tupo salama mpaka siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa namna ya pekee ambavyo wameweza kunyanya kiwango cha ukusanyaji wa mapato yanayotokana na kodi na yale ambayo hayatokani na kodi, tunapongeza sana. Tukiangalia miezi hii sita ya mwanzo TRA wameweza kukusanya 7.2 trillion ukilinganisha na miezi sita kama mwaka wa fedha uliopita 6.4. Kwa hiyo, ni hatua nzuri na Mheshimiwa Rais aendelee na juhudhi hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini upande wa Halmashauri zetu zimefanya vibaya kidogo. Wamekusanya shilingi bilioni 117 ambayo ni sawa na asilimia kama 70, sababu ni zipi? Bado tuna vyanzo vichache vya mapato au kuondolewa kwa property tax na kukusanya kwa upande wa TRA? Kwa hiyo, tungeomba Serikali waweze kuangalia suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tatizo lililopo pia ni haya mapato ya Halmashauri jinsi gani yanapelekwa kwenye miradi ya maendeleo. Halmashauri nyingi kutokana na uhaba wa OC wanatumia fedha zote na kwenye miradi ya maendeleo haziendi. Kwa hiyo, Serikali ifanye tathmini ya hii miezi sita, mapato

ya ndani kila Halmashauri ilikuwa ni ngapi na kulingana na sheria ya asilimia 60 kwenda kwenye miradi ya maendeleo wamepeleka asilimia ngapi. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niipongeze Kamati kwa kazi nzuri sana ambayo wameifanya. Wametoa maoni na tunaomba Serikali iyachukue. Kwanza tukianza na pendekeso la kujenga zahanati kwa Serikali kutoa shilingi bilioni 30, ni muhimu sana. Tuna vijiji karibu 12,800 sina takwimu za haraka sidhani kama vijiji zaidi ya asilimia 60 vina zahanati. Halmashauri yangu nina vijiji 59 lakini zahanati zipo kwenye vijiji 17 tu na ukiangalia uwezo wa Halmashauri nyingi kuweza kukamilisha masuala haya ni ngumu. Kwa hiyo, tuombe Serikali hiyo shilingi bilioni 30 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati kwenye bajeti ya 2017/2018 waiweke. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Kamati imeiomba Serikali kuongeza tozo kwenye mafuta kwa ajili ya Mfuko wa Maji. Sera ya Maji ya mwaka 2012 inasema kwamba wananchi watapata maji ndani ya mita 400 lakini mfano kwenye Jimbo langu mtu anakwenda kufuata maji mpaka kilometra tatu, ni tofauti na sera. Sasa tukishaitunga sera ni lazima tuweke mipango ya kuweza kuitekeleza. Mipango yenye ndiyo hayo maoni ya Kamati tuongeze kwenye mafuta kutoka sh. 50 mpaka sh. 100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge la bajeti ya 2016/2017 tulihimiza sana hapa ndani, lakini Serikali haikuchukua ikasema tutaangalia bajeti hii, sasa bajeti hii tunaomba msiangalie basi mkubaliane na maoni ya sisi Wabunge ili tukatatue matatizo ya maji vijijini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Jimbo langu asilimia 34 ya wananchi ndiyo wanaopata maji safi na salama. Kwa hiyo, ni jinsi gani tutaweza kutatua hili tatizo la maji, tuongeze hii shilingi 50 na tunaomba sana hiki kilio mkisikie. Kwa kufanya hivyo ndiyo utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi kwani wananchi wana kilio sana na maji na sisi Wabunge tunasema tukitatua tatizo la maji hata 2020 mtatuona tena humu ndani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika llani ya Chama cha Mapinduzi tumeahidi kutoa shilingi milioni 50 na Serikali imekubaliana, wametenga kwenye bajeti shilingi bilioni 59. Hata hivyo mpaka sasa hivi ule mpango mzima wa jinsi gani huu mfuko utaendeshwa ili tuondokane na yale matatizo ya awali yaliyotukumba kwa zile fedha maarufu zikiitwa za JK ambazo watu waliona ni za bure na hata hizi shilingi milioni 50 wananchi kule wanafikiria ni za bure, hapana! Tunaomba tuwaambie wananchi hii itakuwa ni *revolving fund*, mnakopa kwa riba iliyo ndogo ili na wengine waweze kukopa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Serikali iangalie uwezekano wa kwenda angalau kata chache kwa kila Jimbo. Kupeleka shilingi milioni 50 kwenye kila kijiji itahitaji fedha nyingi sana. Sasa hivi tukiangalia makusanyo ya ndani ya Halmashauri, zile asilimia 10 kwa ajili ya vijana na akinamama wanaojitokeza kukopa hawakopi kwa kiasi kingi. Kwa hiyo, hata hii shilingi milioni 50 kwa kuwa itahitajika hela nyingi na makusanyo yetu hayatoshelezi kama bajeti ilivyo, basi tuangalie kata chache ziwe kama za mfano tuguse kila Jimbo angalau hata kata mbili shilingi milioni hamsini hamsini ndiyo tuanze kama mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wamezungumzia kuhusu mapato. Naomba nichangie, zile ripoti, Chenge I na II bado Serikali irudi mle ikapekue. Suala la *deep sea fishing* hatujalisikia na masuala mengine. Kwa hiyo, tunaomba sana kwenye hii bajeti, Waziri wa Fedha na Kamati ya Bajeti mrudi kwenye ile ripoti ya Chenge I na II muangalie maeneo yote ya mapato ambayo yalielezwa ambayo yatasaidia katika bajeti yetu. Mwelekeo wa bajeti ni shilingi trilioni 32, tunatoka kwenye shilingi trilioni 29. Sawa, mmeweka vyanzo vingine pale lakini muangalie jinsi gani tunaweza tukafika hata shilingi trilioni 34 kutokana na vyanzo vingine vipyta ya mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wamelalamika kuhusu Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye utalii, basi Serikali ifanye utafiti, je, kweli hii kodi ambayo imewekwa kwenye auxiliary services za watalii imepunguzwa kwa kiasi gani ili watu wapate uelewa? Nafikiri wakati Waziri Mkuu anafunga Bunge, naomba Waziri wa Maliasili na Utalii ampe hiyo taarifa aweze kuisoma hapa tupate uelewa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, biashara imeshazungumzwa upande wa *transit goods*, tumeweka VAT ambayo imeleta mgogoro sana na mizigo yetu mpaka kupungua. Tunamshukuru Mheshimiwa Rais jinsi alivyoweza kujenga mahusiano na viongozi wa nchi jirani na sasa biashara imeanza kurudi na tumeona kwenye vyombo vya habari hivi karibuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masuala ya kilimo kama ndiyo Utii wa Mgongo na asilimia 70 ya ajira. Tunaomba ruzuku iongezwe na pembejeo zije kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna eneo ambalo bado hatujaona ni jinsi gani tunaweza kupata fedha ni upande wa mifugo. Tuweke *blocks* za ulishaji na watozwe. Kwa hiyo, Serikali iangalie suala hili na tupunguze migogoro hii ya

wakulima na wafugaji na tuone ni kwa jinsi gani tunaweza kupata mapato kutoka kwenye mifugo, hili ni eneo ambalo bado hatujaliweka sawa. Tunatoza mifugo tu inapouzwa mnadani lakini kwa kila siku inavyokuwepo na uharibifu wa mazingira kama tunavyoolewa, tuangalie tunawekaje tozo katika mifugo ili tuweze kuongeza mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kamati wameeleza suala la utawala wa Kibunge kwamba Bunge sasa litakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, Wabunge na Kamati nyingi hazikuweza kwenda kukagua miradi ikiwa ni sehemu ya kuisimamia Serikali kwa mujibu wa Katiba, Ibara ya 63 kwamba Bunge tuna wajibu wa kutunga sheria na kuisimamia Serikali. Sasa tunavyoenda kama Kamati kukagua miradi ya Serikali ndipo tunapoisimamia. Kamati nyingi hazijafanya safari na maslahi ya kiujumla kwa mfano, je, Mbunge anatakiwa akakae hoteli ya nyota ngapi? Kwa hiyo, tuangalie maslahi ya Wabunge na gharama kiujumla katika kufanya kazi zao za kuweza kuisimamia Serikali. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyokagua miradi ndiyo tunatia chachu kwa watumishi wetu kule, wakisikia Kamati inakuja ndipo utaona mambo mengi yanakwenda mbiombio wandakimbizana. Tunapotoa maagizo inasaidia sana katika kutekeleza miradi na ndipo tunaleta tija kwa wananchi ili waweze kujua kwamba Serikali yao sasa imewaletea miradi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho naomba niseme kwamba, tunaenda nchi ya viwanda lakini tunaomba Serikali iangalie uwiano. Siku za nyuma Hayati Mwalimu Nyerere alijaribu kuangalia uwiano wa Kikanda kuweka viwanda ili kuweka usawa katika ajira. Kwa mfano, Mikoa ya Kigoma, Katavi, Tabora, Chunya wanalima tumbaku. Je, hatuna haja Serikali ikashawishi NSSF au PPF, hii Mifuko ya Jamii wakaingia ubia na Vyama vyetu vya Msingi kutoa mchango wao kwa kujenga kiwanda Tabora ili ...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Tunaendelea na Mheshimiwa Wilfred Lwakatare atafuatiwa na Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Awali ya yote nitumie fursa hii pamoja na majanga na madhara yote ambayo tumeyapa Mkoo wa Kagera lakini niupongeze Mkoo wa Kagera na hususani Walimu wetu wa Mkoo wa Kagera wa shule za sekondari kwa Mkoo wa Kagera kujitokeza kuwa Mkoo wa tatu kwa matokeo mazuri Kitaifa. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini sambamba na hilo, niipongeze Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ikiongozwa na kijana wa mvuto na mnato Chief Kalumuna kama Mstahiki Meya kwa kuongoza Baraza, Halmashauri, Walimu na shule za sekondari kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ninapotoka mimi ku-appear kama namba moja Kitaifa katika matokeo ya form four. Naomba ushirikiano ambao tunao pale Bukoba Mjini bila kujali itikadi zetu za kisiasa, sisi tukipiga mzigo tunapiga mzigo kweli kweli na matokeo yake tumeyaona kwa matokeo ya mwaka huu, nawapongeza sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili, katika Mpango wa Maendeleo ulioletwa mwaka jana hapa, nilizungumza kwa kina kabisa matatizo ya Mkoo wetu wa Kagera na majanga ambayo tumeyapata na ya kihistoria ambayo yanababisha mkoaa ule kuwekwa katika orodha ya mikoa maskini. Japo matukio hayo ambayo yanatuathiri wananchi wa Mkoo wa Kagera yamegeuzwa sasa kama utani na majina mengine kutumika kama kututania japo ni majina ya kihistoria tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba Serikali kama Serikali na kupitia katika bajeti na mipango ambayo inaletwa na imesomwa hapa na Kamati, ni kazi ya Serikali kusimamia...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lwakatare majina gani umesema?

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Majina?

**MWENYEKITI:** Ndiyo.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Haya. Mwenyekiti ametaka kujua majina ambayo ni ya kihistoria na nafikiri watu wamekuwa wanayatumia vibaya majina kama Mto Ngoni, Katerero, hayo ni majina tu ambayo yana historia yake. Kwa hiyo, naomba watu wanayoyatumia wanione niwaeleze umaana wake wasiyatumie vinginevyo. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kazi ya Serikali kuangalia ustawi wa watu wake. Sisi wananchi wa Kagera na hususani Bukoba Manispaa ninapotoka

Mwenyezi Mungu alipotuweka kule kijografia na tukaumbwa kukaa katika nchi ya Tanzania badala ya Uganda hatukukaa kule kwa bahati mbaya. Serikali inapaswa itambue umbali wa kutoka kwenye centre ya maamuzi na sehemu kubwa ya kiuchumi kama Dar es Salaam na tukawa Bukoba, Serikali inapopanga mipango yake lazima izingatie suala la cost and price standardization katika baadhi ya mambo ambayo yanaweza yakatusaidia sisi kama Watanzania na kama Watanzania wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapozungumzia kwamba baada ya tetemeko kumejitokeza tatizo la watu kupata malazi na kujenga upya nyumba, ni suala ambalo Serikali inapaswa ilizingatie katika mipango yake. Mama Ghasia na Kamati nzima kwa ujumla nawaomba tunapokwenda kwenye bajeti ya mwaka huu bila kuli-address suala la Kagera na matatizo ambayo tumeyapata na nimesikitika pamoja na kwamba tumekuwa tunalizungumza na Mheshimiwa Conchesta na jana amezungumza, inapokuja wakati wa majumuisho sijasikia mtu anayelizungumza hili lakini sisi kama wawakilishi wa wananchi wa Kagera hatutaacha kulizungumza kwa sababu tetemeko limeacha limetusambaratisha, uchumi umeparaganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu fikiria mtu ambaye wamechangishana wakajenga nyumba kwa miaka saba anaishi na familia yake, leo tetemeko la sekunde tatu linasambaratisha kila kitu maana yake ni kusambaratisha uchumi wa familia na ukoo kwa ujumla. Sasa tunapokuja kutaniana na naomba Mheshimiwa Msigwa ambaye ni Mwandishi Mkuu wa Mheshimiwa Rais pale lkulu awe anatusaidia kutoa matamko kwamba safari hii Rais alikuwa anatania au safari hii Rais yuko serious. Hata leo nilisikia Rais wa Chama cha Wanasheria akihojiwa akasema aah, aah Rais alipowaeleza Majaji na Mawakili kwamba kuna Majaji amba wanatetea wahalifu alikuwa anatania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba labda kuwe kunatolewa matamko kwamba Rais hapa anatania, hapa yuko serious kwa sababu mahali pengine utani mwingine unakuwa wa ukweli. Mfano pale alipotamka kwamba magari na pipipiki zikipita kwenye barabara ya mwendokasi zing'olewe matairi na Mapolisi wakaamka wameng'oa matairi ya pipipiki zote. Hata tulipoelezwa akina Lwakatare twende tukajenge Kiwanda cha Mabati ili tukauze mabati kwa Sh.1000, sijui Rais alikuwa anatania au alikuwa serious? Kwa hiyo, kama Rais alikuwa hatanii katika mipango ya bajeti tuanze na suala hili la cost and price standardization kwa vifaa vyatya ujenzi vinavyokwenda Kagera kama imeshindikana katika kuangalia policy na taxation kupunguza bei ya vifaa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sukari inalimwa Kagera lakini inauzwa Sh. 2,000, Sh. 2,200 hata pale pale Bukoba pamoja na kuwa kiwanda kipo kilometre 20 kutoka Bukoba Mjini lakini bei ni ile ile inayouzwa sukari Singida au Kahama ni kwa sababu ya standardization ya price. Vilevile TBL wanauzwa bia Sh. 2,500, Sh. 2,000 au Sh. 1,500 hapa Dodoma na bei hiyo hiyo unaikuta Bukoba, kwa nini suala la cement, nondo, mabati ishindikane? Kwa nini Serikali kupitia kwenye bajeti na mipango thabitii isiliangalie suala hili ili wananchi wa Kagera kama ambavyo ni Watanzania wenzenu tukaweza kurudisha uchumi wa Wanakagera na makazi, tukajenga nyumba zetu kwani sasa hivi hali ni mbaya, nolieleza hili lieleweke. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mtakapokuwa mnajumuisha na hasa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, naomba asipotezee kama ambavyo mmekuwa mnapotezea hamtujibu watu wa Kagera, mnatusadiae suala hili katika mipango ya bajeti kwa sababu hali ni mbaya. Nolieleza hili na nitaendelea kulieleza kusudi lieleweke na hiyo ni sehemu ya kazi ya Serikali kuangalia wananchi wake wanapata malazi, chakula na mavazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tetemeko kutokana na uchumi kuparaganyika, Mkoa wa Kagera unategemea kupata njaa ndani ya mwezi Machi, hili tunalizungumza kwa uwazi, kutakuwepo na njaa. Natoa ilani hiyo acheni kutuletea takwimu ambazo ni za *imaginations*. Waheshimiwa njaa haina bouncer, tunaomba kabisa kabla janga hili halijaukumba Mkoa wa Kagera na hususani wananchi wa Bukoba Mjini ambao tunanunua ndizi kutoka Karagwe kwa Mheshimiwa Innocent, ndizi Mheshimiwa Innocent atawaambia, hakuna ndizi Muleba, hakuna ndizi Karagwe, wananchi wa Bukoba Mjini ambao sisi huwa tunatembeza mchuzi kununua ndizi, tuko katika hatari ya njaa na sasa hivi bei za vyakula zinapanda kama vile hazina akili nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nawaomba mtakapokuwa mnajumuisha hapa hebu toeni tamko mmejpangaje kutusaidia wananchi wa Kagera katika suala hili na hasa katika kuhuisha mfumo utakaowawezesha watu wapate vifaa kwa bei ya chini kwa sababu hali ni mbaya, ni mbaya, ni mbaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kagera nafikiri watanisikia Lwakatare hapa jembe lao nazungumza tena kwamba hali ni mbaya. Serikali itusikilize, iache kuja kututania mambo ya Katerero, mambo ya ngono hayatusaidii, sisi tuna shida. Wanaotaka Katerero waje tutawafundisha kijiji kipo, huo utaalam tutawafundisha. Ahsante. (Makofi/Kicheko)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Waheshimiwa Esther Matiko atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru nami kuweza kupata fursa hii ili niweze kutoa maoni yangu kufuatia ripoti ya Kamati ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nionyeshe masikitiko yangu ya kwamba katika ripoti hii ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni robo moja tu ndiyo tumeletewa katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka huu. Tuko robo ya tatu sasa hivi kwa hiyo nilitarajia kabisa tungeweza kupata mpaka robo ya pili ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017. Cha kusikitisha zaidi tunaona ni kwa kiasi gani bajeti hii haitekelezeki kama vile ambavyo tuliletewa hapa. Ikumbukwe wakati tumeleta hii bajeti mwanzoni nilisema kabisa kwamba hii bajeti haina uhalisia na nitashangaa sana kama hata itafikisha asilimia 70 ya utekelezaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyoongea hivi leo, fedha za maendeleo hazijakwenda kwa kiasi kikubwa sana lakini zaidi madeni. Juzi wakati Waziri anatoa kuhusu hali ya madeni na hapa nisikitike kidogo kwa mwanafunzi wangu Stanslaus anasifia kwamba wanalipa sana madeni. Nizungumzie tu baadhi ya haya madeni ya Watanzania wa ndani ambao wanaidai Serikali na inapelekea hata hawa Watanzania wanauziwa mali zao na wengine wanajiu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa aliyotoa Waziri mwenyewe hapa ndani anaeleza kabisa kwamba mathalani wakandarasi wanadai shilingi trilioni moja, bilioni moja na milioni mia nne na mpaka sasa hivi wamelipa tu shilingi bilioni 360. Wanaotoa huduma za ndani wanadai shilingi bilioni 237 na wamemaliza kulipa shilingi bilioni 11 tu. Wazabuni wanadai shilingi bilioni 900 na kwa mujibu wa taarifa ya Waziri ya tarehe 19 wamelipa shilingi bilioni 49 tu. Hivi tunavyoongea hawa watu wanaotoa huduma hospitalini, shuleni, majeshini wanasitisha kwa sababu Serikali mmeshindwa kuwalipa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti sasa ningependa kujua mkakati wa utekelezaji wa ulipaji madeni haya ukoje. Jana mnasema madai ya Walimu mnafanya uhakiki yaani sasa hivi Serikali inajificha kwenye kufanya uhakiki. Madeni ya pembejeo tunafanya uhakiki, madeni ya Walimu tunafanya uhakiki, madeni ya wazabuni mnafanya uhakiki, kuajiri watu mnafanya uhakiki, muwe wazi mseme Serikali haina fedha ili Watanzania wajue kwamba Serikali haina fedha, kama wanauziwa mali zao ni kwa sababu Serikali haitaki kuwalipa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho kinasababisha hata Serikali isipate mapato kama ilivyokuwa ime-project, tulisema hapa kuna kodi zingine mmeziweka ambazo hazina uhalsia, hazitekelezeki, kodi kwenye sekta ya utalii, kodi kwenye *transit goods*. Ikasikitisha zaidi Mheshimiwa Rais anasema kabisa ni bora aje mtalii mmoja lakini ali pe kodi, waje watalii wachache walipe kodi kuliko kuacha tusiweke hizi kodi ili watalii waje wengi. Mtalii akija alikuwa analipa hiyo kodi, akilala hotelini analipa na sehemu zingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tungekuwa tumewekeza kimkakati kwenye utalii kuhakikisha tunakuwa na angalau watalii hata milioni tatu, milioni nne ingesaidia kwani ni sekta pekee ambayo inatoa ajira nyngi, ni sekta pekee ambayo ingekuwa inaingiza fedha za kigeni. Leo Tanzania tuna vivutio vingi sana, tuna utalii wa fukwe, ukilinganisha hata na Afrika Kusini tu, wenzetu on average wana watalii zaidi ya milioni 15 sisi Watanzania eti milioni moja, halafu tunakaa hapa tunafikiri nchi yetu itaenda, tuna utalii wa kila aina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo ukienda Afrika Kusini pale Soweto utakuta watu wamepanga foleni kuangalia sehemu aliyoisha Baba wa Taifa Mandela lakini hapa kwetu ukienda Butiama ambayo ni makumbusho ya Baba wa Taifa utashangaa. Uwanja wa ndege wa Musoma tunesema mturekebishie ili watalii waweze kwenda pale watu wanaenda kujenga Chato, ndiyo vipaumbele! Yaani badala uboreshe Musoma, uboreshe na kwa Baba wa Taifa ili watalii waje wengi kwenye makumbusho unaenda kujenga Chato! Vipaumbele vya nchi hii, inasikitisha sana. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuweke mkakati wa kuhakikisha angalau tunapata watalii milioni tatu, milioni nne, Taifa letu litasonga mbele. Tuna vivutio vingi sana, eti vi-table mountain vya South Africa, sisi tuna milima mingi tu hapa, tuna fukwe nyngi. Leo Brazil fukwe zao wanazitumia vizuri sisi Watanzania tupo tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine, uwekezaji kwenye bahari kuu, wanasema Chenge report na vitu kama hivyo. Serikali ingeamua kujielekeza kutafuta wawekezaji kwenye uvuvi wa bahari kuu ingekuwa ni chanzo kingine kizuri tu ambacho kingeweza kutupatia mapato. Hii ina maana wale watu wavue wale samaki, tuwe tumejenga viwanda hapa hapa waweze ku-process hapa hapa itatoa ajira nyngi lakini pia tukisha-process na ku-pack tutasafirisha ina maana tutapata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yote hayaonekani kama ni chanzo, tunabaki kusubiria Watanzania wakamatwe kwa boda boda, matrafiki siku hizi

wanakaa kwenye magari wanasema kabisa sijui mnawa-promote, leo nimekusanya shilingi bilioni moja kutokana na makosa ya barabarani. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku hizi huko mikoani, walala hoi waendesa pikipiki wanakamatwa, Tarime mfano hata tumeona Mheshimiwa Lacairo wa Rarya analalamika, mtu amejiriwa na kapikipiki kake unamwandikia faini Sh. 90,000 atoe wapi wakati mwisho wa siku anatakiwa apeleke Sh.10,000 kwa tajiri wake, akishindwa pikipiki inachukuliwa na magari hivyo hivyo. Yaani sasa hivi Serikali hii ya Awamu ya Tano chanzo kikuu cha mapato ni kupitia makosa ya barabarani, aibu! Kama Taifa tuwekeze kwenye bahari, viwanda viwe vikubwa, kama nilivyosema vichakate hapa hapa, ajira zitapatikana tutasafirisha nje. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia kingine cha mwisho ni kilimo. Zaidi ya Watanzania 80% wamewekeza kwenye kilimo lakini kilimo chetu hakina tija kwa sababu hata vichocheo vya kuhakikisha kilimo kina *take over* vyenyewe bado viko hoi. Huwa tunaimba hapa kuboresha miundombinu ya usafirishaji, kwa sababu mimi nikilima niko kule kijijini lazima niwe na barabara ambayo itanisababishia lori kubwa lifike niweze kusafirisha mazao yangu kutoka point A kwenda point B, barabara ni mbovu, hazijatengenezwa kabisa. Tunaona lami tu za kwenye *highway*, mkatengeneze na huko ambako ndiko wakulima wako wengi ili waweze kusafirisha mazao yao kutoka vijijini kuja mijini. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kingine ni umeme. Kaka yangu hapa Profesa Muhongo alisema ame-invest kwa mwaka huu ni zaidi ya shilingi trilioni moja na bilioni mia ngapi kwamba tutaona umeme unawaka vijijini. Ni matarajio yangu kwamba tutaona umeme unawaka huko ili hao wakulima wanaolima waweze kusindika yale mazao yasiharibike, waweze kujenga viwanda vidogo vidogo kuviongezea thamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukiwa na umeme, tukiwa na miundombinu mizuri ya barabara, maji yakawa yanapatikana tutaweza kuona kweli tunasonga mbele vingineyo hatutaweza kuwa na mapato kabisa. Tutakuja hapa tunatoa bajeti, mapato ni hayo unaelekeza kwenye vinywaji, unaelekeza kwenye vikodi vya utalii kwa hiyo watalii hawaji mnakosa, tuwe na watu ambao wamesomea mambo haya waweze kuishauri Serikali na kuleta bajeti ambayo inaakisi uhalisia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, nimekuwa nawatetea sana hawa ndugu zangu wa Magereza. Naambiya Askari Magereza wanaidai Serikali kuanzia mwaka 2012/2013, 2013/2014, 2015/2016 ndiyo nimesikia sasa hivi

mmewapelekea ya 2015/2016 nataka kujua 2012/2013 na 2013/2014 ni lini mtaenda kuwalipa? Pia tuweze kujua fedha za kuweza kufidia yale maeneo ambayo mmechukua...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha  
kwa muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Bashe atafuatiwa na Mheshimiwa Salma Mwassa.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa. Kwanza nianze kuipongeza sana Kamati kwa kazi waliyoifanya ingawa taarifa yao ni ya quarter moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili nataka niishauri Serikali. Siyo dhambi kufanya evaluation ya kipindi cha miezi sita na kurudi kwenye drawing table ili kujipanga upya. Ujisoma taarifa ya Kamati, ujisoma Taarifa ya Hali ya Uchumi aliyoiwasilisha Mheshimiwa Waziri kwenye Bunge hili, ujisoma Taarifa ya BOT waliyoitaa Desemba inatuonesha kabisa tuna kila sababu ya Serikali kurudi kukaa chini kujitathmini na kupanga upya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe indication chache ambazo kwa upande mmoja Kamati wamezi-observe upande mwingine taarifa ya BOT waliyoitaa Desemba wamezionesha. Kwenye taarifa ya BOT na Waziri wa Fedha kwenye taarifa yake aliyoisoma juzi ndani ya Bunge hili, ujisoma kwenye taarifa aliyoisoma kwenye Bunge hili, item number (6) na (7) naomba ninukuu. Kwenye item number (6), Mheshimiwa Waziri anasema:-

“Kiashiria kingine cha jumla cha afya ya uchumi wa Taifa ni mfumuko wa bei ambaa unapima mabadiliko ya bei za bidhaa na huduma zinazotumiwa na kaya nchini. Mfumuko wa bei ulipungua kutoa 6.5 Januari mpaka 5.5 Juni 2016”.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda item number (7), Mheshimiwa Waziri anasema:-

“Kuna viashiria vinavyoonesha uwezekano wa kuongezeka kwa mfumuko wa bei kutokana na hali ya ukame uliojitokeza hapa Tanzania na Ukanda wa Afrika Mashariki na uwezekano wa kuongezeka kwa bei za mafuta katika soko la dunia”

Mheshimiwa Mwenyekiti, *item (6)* ni viashiria vya kuporomoka wakati *item (7)*, kuna uwezekano wa kupanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya Benki Kuu inasema, headline inflation *ime-grow* kutoka 0.1% kwenda 1.1% na *contributing factor* ni energy na fuel growth. Kwa hiyo, tafsiri yake ni nini? Ni kwamba kuanzia leo Januari mpaka tunapofika Julai hali ya mfumuko wa bei itakwenda juu. Maisha ya Watanzania yatakuwa magumu. Kwa hiyo, ni vizuri sasa Serikali ikachukua hatua ili ku-rescue situation inayotukabili huko mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini nasema hivi? Kwa sababu sehemu kubwa ya bajeti yetu tuliyopitisha, fedha za maendeleo tulitarajia kutoka nje ya nchi. Hali inavyoonesha *tume-attain less than 30%* na kuna uwezekano *development partner* wasitupatие hizi fedha. Tumekimbilia kwenda kukopa ndani ambako *tume-burst*, tumekwenda 132%. Tafsiri yake mzunguko wa fedha kwenye soko utashuka maisha yataendelea kuwa magumu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuongelea kushuka kwa shilingi. Mheshimiwa Waziri anatuonesha *confidence* na mimi nayasema haya kufuata maelekezo yako kwamba tujikite kwenye ripoti ya Kamati, najenga hoja zangu hizi za awali ili ripoti ya Kamati ambayo wamei-submit hapa iweze kutu-guide na Serikali ikubali kuna tatizo. Dola ya Kimarekani wameamua wao wenye kwenyeza kutoka 0.25% *interest* kwenda 0.5% na wana *project by December* itakwenda 0.75%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tafsiri yake ni kwamba madeni tuliyokopa kama nchi gharama yake itaongezeka. Serikali inasema deni linahimilika, Mheshimiwa Waziri umefika wakati sasa, ushauri wangu kwenye hili, tuanze kulitathmini deni letu sio kwa GDP tulitathmini deni letu kwa mapato yetu halisi *against revenue* kwa sababu tunalipa kwa kodi tunayoikusanya kutoka kwa Watanzania. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nchi, Kamati imesema na Serikali imesema kwamba tumekusanya vizuri kodi kutoka kwa Watanzania, tafsiri yake ni nini? Tumetoa fedha kwenye mifuko ya Watanzania, tumeipeleka Serikalini. Njia pekee ya kutatua hii changamoto ni fedha hizi zirudi kwa shughuli za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami niipongeze Serikali kusaini mkataba wa ujenzi wa reli ya katì na Waturuki wa kilometra 200. Naipongeza sana na nikitazama kwa bajeti ya 2016/2017 achievement zitaonekana kwenye *item*

ambazo hazigusi maisha ya Watanzania moja kwa moja, ndege tuta-attain na hilo ni jambo jema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawaelewa sana Wizara ya Fedha wanafanya jitihada ya katuondoa kwenye *consumption based economy* kwenda kwenye *investment based economy* lakini hatutakiwi ku-destroy fundamental pillars tulizozijenga, uchumi wetu muda mrefu umekuwa based on *consumption*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niishauri Serikali, tuna dhamira ya kwenda kwenye viwanda, angalieni takwimu zifuatazo. Ukituza taarifa ya Waziri na taarifa ya Kamati tunasema kwamba tumepezunguza *importation* lakini *importation* zipo tulizopunguza? *Capital goods imports* zimeshuka kwa 33%, *building and construction* zimeshuka kwa 29%, *machinery* zimeshuka kwa 36%, *fertilizers* zimeshuka kwa 24%, *transport equipment* zimeshuka kwa 32%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tafsiri yake ni nini? Ni kwamba uwekezaji kwenye viwanda haupo! Hakuna mtu anaenda kuwekeza! Kwa hiyo, Serikali sasa hivi inachotakiwa kukifanya na mkubali kwamba bajeti ya mwaka jana tuliyopitisha haikuwa *realistic!* (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri la kwanza na tulisema kwenye bajeti wakati tunachangia mwaka jana kwamba wakati umefika tuwe na *realistic budget* na *vipaumbele ambavyo* tunaweza ku-attain kwa muda mfupi. La pili, *financial institution*, Waziri amesema Benki zetu ziko imara, moja ya benki iliyopata hasara *quarter* ya pili ni *Tanzania Investment Bank*, ndiyo *ime-lead!* Imepata hasara ya 20 billion shillings lakini hoja tunayoisisikia sana kutoka Wizara ya Fedha ni kwamba provision zinazowekwa na benki za *non-performing loans* ni nyingi ndiyo maana wanapata hasara. Kunapokuwa na *NPL* nyingi sio *rocket science* ni kwa sababu wakopaji waliokopa wameshindwa kulipa! Kwa hiyo, wanacho-*provide* ni kwamba hazitakusanyika huko na kwa kuwa hazitakusanyika maana yake mabenki yatapata hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazama Benki yetu ya Kilimo ilikuwa ina 56 billion shillings, wamekopesha only 3.6 maana yake hakuna mikopo inaenda kwenye sekta ya kilimo. Sekta ya kilimo ndiyo uti wa mgongo wa kutuletea fedha zetu za nje pamoja na *tourism* lakini hali ya nchi inavyoonekana, sekta ya kilimo imeshuka kwa 0.5. Kitakachotokea mavuno ya 2016/2017 itashuka zaidi kwa sababu hatukutenga fedha kwa ajili ya pembejeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa perception ya Serikali sasa hivi kwamba uwekezaji kwenye pembejeo na researchers wamefanya uchunguzi duniani kwamba msipo-provide fedha nyngi kwenye kilimo kwa kuwekeza kwenye pembejeo ukuaji wa sekta ya kilimo utakuwa ni historia, hatuwezi! Kwa hiyo, ningiomba Serikali, Wizara ya Kilimo uwekezaji kwa ajili ya pembejeo kwenye bajeti ijayo ufanyike...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante kwa mchango wako.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naunga mkono ripoti ya Kamati. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Salma Mwassa atafuatiwa na Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Ezekiel Maige ajiandae.

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii lakini vilevile nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia afya njema na mimi niweze kuchangia ripoti hii ya Kamati hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nijielekeze kwenye ukusanyaji hafifu wa mapato. Kwa kiasi kikubwa kabisa ukiangalia kwenye taarifa hii ya Kamati imeonesha kwamba ukusanyaji hafifu wa mapato umeathiri bajeti kwa kiasi kikubwa. Tuangalie kwa mfano kodi ya majengo kwenda TRA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukusanyaji hafifu wa mapato kwanza unasababishwa kwa kiasi kikubwa na Serikali Kuu kuingilia hizi Halmashauri zetu au Serikali ya Mitaa hata kwenye vyano vyao wanavyovibuni na kuviona kwamba sasa vinakua badala ya kuwapa moyo zaidi na kuwasimamia katika sera wanavipora vile vyano kama kodi ya majengo na kuvipeleka Serikali Kuu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam, Kinondoni, Temeke, Ubungo zilikuwa zinafanya vizuri sana katika kodi hii ya majengo na ndiyo uti wa mgongo wa Halmashauri zetu lakini leo imepelekwa TRA hakuna hata mia iliyokusanya. Wakati mwaka jana ukiangalia takwimu kwa mfano Manispaa ya Kinondoni imekusanya zaidi ya shilingi bilioni tisa kwa mwaka na ilikuwa ina uwezo wa kukusanya zaidi ya shilingi milioni 800 mpaka shilingi bilioni moja kwa mwezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tuna miezi nane toka kodi hii ihame kutoka kwenye Halmashauri kwenda TRA, TRA haijaleta hata senti tano kwenye Halmashauri. Unategemea huo utekelezaji wa bajeti utafanyika kwa kiasi gani wakati Serikali Kuu ndiyo chanzo cha kuvuruga hizi kodi badala ya kuzisimamia. Miaka miwili tu iliyopita kodi hii ilikuwa kwenye Halmashauri na ilikuwa ina perform vizuri kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufupi, kodi hii ni kodi ya *local*, inatakiwa ikusanywe kule kwenye *local level* na sio kodi ya *central level* hii. Ukiipeleka kodi ya majengo kwenye *central level* unaharibu mpango mzima kwa sababu kodi hii inatakiwa ikusanywe kwenye mitaa. Kwa hiyo, napenda kuishauri Serikali ingeandaa mfumo mzuri kuzisimamia Halmashauri ili kwamba wale Wahasibu wa Halmashauri waende kwenye mitaa na zile mashine za *EFD* wakusanye ile kodi ya majengo kutoka kule kwenye *local level* sio kwenye *central level* huku kwenye TRA ambayo kwanza akienda tu pale mwananchi wa kawaida anaulizwa, una *TIN*, majina yako matatu, sijui mfumo wa nini, yaani TRA kwa kifupi haina uwezo mzuri wa kukusanya kodi ya majengo kama ilivyokuwa kwa Halmashauri, tume-prove failure kabisa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano sasa hivi ni miezi nane, miezi nane unajipanga vipi? Unajipanga mwezi wa kwanza, mwezi wa pili, wa tatu, mpaka miezi nane hujakusanya hata senti tano? Wakati Halmashauri yenyewe ilikuwa ina uwezo wa kukusanya kati ya shilingi milioni 800 mpaka shilingi bilioni moja kwa mwezi, wewe unajipanga nini? Wamechukua ma-valuer wa Halmashauri kuwapeleka TRA, wamechukua mifumo kutoka kwenye Halmashauri, majengo mengi kwa asilimia kubwa yamethaminiwa, kwa nini mpaka sasa hivi hawakusanyi, ina maana wameshindwa. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lisimamie hii kodi irudi tena kwenye Halmashauri. Halmashauri zinakufa! Hii kodi ndiyo uti wa mgongo wa Halmashauri, Halmashauri zime-paralyze kwa sasa, hazina chochote kutokana na kuwanyang'anya hii kodi yao na hiki ndiyo chanzo kikubwa cha mapato. OC zao kwa asilimia kubwa zilikuwa zinatoka kwenye kodi ya majengo. Kwa hiyo, naomba kabisa kwa miezi hii minane itoshe kutathmini kwamba TRA ni kama imefeli kukusanya kodi hii. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nijielekeze kwenye kukopa zaidi ndani. Naishauri Serikali kwamba, ni vizuri tukatoka sasa kwenye wigo huu wa kutegemea mikopo ya ndani na tukaangalia kujenga mahusiano zaidi nje. Kukopa zaidi ndani, tuwaachie hawa sekta binafsi, lakini sisi kama Serikali

tupunguze kukopa zaidi ndani, tukope nje ili tupate wigo wa kupata fedha za kigeni na kuja kuzisambaza ndani na uchumi uendelee kukua. Sisi kama Serikali ambao tuna uwezo wa kukopa nje kirahisi, tukiendelea kukopa ndani: Je, mwananchi mdogo atakakopa wapi? Kwa hiyo, tutaendelea kuudumaza uchumi wetu na hatutaweza kufikia lile lengo tulilojiwekea. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niende kwenye mada ya ukuaji wa uchumi kutokumfikia mwananchi wa kawaida. Kwenye ukurasa wa saba ripoti ya Kamati ime-quote kabisa, "pato la mwananchi wa kawaida bado ni dogo sana na asilimia kubwa ya wananchi wetu wanaishi kwa kipato cha chini ya dola moja za Kimarekani." Nimemsikia Mbunge mmoja hapa anakana kabisa, hivi kweli sisi tunaotegemewa na watoto, sijui na akina nani, hivi kweli tungekuwa tunaishi kwa dola moja tungeweza? Kwa hiyo, ina maana unapingana na ripoti ya Kamati? Sijamwelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaishi chini ya dola moja kwa siku kwa sababu tu, sisi kwa ujamaa tuliojengewa toka huko nyuma na Hayati Mwalimu Nyerere kwamba huyu mwingine akiwa hiki, tunasambaziana; lakini ni ukweli kabisa tunaishi chini ya dola. Usibishe! Mheshimiwa Mbunge wewe tu kwa sababu tu maisha yako yako vizuri, uko hapa, lakini wananchi huko nje wanateseka. Sasa sisi tunaona tu uchumi unakua, unakuaje? Mbona hatuoni kwenye maisha halisi ya Mtanzania kwamba uchumi unakua! Sasa hizi taarifa tunazoambiwa kwamba uchumi unakua, unakua wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokukua kwa uchumi kwenye *level* ya chini inasababishwa na Halmashauri zetu zinaposhindwa kusambaza ule utajiri chini ya wananchi wake kutokana na kuingiliwa, mara hivi; wakiendelea kukusanya vitu vyao, wanaingiliwa, mara hivi. Kwa sababu huwezi ukawa Serikali Kuu kule juu ukapata maisha ya Mtanzania halisi. Maisha ya Mtanzania halisi yanapatikana huku chini kwenye Halmashauri. Kwa hiyo, Halmashauri zipewe uwezo, zitungiwe sera. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kikubwa cha kufanya, Serikali Kuu isimamie sera za kwenye Halmashauri. Siyo kuona kama, sasa hivi Halmashauri zime-perform kwa kiasi kikubwa kwenye chanzo hiki, inapora. Badala ya kubuni vyanzo vyao, wao wanatafuta tu kwamba chanzo hiki ipore iende kupeleka Serikali Kuu. Hii siyo sahihi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nijielekeze kwenye hoja ya wahisani kutokuleta pesa kwa wakati. Kwanza tuijulize, kwa nini wahisani washindwe kupeleka pesa kwa wakati kipindi hiki? Kama Serikali tufanye tathmini kwa nini mpaka leo

wameleta tu asilimia 16 na wakati ilitakiwa walete 36? Kwa hiyo, tujulize ni nini hasa? Kama wao walikuwa marafiki zetu wa karibu tu, lakini leo hawana hata sababu na ripoti ya Kamati inasema, hata wao hawakuambiwa sababu ni nini. Yaani hawana sababu zinazokwamisha. Sasa kwa nini hamna sababu? Inawezekana sababu zimejificha huko kwa ndani, lakini hamzisemi. Nadhani tujitathmini upya. Je, tuna mazingira rafiki na wenzetu? Kwa sababu sisi tumejifungia hapa kisiwa. Hatusafiri kwenda ku-interact huko nje, wafanyakazi wa Serikali wamekuwa *blocked*, hawaendi huko nje. Sasa hao wahisani, huo urafiki tunaujenga wapi? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi kweli kwenda kuomba kwa mwenzako si lazima kwanza uende wakuone ndio uende kuomba! Unaomba ukiwa hapa, utaweza? Hawa wahisani tujenge mazingira mazuri kule, *internationally*. Sisi Wabunge tusafiri tuka-interact kule, ili tukienda kule kwa Wabunge wenzetu, tunawaambia jamani sisi bwana wenzenu twafa huku. Hivi na hivi tuambieni. Eeeh, sisi hatuna huku hivi na hivi! Mahusiano Kimataifa ni madogo. Serikali hii ya Awamu ya Tano ijitafakari upya, tutoke. Wabunge wenyewe hapa hatusafiri; sasa kama hatusafiri tutaendaje kuomba kwa wenzetu? Utaomba vipi wewe usaidiwe huku wakati huendi kule kwa mwenzako. (Kicheko/Makofi)

#### **MBUNGE MWINGINE:** Wanaomba kwa email!

**MHE. SALMA M. MWASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kwa hiyo, tuangalie tena kwa nini hii misaada imekuwa midogo? Tutoke tuanzie na Mheshimiwa Rais, atoke; sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tutoke, wafanyakazi wa Serikali watoke, wote; yaani isiwe ile kubana bana sijui kitu gani. Tutoke huko tukaombe! Sisi hatuwezi kujitegemea wenyewe hapa! Eeeh, tutoke, Mawaziri wenyewe watoke vilevile wakaangalie hata wenzao kule wanafanya nini kwenye Wizara zile. Tokeni hii misaada tuipate tena. Mbona mwanzoni huko ilikuwepo! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kweli Mheshimiwa Rais Kikwete, alikuwa anatoka sana. Mbona mambo yalikuwa sawa! Eeh, tutoke. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye mambo ya ukame kuhusu chakula. Nakumbuka kabisa kwenye ndani ya Bunge lako hili, kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walilalamika kwamba mazao ya chakula yanaiza, hapa hapa ndani ya Bunge hili. Sikumbuki ni kikao kipi lakini akiwemo Mheshimiwa Keissy alikuwa analalamika kabisa; mazao yanaiza, hayanunuliwi. (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii NFRA haipewi fedha za kutosha kununua chakula cha kuhifadhi na ndiyo maana leo Waziri wa Chakula anasema Halmashauri 55 zina upungufu wa chakula lakini hazina njaa; hivi hiyo si ni lugha tu! Yaani upungufu wa chakula na njaa, maana yake nini? Eti hazina njaa, lakini zina upungufu wa chakula. Sasa ndiyo nini? Mimi sijaelewa hapo, labda niombe kufafanuliwa zaidi. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kabisa Serikali, sasa hivi tuendelee kuambiana ukweli kwamba hii mamlaka hii tumeiunda wenyewe, ipewe hela za kutosha inunue. Kama mahindi yapo Kibaigwa, basi yapelekwe Songea, yasambazwe kwenye magodauni yao ya mikoa ili hili janga la ukame na njaa lionekane kama linaweza kuepukwa, tujikidhi kwa mahitaji ya chakula kilichopo. Kwa mfano, kama hivi matetemeko, ingeku... (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Haya! Huyo ndio Mheshimiwa Salma Mwassa. Tunaendelea, Mheshimiwa Richard Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba nichangie kuhusu taarifa ya Kamati ya Bajeti. Nakushukuru kwa nafasi hii, lakini nisingependa kurudiarudia yale ambayo yamesemwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba niipongeze sana Serikali kwa kweli kwa kazi nzuri lakini kwa nidhamu ya matumizi ya fedha inazokusanya. Nidhamu ya matumizi ya fedha kwa kweli imeongezeka sana. Kwa hiyo, naomba Serikali iendelee na utaratibu huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitajikita sana kama ulivyoshauri kwenye maoni na mapendekezo ya Kamati. Maoni ya Kamati hasa ukusanyaji wa ulipaji wa deni la TANESCO. Deni hili limekuwa likikua siku hadi siku. Mwaka 2014/2015 deni la TANESCO lilikuwa shilingi bilioni 186.4. Kwa mujibu wa taarifa ya Kamati, inasema deni hili sasa hadi Agosti, 2016 limefikia shilingi bilioni 794.9. Kutoka shilingi bilioni 186 kwenda shilingi bilioni 794. Kwa hiyo, limeongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukijipa mwaka mmoja mbele, usishangae likafikia shilingi trilioni moja, sasa ni kwa nini deni hili linakuwa siku hadi siku? Nani halipi deni hili la TANESCO? Ni kwa nini halipi? Kama ni Taasisi za Serikali, nina uhakika zinapata kasma ya kulipa umeme. Taasisi hizi; watu binafsi na mashirika

ya umma, kwa nini hawaiiipi TANESCO pesa zake ambapo yenewe inatoa huduma ya umeme? Ni lazima ilipwe, kwa sababu ni azimio.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba Serikali kupitia Bunge lako, deni hili ni kubwa; ndio maana TANESCO kwa sababu ya madeni makubwa inatumia nguvu nyingi lakini hailipwi na ndio maana wanafika mahali TANESCO wanataka kupandisha bei ya umeme. Inawezekana sababu mojawapo ni hii. Kama hili deni la shilingi bilioni 794 lingelipwa hata robo tatu, nina uhakika TANESCO ingeweza kuijendesha. Vinginevyo, TANESCO itakufa, itashindwa kufanya kazi yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia viwanda, kama hatuna umeme wa uhakika na wenzangu wamesema kwamba umeme unakatikakatika, lakini kama TANESCO haipewi fedha zake, viwanda hivi vitakufa kwa sababu hakuna umeme wa kutosha. Naomba sana Serikali iangalie na tulishauri mwaka 2014 - 2016 kwenye taarifa ya nishati na madini, wakati deni lilikuwa shilingi bilioni 186, lakini nashangaa kwa nini Serikali haitaki kulipa deni hili, mpaka limefikia shilingi bilioni 794. Naomba sana Serikali deni hili lilipwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati tunahitimisha hapa, mhusika mwenye taarifa hii alisema, hasa kuhusu deni la TANESCO, shilingi bilioni 794 lazima lilipwe vinginevyo TANESCO itakufa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, tulipitisha vizuri kabisa hapa, sheria nzuri kuhusu gesi na mafuta. Sheria ile tukakubaliana kwamba kwa sababu tumepitisha sheria hii, ambayo na kwenye mapendekezo ya Kamati imo, kwamba kukamilisha kwa kanuni ya sheria ya kusimamia, mapato ya mafuta na gesi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa tulipitisha mwaka juzi, 2015 nami nilikuwa Mwenyekiti, tukapitisha hapa, tukategemea kwamba Serikali sasa, kwa mfano mwaka jana, 2016 kanuni hizo zingekuwa zimeshakamilika. Mpaka leo kanuni hizo hazijatekelezwa. Hivi tatizo hasa ni nini? Hizi shughuli za gesi na mafuta zinafanyikaje kama kanuni hazipo? Naishauri Serikali itekeleze agizo la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekubaliana na Kamati imesisitiza, sijui Serikali inapata kigugumizi kwenye eneo gani? Kwa sababu tunategemea umeme wetu kupitia maji kwa maana ya hydro, gesi; lakini tukasema twende mbali zaidi, kwenye umeme wa joto ardhi (geothermal), tutoke hapo twende kwenye solar power.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukitazama, tumekubaliana humu humu kwenye Bunge suala la umeme wa upemo pale Singida; sasa nauliza, hivi tatizo hasa ni nini? Tukitegemea chanzo kimoja au vyanzo viwili; hydro pamoja na gesi, lakini tunataka tusonge mbele zaidi umeme wetu huu tuuze nje, tupate pesa nydingi za kigeni, lakini tuweze kujitosheleza kwenye umeme wetu wa ndani hasa tunapotaka kwenda kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viwanda hivi tunavyovisemea, bila kuwa na umeme wa uhakika wa bei nafuu usiokatikakatika, hatuwezi kufika. Itakuwa ni hadithi tu! Ni lazima tujitosheleze na umeme wa kwetu kwa sababu tuna vyanzo vingi, Mungu ametujalia, vyanzo vingi tunavyo isipokuwa ni kuvisimamia na kuvitekeleza. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kama tumekubaliana jambo fulani litekelezwe, kwenye eneo fulani, hivi tunashindwa nini kulitekeleza? Leo tuambiane, kwenye geothermal timesikia asilimia ngapi? Tukubaliane kwenye umeme wa juu, asilimia ngapi? Tutoke hapo twende kwenye umeme wa upemo, asilimia ngapi? Ukitoka hapo, kule Liganga na Mchuchuma ni maneno tu, yanasemwa kila siku; Liganga, Mchuchuma; Liganga, Mchuchuma; hata tutakapokuja tena kesho kutwa, Liganga, Mchuchuma! Ni history tu! Tufike mahali tuseme hili linawezekana, tunaliacha. Nafikiri hata huku kwenye taarifa ya Kamati, limesemwa hili la Liganga na Mchuchuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe umekuwa muda mrefu huku ndani, inawezekana tangu umeanza U-AG Liganga Mchuchuma umeisikia, lakini imefikia wapi? Sijui kuna mgonjwa gani huku anayezua kila siku! Liganga Mchuchuma kila siku, lakini kama kweli tungeamua tukawekeza pale Liganga Mchuchuma, tungepata umeme wa uhakika, tungepunguza matatizo. Ukiwa na vyanzo vizuri vya umeme nina uhakika hata bei ya umeme itashuka. Ukiwa na vyanzo vingi vya umeme, utauza nje ya umeme wako huu, utapata fedha za kigeni, lakini ni mizunguko tu, tunazunguka lakini hatufiki. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema mambo matatu haya, kukamilishwa kwa kanuni na sheria za kusimamia mapato ya mafuta na gesi, lakini kuilipa TANESCO deni lake, shilingi bilioni 790, pia kukamilisha kwa miradi mbalimbali ya vyanzo vya umeme, tufike mahali tumalize tuhamie kitu kingine. Mengine najua yamesemwa sana, sitaki kurudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo yangu kuhusu taarifa hii, ni hayo. Nashukuru sana. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Richard Ndassa kwa mchango wako. Tunaendelea na Mheshimiwa Ezekiel Maige, atafuatiwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na Mheshimiwa Frank Mwakajoka ajiandae. Mheshimiwa Maige hayupo, haya tunaendelea. Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami nashukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza niwapongeze Kamati ya Bajeti kwa ripoti yao nzuri na kwa kweli vitu vingi wamevielezea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongea machache. Moja, ni deni la Taifa. Naamini, nilisema wakati wa bajeti na leo naomba nirudie tena. Kama kuna eneo ambalo tusipolisimamia vizuri juhudii kubwa zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, hatutaziona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila unapoongelea deni la Taifa, tunaambiya deni letu ni himiliyu (*sustainable*) kulingana na viwango vya Benki ya Dunia na IMF. Naomba tufikiri tofauti kidogo. Deni hili tunatumia GDP kujua kama deni la Taifa linahimilika. GDP ni sawa, ndiyo mali zote tulizonazo, zinajumlishwa, halafu unaangalia percentage ya deni ulilonalo. Unapoanza kulipa deni, hutumii ile GDP sasa, unalipa deni kutoka kwenye mapato yako. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unakusanya kila mwezi ukishakusanya, *first charge mshahara*, *first charge*, deni la Taifa. Wizara ya Fedha watatuambia, tumefika sasa tunakusanya makusanyo; asilimia 86 ya makusanyo yanaenda kwenye mshahara na deni la Taifa. Maana yake ni nini? Hatutapeleka hela kwenye maendeleo. Kwa hiyo, lazima tubadilike; tunapotaka kuliangalia deni letu, tuli-peg na revenue base yetu. Tukifanya hivyo, tutaweza kwenda huko tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kwenye deni la Taifa, tumeshafika hapa. Hilo la kubadilisha namna ya ku-calculate, tuamue sasa kama Serikali, tutumie revenue ratio ili tuweze kujua tunaweza ku-manage deni la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo litaleta shida, mikopo yote ambayo tumeichukua, hasa ile ya kwenye mabenki, kuna kitu kinaitwa *floating libor*, wakubwa wanaenda kukopa kwenye mabenki wanatuambia chukua *floating libor* kwa sababu kwa hii inaweza *interest zikashuka* ama *zikapanda*; lakini *trend* imekuwa, ni *interest zinapanda*. Kwa sababu huwezi ku-control wewe. Ikishakuwa *floating libor* huwezi ku-control wewe, mwezi kesho unalipa nini kwenye *interest rate*? Anaye-control ni bwana mkubwa Marekani. Reserve Bank ya Marekani mwaka 2016 imeongeza kutoka 0.25% to 5%. Maana yake

nini? Interest zetu nazo zikapanda. So we are here tumekaa, tunasubiri *the mercy* ya wengine. Lazima twende kama wanavyofanya wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti nilisema nikajiwa hapa, kwamba unachosema sawa, lakini nahitaji a complicated work force. Hii complicated ya wapi? Duniani wanafanya, kuna kitu kinaitwa swap *interest rate*. Ukitanya swap, utalipa kingi mwezi wa kwanza, baada ya pale, *interest* yako unayoilipa inakuwa ni constant kila mwezi. Kwa hiyo, kama Taifa, utakuwa unajua kila mwezi ni shilingi ngapi nalipa kwenye deni la Taifa. Leo hii tukimwuliza Waziri wa Fedha, mwezi kesho atalipa shilingi ngapi kwenye deni la Taifa, hajui kwa sababu sio yeye anaye-control. Ni uchumi mwingine ndiyo una-control kwa sababu tu tumekwenda kwenye *floating libor*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unajua kinachotokea? Wanakuja wale wenye mabenki wanakwambia ukienda kwenye *floating libor interest rate* mwezi wa kwanza utalipa 0.1% au 1.3%, lakini ukienda kwenye fixed anakwambia itakuwa ni 1.75%. Kwa hiyo, wewe as a country una-save kwenda kwenye 1.3%! Uliza mwezi wa Pili, mwezi wa Tatu au mwezi wa Nne inakuwaje? Unakwenda kila mwezi unaongezeka, utatoka 1.3% mpaka 5%, lakini yule aliyelipa 1.75% ataendelea kulipa hiyo mpaka mwisho wa hilo deni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya tunayoyasema wenzetu wamefanya, sisi sio wa kwanza. Nawaombeni sana watu wa Wizara ya Fedha, tufike sehemu tufikiri tofauti kidogo. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ni suala la *investment model* ya growth ya economy yetu. Naomba sana Serikali, tusirudi tulikotoka miaka ya nyuma. Nawaombeni sana. Wenzetu wote wanakwenda kwenye *private sector* ndiyo engine ya growth. Tukidhani Serikali hii inaweza ikafanya kila jambo, nawaambia hatutafanikiwa. Mwalimu Nyerere alifanya hapa, alijenga kila kiwanda, leo viko wapi vyote? Kwa sababu, mambo haya ya viwanda, mambo haya ya *investment*, lazima uingize hela kila wakati. Siyo kila wakati utapata faida! Kitakachotokea leo utapata hasara, kesho unafanyaje? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi zilizoendelea hivi karibuni baada ya miaka ya 60, nchi kama Malaysia wanatumia hela za watu kufanya uwekezaji. Wewe unachotaka kama nchi, unataka huduma. Nchi inataka umeme megawati 5,000; kuna mtu anaweza akaleta fedha zake akaweka umeme, shida yetu ni nini kumpa? Ni lazima kila kitu kifanywe na TANESCO? Mtu anataka kujenga barabara kutoka Dar es Salaam; Swiss Dual Carriage, mpaka Dodoma, aweke road toll, sisi hatutaki. Maana yake ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea habari ya PPP, tumeweka Sheria, lakini soma Ripoti za Wizara ya Fedha; kama kuna jambo hawana *interest* ni suala la private sector. *Private Sector* ni wezi hawa. Naomba sana tubadilishe mentality ili twende kwa kasi. Kwa kasi ya Rais Magufuli, tukimsaidia tukaanzisha miradi ya private sector tutaenda kwa kasi sana ya maendeleo. Naomba sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa bajeti tulisema kuhusu bei ya mafuta. Niliwaambia jamani eeh, bei ya mafuta duniani inapanda na wenzetu wanahedge na hata Kenya wame-hedge, kwa nini sisi hatu-hedge? Watu ni kama vile tunaongea, tunayaacha hapo hapo. Ilikuwa wakati ule ni dola 44 per barrel, leo inakaribia dola 60 per barrel, tuko hapa hapa! *We are at their mercy*, tumekaa tunasubiri tu. Kwa hiyo, inaweza ikapanda mpaka ikafika 100, wakishakuja wanakwambia, unajua viashiria vya mwaka huu, bei ya mafuta duniani inapanda; lakini inapanda ukiwa unaangalia. Naomba watu wa sera wa Wizara ya Fedha mtusaidie. Vitu hivi wenzetu wanafanya, haiwezekani sisi tusifanye. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie kilimo. Naomba sana, kilimo chetu tumelima namna hii miaka 50, karibia 60 ya uhuru tunaendelea kulima namna hii. Mvua ikitetereka kidogo tunaanza kupiga kelele. Ni kwa sababu hatu-embrace *commercial farming*. Naomba tu-embrace *commercial farming*, ndiyo itakayotutoa hapa kwenda mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano rahisi wa *commercial farming* ndugu zangu, twende Zimbabwe. Bwana mkubwa yule wa Zimbabwe aliamua akafukuza wale Wazungu kwa sababu ya uzalendo wa ardhi, leo wanakufa njaa. Maana yake nini? Kilimo kinahitaji uwekezaji mkubwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeongea habari ya pembejeo hapa, mwaka huu pembejeo hakuna. Tumetoka shilingi bilioni karibu 80, mwaka huu tumeweka shilingi ngapi za pembejeo? Tunatarajia kupata nini? (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tuweze kutoka hapa, ni lazima tuone namna bora tuwe na mashamba haya ya akina mama yake na Peter, ambayo wanalima miaka yote hawajawahi kujitosheleza, lakini tuwe na mashamba ya mabwana wakubwa wenge fedha ambao watajitatutia wagani wao, watanunua pembejeo za kwao, wataweka umwagiliaji, watatafuta mbegu bora, hawatasubiri Serikali. Hapo kama Taifa, tutatoka hapo tulipo, tufike tunapokwenda. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea habari ya viwanda, tunaingiza mifuko ya jamii kwenye viwanda. Tuwe waangalifu sana. Tukizubaa mifuko hii tutaiptoteza. Nilidhani mifuko iingie kama kuweka mtaji, shughuli ifanyewe na wengine, lakini mkitaka waingie wafanye wenyewe, nawaambieni wataanza ku-provide losses hapa, tutashangaa baada ya miaka michache ijayo. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, duniani kote hawafanyi. Wanachofanya, wanaingiza kwenye *investment program*. Kama llovo anaweza akalima shamba, ana uwezo wa kutengeneza sukari, unanunua mtaji, unaweka hela kule kwa sababu yeye ana ile experience. Tukiamua kufanya wenyewe, muwe na hakika tutakuja kuulizana hapa siku moja. Tuko tayari kuzibeba losses hizo? Kwa sababu, biashara ina faida na losses. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ni mabenki yetu. Nawaomba sana, suala hili la *Financial Sector* tuwe waangalifu sana. Quarter ya pili, karibu benki 15 zime-provide losses. Majibu tunayopewa inawezekana ni majibu sahihi, lakini twende mbali zaidi tuijilize: Je, ni sahihi kwa uchumi wetu? Money supply kwenye market imepungua. Mwaka jana 2016 ni 4.6% wakati mwaka uliopita 2015 money supply ilikuwa almost 14.6%. Maana yake ni nini? Hela imetoka kwenye money supply. Kwa hiyo, hii ni shida. Lazima uchumi uende unaongeza, unatoa, unapunguza, then ndiyo tuta-stabilise.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua wanafanya kazi nzuri sana. Kamati imetuletea mapendelekezo mazuri sana; ni matarajio yangu kwamba mapendelekezo haya Serikali itaenda kuyafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalize kwa kusema, nawaombeni watu wa Hazina twendeni tukafanye *analysis proper* kuhusu deni la Taifa. Tusiposimamia deni hili, muwe na hakika mtakusanya kwa juhudu kubwa, hela yote inakuja inakwenda kulipa deni, maana kulipa ni lazima. Tunasema tunaenda kwenye miundombinu, tumekopa madeni haya yanakwenda kwenye miundombinu, sawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umeme, bandari, baadhi ya barabara, naomba tuweke *private sector* wafanye. Hata viwanja vya ndege. *Private Sector* ndiyo inayoleta biashara. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana watu wa Wizara ya Fedha, ni dhambi sana kujivunia kufunga biashara. Serikali serious, huwezi kusimama unasema nafurahi biashara zaidi ya 2000 zimefungwa. Hili siyo jambo la kusema. Tafadhalini sana wenzangu! Kama kweli Serikali you are serious, Waziri wa Fedha

unasema mwaka 2016 tumefunga biashara 2000 ni jambo la kujisifia, hili siyo jambo la kujisifia hata kidogo, tunyamaze. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shughuli ya Serikali, shughuli ya Watu wa Wizara ya Fedha ni kusaidia biashara zianzishwe nyingi zaidi kwa sababu, biashara zikianzishwa nyingi zaidi maana yake ni ajira, maana yake kodi itaongezeka, maana yake maisha ya watu yataboreka. Kama kweli, mnataka tukae hapa tunasema wale tumewafungia maana walikuwa wanakwepa kodi, mtu wa kodi unamwita, una-negotiate naye unamwambia bwana wewe nakudai. Sasa nitakukata mwakani. Mna-negotiate! Ndio kazi ya taxation! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naombeni watu wa tax, kazi ya kukusanya kodi ni sayansi *of its own*. Haiwezi kuwa kazi yetu ni kufunga biashara, ni kuwashtaki, hapana! Ukifunga biashara zote, kitakachotokea ni nini? Wewe utapata kodi? (Makofi)

**WABUNGE FULANI:** Hupati!

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Hatutapata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mapendekezo yaliyoletwa na Kamati ya Bajeti. (Makofi)

**MBUNGE FULANI:** Ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Serukamba kwa mchango wako mzuri. Ndiyo hayo yanayopaswa kusemwa. Sasa tunaelekea mwishoni, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Napenda kukushukuru kwanza kwa kunipa nafasi hii, lakini pia naishukuru sana Kamati kwa maoni yake ambayo wamejaribu kutoa na ushauri mbalimbali walioutoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba, siku zote nikisimama nikiwa nachangia hasa kuhusiana na mambo ya bajeti au na masuala ya fedha, najaribu kuzungumza sana kuhusiana na siasa kuondoka kwenye masuala ya kiutendaji. Masuala ya kiutendaji yakiingiliwa sana na siasa kama tunavyofanya sasa hivi katika nchi hii, lazima tukubaliane kabisa kwamba hatutaweza kufanya vizuri na tusitegemee kabisa kama Taifa hili litabadilika kama wataalam wetu ambao tumewasomesha kwa gharama kubwa na tumewapa majukumu

wanashindwa kutekeleza wajibu wao, wanashindwa kuishauri Serikali kitaalam na sisi tunatoa maagizo kuhakikisha kwamba Serikali inatekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia na nimejaribu kupima bajeti yetu ya mwaka 2016/2017 na ushauri mbalimbali ambao umetolewa na Kamati. Ukijaribu kuangalia utaona kabisa kwamba sisi wakati tuko Bungeni humu tunatengeneza bajeti hii, sisi kama Upinzani tulitoa Bajeti Elekezi, ili kidogo vitu ambavyo viko mle viweze kuchukuliwa kama msaada wa kusaidia bajeti hii. Kilichotokea, tulionekana watu wa hovyo, tulibezwa humu ndani na baadaye ilionekana kwamba hata bajeti yetu isingeweza kusomwa na watu hawakuipitia kuangalia nini ambacho kinaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana wenzetu ambao walikuwemo humu wanapitisha hii bajeti, leo wanalamika na wao. Nami nashangaa, hata wewe Mheshimiwa Mapunda! Hata wewe fulani! Nashangaa sana, yaani wanalamika wakati bajeti walipitisha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema tu kwamba uko upungufu mwingi sana ambao tuliukataa na tulishauri humu ndani. Tulianza na suala la VAT, tukajaribu kueleza hali halisi kwamba ndugu zangu mkiweka VAT kwenye masuala ya utalii mtapunguza pato la Taifa kwenye Idara ya Utalii. Tukawaambia ondoeni, angalieni wenzenu Kenya na Mataifa mengine yanafanya hivyo. Watu mkabeza mkasema haiwezekani, tunaweka sisi. Leo hii kila mmoja anashangaa humu ndani utafikiri hakuwemo Bungeni wakati wanapitisha bajeti hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme tu kwamba, sisi Wabunge tumepewa dhamana na wananchi kwa ajili ya kuishauri Serikali na kuisimamia Serikali. Kwa hiyo, wajibu wetu ni lazima tuutekeleze tukiwa ndani ya Bunge hili. Tukiendelea kuendekeza siasa ndani ya Bunge hili ni lazima tufike mahali ambapo tutaendelea kushindwa na kufeli na kila siku tutakuwa tunashtuka humu utafikiri hatukupitisha na kujadili sisi wenyewe. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka kusema, tunachotaka kushauri hapa ni kwamba, ni lazima turudi kwenye misingi. Lazima Serikali ikubali kushauriwa na kama Serikali haitakubali kushauriwa, itaendelea kufunga masikio na kuendelea kuona Wabunge wanachozungumza ni hamna! Mheshimiwa Magufuli, kama Rais wetu, ni lazima akubaliane na sisi kwamba, sisi kama Wabunge tuliopewa majukumu haya, ni lazima akubali ushauri wa Wabunge. Sisi ndio tunaoishauri Serikali na kuisimamia Serikali, kwa hiyo, akubali ushauri wetu. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tulizungumza sana kuhusiana na hali halisi ya watumishi kukusanya mapato kwenye Halmashauri zetu. Leo Halmashauri zetu kwenye nchi hii, zote ambazo zilipelekwa kwenye majaribio, ziko chini ya 24% kwenye nchi hii katika makusanyo yake. Ni kwa sababu, watumishi waliokwenda kukusanya yale mapato wameshindwa kufikia malengo kwa sababu, watumishi ni wachache katika Halmashauri yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Serikali tunazungumza hapa tunasema kwamba, makusanyo yanakwenda vizuri. Nataka kusema tu kwamba, fedha ambazo zimekusanya wa kwenye Halmashauri zetu ziko chini kabisa. Sasa Serikali sijui kama nayo itachukua nafasi ya kuweza kufidia fedha ambazo tumeshindwa kukusanya kwenye Halmashauri zetu. Sielewi kama zitafidiwa fedha hizo. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia kwenye Taarifa ya Kamati hapa, ukisoma kwenye ukurasa wa 26 kwenye kipengele cha 2.52 - Matumizi ya Serikali. Ukiangalia, utaona kabisa katika quarter ya kwanza katika Halmashauri, fedha kwenye Halmashauri zetu haikupelekwa hata shilingi kwenye upande wa utawala. Kwa hiyo, fedha ambazo zinatumika sasa hivi kwa ajili ya kuendeshea shughuli za utawala kwenye Halmashauri zetu, zinatumika fedha za vyanzo vya ndani, kitu ambacho kinarudisha utendaji kazi wa Halmashauri zetu. Nasi kama Halmashauri, tunashindwa kutekeleza majukumu ya wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninachotaka kusema ni kwamba, ni lazima tukubaliane tukiwa tunatengeneza bajeti hii tujue kwamba ni bajeti ya Serikali, siyo bajeti ya vyama vya siasa. Kwa hiyo, lazima tunapoingia kwenye bajeti hizi, tukae tukubaliane, tusikilizane, tupokee ushauri wa kila mmoja wetu ili kujenga nchi hii. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa najaribu kuangalia shughuli mbalimbali ambazo zimefanyika na mambo ambayo yameshindwa kufanyika katika bajeti hii. Ukijaribu kuangalia katika hali halisi, Serikali yoyote duniani ina wajibu wa kuwajengea wafanyabiashara wadogo wadogo na wafanyabisahara wakubwa mazingira ya kufanya biashara ili wafanyabiashara wakubwa waweze kupata mitaji mikubwa ili waweze kulipa kodi ya nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali yoyote makini inaendesha Serikali yake kwa kutumia kodi. Leo hii Watanzania wengi katika nchi hii wameshindwa kufanya biashara kwa sababu ya masharti magumu ambayo Serikali imeyaweka. Pia, Serikali hii haichukui hata jukumu la kuwaelimisha walipakodi wa nchi hii, ni nini ambacho kinalipwa katika Serikali hii. Wananchi hawaelewi;

Watanzania hawajui! Watanzania wanajiuliza, kinacholipwa ni mtaji? Ni faida au ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Watanzania sasa hivi wanaviziwa, wanapangiwa fedha ambayo haiwezekani, wengine wanafunga maduka, wengine wanaacha biashara zao, wanahamisha biashara zao, Serikali haichukui jukumu la kuwafundisha na kuwaeleza wananchi nini ambacho kinatakiwa kilipwe kama kodi ya Taifa hili. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba inawaelimisha wananchi nini ambacho kinalipwa ili wananchi walipe kodi na Serikali iweze kupata fedha, lakini Serikali haina muda huo. Ni lazima tukubaliane, kama wananchi wataendelea kuwa maskini, biashara zao zitaendelea kufungwa na Serikali hii. Maduka sasa hivi tunahesabu. Ukienda Dar es Salaam wanakwambia maduka 300 yamefungwa; ukienda Mwanza wanasema maduka 200 yamefungwa; ukienda Mbeya wanasema maduka 300 yamefungwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inasema inatekeleza wajibu wake wakati watu wanaendelea kufunga maduka na uchumi unazidi kushuka katika nchi hii. Kwa hiyo, ninachotaka kusema, ni lazima Serikali ijikite kabisa kuwaelimisha wananchi na kuweka ustawi wa biashara zao ili wafanyabiashara wafanye biashara, mitaji ikue na waweze kuwa walipa kodi katika Taifa hili. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna jambo lingine la mikopo. Wanafunzi wamepewa mikopo mwaka 2016, lakini kitu cha kushangaza, sasa hivi ukienda mashulenji, ukienda UDOM hapa sasa hivi kuna wanafunzi ambao wameambiwa hawana sifa tena za kukopeshwa. Tunataka Serikali itupe ufanuzi; kama mtoto alipata mkopo awamu ya kwanza, leo hii wanasema kwamba hana sifa ya kupata mkopo, tafsiri yake ni nini? Serikali haina fedha? Au nini kilichotokea?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi sasa hivi hawalewi kinachoendelea. Watoto wao wanapata shida, hawalewi nini kitakachotokea hapo mbele ya safari. Kwa hiyo, tunataka tupate majibu; kama Serikali haina fedha, iseme kwa wananchi kwamba Serikali haina fedha ili wazazi wa wototo hawa waangalie ni namna gani watahanganya na watoto wao kuliko kuanza kuwahangaisha watoto ambao wameshalipiwa mkopo kwa Awamu ya Kwanza na leo hii wanaambiwa kwamba hizo fedha hazipo na watoto hawana sifa za kuweza kupewa tena mikopo. Ni jambo la kushangaza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la kilimo. Wakati tunapitisha bajeti hapa, tulishangaa sana. Huko nyuma tulikuwa tunasema wakulima wanapata pembejeo kidogo, Serikali iongeze bajeti, lakini mwaka 2016 hapa wakati tunatengeneza bajeti, tulishangaa Serikali inaondoa shilingi bilioni 47 kwenye ruzuku ya Serikali kwa ajili ya wakulima, tukashangaa. Serikali hii inajinafasi kwamba inataka kuwa ni Serikali ya viwanda, huku inaondoa shilingi bilioni 47 kwenye bajeti. Leo hii mnashangaa kwa nini kuna 0.5 ambayo imeshuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnashangaa kitu gani wakati mliondoa...  
(Makofij)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Sasa muda unagombewa kama mpira wa kona. Tuna Mheshimiwa Kubenea, Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, Mheshimiwa Kaboyoka na Mheshimiwa Mgumba. Mheshimiwa Kubenea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Kubenea ameniachia muda wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kuniruhusu...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Komu!

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mmepatiana muda! Mimi sijakutambua, lakini basi endelea Mheshimiwa. (Kicheko/Makofij)

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.  
(Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nichangie. Kwanza nawashukuru sana na nawapongeza sana Kamati kwa kazi nzuri ambayo wamefanya kwa sababu, kwa kweli, wamezungumza kitu kile ambacho kinapaswa kuzungumzwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wengi wameshazungumza kuhusiana na deni la Taifa. Naomba niweke mstari tu kwamba sisi kama Bunge fusiposimama

kwenye nafasi yetu na kuiambia Serikali kinachopaswa kufanyika, tunaweza tukajikuta tuko kwenye hatari kubwa na tukawa mufilisi; tukawa hatuwezi kukopesheka na tukawa vile vile hatuwezi kuhudumia Watanzania ambao tunapaswa kuwahudumia. Hii ni kwa sababu ukiangalia kwenye maandiko ya Kamati inaonesha kwamba deni linakua kwa asilimia 18. Hili ni jambo la hatari.

Mheshimwa Mwenyekiti, wakati deni hili linakua, kuna mambo ambayo yanafanya na Serikali ambayo yangeweza kufanywa kwa namna nyingine ambayo ingeweza ikawa na tija zaidi kwa Serikali. Kwa mfano, tumenunua ndege kwa pesa taslimu; ule ni mradi wa kibashara ambao ungeweza ukaachwa ukakopa wenyewe, ukajiendesha wenyewe, uka-service hiyo riba wenyewe; lakini tumeenda kununua cash.

Mheshimwa Mwenyekiti, lakini wakati huo huo tunakopa, tena tunakopa ndani kwa kiwango ambacho ni kinyume hata na kiwango kilichoidhinishwa na Bunge hili. Maana yake ukiangalia huku, tumekopa tukazidisha asilimia 32. Naomba sana Bunge hili lisimame mahali pake liiambie Serikali iache tabia za aina hiyo, kwa sababu inakwenda kutuingiza kwenye hatari ambayo itakuja kuwa tatizo kubwa sana. (Makofii)

Mheshimwa Mwenyekiti, kutokupeleka fedha kwa wakati kwa miradi mbalimbali, hili ni jambo lingine ambalo linaonekana kama ni rahisi tu; lakini ukweli ni kwamba usipopeleka fedha kwenye mradi kwa kadri ilivyoelekezwa, maana yake unalipa watumishi wengi bila kazi yoyote. Unakuta watu wapo kwenye Serikali, mashirika mbalimbali na Halmashauri, hawana kazi ya kufanya, lakini mwisho wa mwezi lazima walipwe mishahara. Sasa tukiendelea na tabia hii, tunakwenda kwenye jambo ambalo ni tatizo kubwa sana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye kuchelewa kupeleka fedha au kushindwa kupeleka fedha maana yake ni nini? Miradi ile ambayo ilikusudiwa, ghamama zake za kuitekeleza zinaongezeka na mahali pengine inaleta migogoro. Unakuta mahali ambapo kulipaswa kufanyiwe fidia ya labda shilingi bilioni 10, unaambiwa sasa ni shilingi bilioni 20 na hiyo ghamama kwa vyovyyote inabebwa na Serikali na kodi za wananchi. Kwa hiyo, tunaendelea kuweka mzigo mkubwa zaidi kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa nilizungumzie, ni kuwa na mipango mingi ambayo kimsingi haitekelezeki. Kwa mfano huku, unaona mahali ambapo Kamati imebainisha kwamba miradi ambayo inapaswa kutekelezeka; kwa mfano, mradi wa makaa ya mawe Mchuchuma na Liganga, hili ni jambo ambalo lipo kila siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba jambo hili pamoja na kwamba wamesema linaweza likatekelezwa robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha. Jambo hili halitawezekana kwa sababu mpaka sasa hivi fidia peke yake ya kuwahamisha wale wananchi ambao wanapaswa wapishe mradi huu haijafanyika. Kama haijafanyika, ukiangalia urasimu unaotakiwa kwa vyovyyote haitawezekana kukamilisha hilo zoezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba tunakuwa na vitu vingi ambavyo hatuwezi kuvitekeleza. Tunashindwa kuwa na vipaumbele. Kwa hiyo, nashauri kwamba tuwe na vipaumbele vichache ambavyo tuna uwezo navyo na hivyo vipaumbele, kwa sababu Serikali ilishasema kwamba mradi huu ni wa kimkakati, maana yake ingekuwa ni jambo la busara sana kama Serikali ingeelekeza nguvu zake zote kwenye haya mambo machache ambayo yana *input* kubwa kwenye uchumi wetu ili yakifanyika, tuweze kupiga hatua haraka na tukaendelea kweli kama ambavyo inaelezwa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea na hadithi hizi za kwenye makaratasi za kueleza kwamba hili litafanyika halafu, yaani kama *bluffing* tu, kwamba "funika kombe mwanaharamu apite," yaani tunaliambia Bunge kwamba jambo hili litatekelezeka, lakini ukweli ni kwamba inaendelea kuwa hadithi. Nimemsikia Mheshimiwa Ndassa akisema, kwa sababu Mheshimiwa Ndassa ni mtu senior sana kwenye hili Bunge, kwa maana ya kukaa muda mrefu kwenye hili Bunge; akisema hiyo hadithi, kwamba toka ameingia Bungeni na labda ataondoka Bungeni, huo wimbo umekuwepo wa Mchuchuma na Liganga. (Makofii)

Mheshimwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana sasa tupige hatua, tuwe na vipaumbele vichache ambavyo tunaweza kuvifanyia kazi, bajeti ambayo ni *realistic*, inayotekelvezeka na tuifanye kulingana na *time*. Kitu kingine ambacho kinasikitisha sana ni kwamba mambo haya yanashindikana, lakini yapo mambo ambayo hayajapangiwa bajeti; hayapo mahali popote, unaona yanatekelezwa.

Mheshimwa Mwenyekiti, nimemsikia Mheshimiwa Rais akiwa kule Magomeni anasema natoa shilingi bilioni 10 kujenga nyumba; lakini huu mradi wa Mchuchuma kwa ajili ya fidia inayotakiwa pale ni shilingi bilioni 15. Hivi ni kwa nini hakushauriwa kwamba hili jambo la kwenda kufanya fidia kule mchuchuma ni la muhimu zaidi kuliko kwenda kujenga nyumba pale

Magomeni? Kwa hiyo, naomba sana Bunge lako liibane Serikali katika jambo hili ili haya mambo yaweze kufanyika. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ni suala la uzito unaotakiwa kutolewa kwa ajili ya sekta binafsi. Sekta binafsi ina mchango mkubwa sana kwa uchumi wetu. Nafikiri zaidi ya asilimia 57 ya uchumi wetu unategemea sekta binafsi. Ukiangalia mwenendo wa Serikali ya Awamu ya Tano kwenye suala la sekta binafsi, ni kana kwamba tunarudi kwenye ujamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesikia juzi hapa kwamba, limetolewa agizo kuwa nyumba zote za Serikali sasa hivi zitajengwa na *Tanzania Building Agency*. Hii ni kampuni kama kampuni nyingine; na kimsingi agency hii kazi yake siyo kujenga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni lazima tuishauri Serikali na Serikali iwe wazi, ituambie tunakwenda wapi? Sisi tunakwenda kwenye ujamaa au tunakwenda kwenye ubepari au tunakwenda kwenye ile mixed economy. Kwa sababu kimsingi ni kama tumechanganyikiwa hatujui tunapokwenda. Sasa matokeo yake ni kwamba tunaua private sector.

Mheshimwa Mwenyekiti, dada yangu hapa, Mheshimiwa Esther Matiko amezungumza habari ya madeni ambayo yanaibana sekta binafsi. Hili la kuibagua sekta binafsi kwenye kandarasi za Serikali na lenyewe linaua private sector ambalo ni tatizo kubwa na inaweza ikatuletea matatizo makubwa kwenye uchumi wetu. (Makofi)

Mheshimwa Mwenyekiti, hatupaswi kushangaa ni kwa nini uchumi unadorora... (Makofi)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. ANTONY C. KOMU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Narudia tena, wanaofuata ndio wanrifungia kabla sijahamia upande wa wachangiaji wa Serikali. Mheshimiwa Mtulia achukue nafasi ya Zuberi Kuchauka, halafu atafuatiwa na Mheshimiwa Kaboyoka na mwisho atakuwa Mheshimiwa Mgumba. Tunaanza na Mheshimiwa Maulid Mtulia.

**MHE. MAULID S. A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa namshukuru kaka yangu Mheshimiwa Kuchauka kwa kukubali kunipa nafasi hii badala yake. Pili, nakushukuru wewe Mheshimiwa Mtemi Chenge, kwa kunipa fursa hii adhimu kabisa na namna bora unavyotuendesha katika mjadala wetu huu. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, napenda nianze na kuelezea hali halisi ya uchumi na hasa nikichukua Jimbo langu la Kinondoni kama case study. Mimi kama mwakilishi nilijitahidi kupita kwa watu wangu; hali ni mbaya sana kwa wananchi wetu. Imefika mahali katika Manispaa yetu ya Kinondoni, mahotelii yanafungwa, nyumba za wageni zinafungwa, saluni watu hawaendi; hata sasa hivi tumerudi mtu ananunua nyembe anamtafuta mwenzie anampa kitana, anamnyoa nywele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliokwenda saluni sasa hivi hawafanyi tena scrub. Akiamiwa afanyiwe scrub, anasema hana muda, ana jambo anawahi. Hali imekuwa mbaya zaidi mpaka kwa akinamama lishe. Dar es Salaam imefikia sasa vijana hawali mchana. Mimi mwenyewe nimeshawahi kukaa na vijana nikawakuta wamechanga, wamesonga ugali wenye na samaki wa kukaanga wanakula. Wanakwepa mpaka kwenda kula kwa mama lishe. Hawa akinamama lishe wamekopa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kusisitiza hapa, mzunguko wetu wa pesa kwa wananchi ni mdogo sana. Nimesikitika umetolewa mchango hapa na Mbunge mwenzangu kijana, nimekatishwa tamaa sana. Kwa sababu sisi vijana tunategemewa kuja kuwa viongozi wa baadaye na inapofikia kijana haamini, analeta porojo kwenye suala la kiuchumi, mimi imenikatisha tamaa sana. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme suala la bajeti ya nchi yetu siyo suala la vyama, ni suala la Kitaifa. Tunapolichukua suala hili tukalifanya ni la vyama matokeo yake inakuwa mchezo wenu ni mauti yetu. Napenda tuangalie kwanza msingi wa bajeti yetu, kwa sababu inaonekana tulipotoka na tulipo ni tofauti. Hivi msingi wa bajeti yetu ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeambiwa msingi wa bajeti yetu ni llani ya Chama cha Mapinduzi; wakati mwingine ni hotuba ya Mheshimiwa Rais; Mpango wa Miaka 25 wa Maendeleo na mengine mengi yanaingizwa hapa. Turudi tuangalie misingi yetu tunayoitumia katika kutengeneza bajeti zetu. Kama utaratibu ndiyo huu, hatuwezi kufika. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bajeti ya nchi tukaikabidhi kuwa eti kigezo kikubwa ni ilani ya chama wakati hili jambo linahusu nchi nzima; nafikiri hapa ni mahali pa kuanza kubadilika. Lazima suala la uchumi wa nchi yetu liwe ni suala la kitaifa, tukubaliane tunataka kwenda wapi na kwa namna gani. Vyama vya siasa vipimwe kwa kutekeleza mpango kwa ufanisi, visiwe vyama vya siasa vinatuletea mipango hapa ya kila siku ya kuibuka. Leo ikipangwa ilani hii, nasi tunaitikia ilani hii, kesho akija Mheshimiwa Rais akatoa hotuba hii, nasi tunafuata hotuba hii. Haiwezekani! (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lazima mpango wa uchumi wa nchi yetu usiwe wa kikundi cha watu wachache, tukubaliane; halafu vyama vya siasa vipimwe utekelezaji wa mpango wetu wa uchumi tuliokulian. Wananchi watamchagua mtu kwa kutekeleza mpango wetu tuliokulian. Isiwe mtu akipata nafasi ya kuongoza nchi hii, basi ye ye ndio awapangie watu waende wapi. Hili nafikiri kuna mjadala hapa inabidi tufanye ili tupate muafaka. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuna tatizo kubwa la nidhamu ya bajeti yetu. Ukiangalia bajeti yetu tulichokubaliana na watekelezaji wetu, watu wetu wa Serikali wanavyotekeliza, ni tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye bajeti, tulikubaliana hapa futanunua ndege nne; lakini leo unaweza ukasikia mtu anajigamba eti tumeshalipa hela ya ndege sita. Msingi wa bajeti uko wapi? Kwa nini bajeti inapitishwa kama sheria? Leo nchi ya Tanzania imekuwa kama genge; mtu anaamua kufanya matumizi kwenye genge lake na siyo suala la Tanzania kuendeshwa kwa msingi wa bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo unaweza ukamsikia kiongozi wetu anakwenda mahali anasema nyie nitawapeni shilingi bilioni 10 hapa mjenge; nyie Magereza nawapa shilingi bilioni moja hapa mjenge; nyie Magomeni, nawapa shilingi bilioni 10 hapa mjenge; nyie sijui Katavi au wapi, nitawapeni hapa mjenge TRA ya shilingi bilioni ngapi! Hatuwezi kwenda kwa mtindo huu. (Makofi)

Mheshimiwa Naibu Spika, nidhamu yetu ya matumizi ni muhimu sana na lazima Bunge liheshimiwe kwa kuwa linapitisha bajeti na inakuwa sheria na ihakikishe inafanya kwa mujibu wa Sheria ya Bajeti. Hili ni muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukweli wa mipango yetu; hivi tumeongeza mipango yetu ya maendeleo ya bajeti kutoka 26% au 27% tukaweka asilimia 40;

ni kweli tulikuwa tunakusudia kutekeleza? Hivi kweli tunachokipanga tunakusudia kukitekeleza? Kwa nini hatuwi wakweli? Imefika mahali na sisi Wabunge tunapenda kuongopewa. Inafika mahali sisi Wabunge wenyewe tunataka Serikali ije kutuletea muujiza hapa. Nitafanya hivi asilimia 200, nitafanya hivi asilimia 300 mpaka mtu mmoja siku moja akasema kwanza asilimia mwisho 100. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hatuwi wakweli katika mipango yetu? Hivi wachumi wetu hawa hawajui projection ya mapato yetu? Leo inafika bajeti yetu, tumepeleka mipango yetu, fungu la maendeleo asilimia 20, tena inapelekwa kwenye quarter ya tatu mwezi wa 12. Hivi kweli watendaji wetu, wapangaji wetu wa mipango hawajui uhalsia wa hali yetu? Kama tunataka tubadilike tutoke hapa tulipo, tuwe wakweli. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiunga mkono sana Kamati ya Bajeti, imeeleza mambo mengi mazuri sana na kwa kweli kama Serikali itayafanyia kazi tutatoka. Nawaomba Wabunge wenzangu, bajeti ijayo na mipango ijayo; mpango amba siyo realistic tuukatae. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo mapato tuliyotegemea kutoka kwa wafadhili imekuja asilimia 16 tu na mapato tuliyokuwa tunayategemea kutoka kwa wafadhili ni zaidi ya shilingi trilioni 10.08. Asilimia sita ni sawasawa na shilingi trilioni moja. Kamati inatuambia kwamba hawajui kwa nini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuishauri Serikali na kuliomba Bunge lako Tukufu; tuna tatizo sisi na tatizo letu hatutaki kuambizana ukweli. Kuna jambo linasemwa kwamba sisi Zanzibar hatuko vizuri. Sisi ni Watanzania, ni wenyewe kwa wenyewe; hivi Wazanzibari wale wakikaa pamoja kuna tatizo gani? (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili Mheshimiwa Rais aliyepita Mheshimiwa Dkt. Jakaya Kikwete alitumia nguvu kubwa sana na muda wake mwangi kuwaunganisha Wazanzibari, Wazanzibari wakafika wakawa na Serikali yao ya Umoja wa Kitaifa. Hivi jamani sisi kama Taifa tunakwenda mbele au tunarudi nyuma? Baada ya kufika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, leo tunakwenda tunarudi nyuma? Naomba hili jambo lizungumzwe wale wenzetu wakae pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naamini kabisa, hizi pesa za nje zinakawia; mionganoni mwa sababu ni pamoja na huu utengamano wa Zanzibar, inaweza ikawa ni sababu. Hili jambo tusilichukulie kishabiki; ni jambo la Kitaifa, ni letu; sisi ni wenyewe kwa wenyewe, kwa nini tusikae kama Taifa tukatatua tatizo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wetu wote wapo na wote walikuwa ma-senior katika uongozi wa nchi hii. Nani asiyemjua Mheshimiwa Maalim Seif, nani asiyemjua Mheshimiwa Mzee Shein? Wote hawa wanajua na wote wana malengo ya kuhakikisha Wazanzibari wanafika mahali pazuri. Tukizungumza kama Taifa, naamini tutatoka na pesa hizo tutazipata. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho ni kwamba mipango yetu haizingatii hali yetu ya kimazingira. Hivi sisi tangu nchi hii imeumbwa, kuna samaki kule baharini wanapita, wanavuliwa huku juu Somalia, South Africa, wanapita wale samaki kila siku. Nimeongea na wataalam wa samaki wanasema, wale wanakua na wakishakua wanakufa. Sisi tangu tumepata uhuru nchi hii hatujawahi kutumia resource ile ya samaki. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Magufuli kuna kipindi aliikamata ile meli, wakapatikana samaki wengi, yule mtaalam anawaambia Watanzania hawajui hata resources zilizopo kwenye bahari yao, wananchi waliambiwa waende wakachukue samaki watu wamekwenda na mabeseni, kumbe samaki mmoja beseni halitoshi.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jamani, kwa nini hatuangalii mazingira yetu, Tanzania kwa jiografia yetu tunapokuwa maskini wenzetu hawatuamini, hawatuelewi, hawaelewi kwa nini tumekuwa maskini sisi, lakini sisi tukipanga mipango hatuangalii jiografia yetu, hatuangalii vitu gani sisi tunavyo wengine hawana, tunataka kufanya vitu wanavyofanya watu wasiokuwa na vitu kama vya kwetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaimba tu hapa viwanda, hivi sisi kweli tunaweza kwenda kwenye viwanda, kwa nini tusiende kwa yale tunayoyaweza. Sisi tunaweza kulima na watu wetu wanakuwa kwenye kilimo na tuliambizana hapa kilimo ndiyo uti wa mgongo, hayo ni majina – Kilimo Kwanza, kilimo cha kusonga mbele, majina yalikuwa mengi, lakini kimsingi kilimo ni uti wa mgongo. Kwa nini hatu-invest kwenye kilimo? Leo tunategemea...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MHE. MAULID S.A. MTULIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kaboyoka kwa upande huu namalizia na Mheshimiwa Omary Mgumba.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii. Mengi yameshasemwa, lakini napenda ni-concentrate katika mambo mawili au matatu. La kwanza, nilikuwa naangalia ripoti hii ya wenzetu, ni nzuri sana, Kamati inawapa pongezi mmeiweka ripoti vizuri. Nilipokuwa napitia ukurasa wa 42 kuhusu ukuaji wa Sekta ya Kilimo na kwamba asilimia 70 ya nchi yetu wananchi wetu wanategemea kilimo na kwamba sekta hii ndiyo inaweza kuondoa umaskini hasa vijiji na kweli vijiji ndio kwenye hii asilimia kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikaanza kujuliza, hii slogan ya Kilimo Kwanza tumeisikia muda mrefu sana, slogan hii sikuona ikiwekewa mikakati ya jinsi ambavyo ingeweza kutekelezwa. Nilikuwa nikipitia, nikiangalia jinsi ambavyo Kilimo Kwanza kingetekelvezwa wakati kila sekta inafanya bajeti yake, Sekta ya Maji imegeukia kulia, Sekta ya Kilimo imegeukia kushoto na sisi tunaongelea Kilimo Kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama priority ilikuwa katika umwagiliaji, kwa akili ya kawaida ungetegemea hizi sekta mbili ziweze kufanya assessment, ni maeneo gani basi tunakwenda kuyaboresha, je, tunakwenda kwenye Bonde la Rufiji, kuliko jaa maji, yale maji tunayatoaje pale? Ili bonde lile liweze kuilisha Tanzania na nchi za jirani, hilo hulioni. Hiyo slogan imekwisha. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imekuja slogan ya viwanda nayo naiangalia, hivi priority ya viwanda vyetu ni ipi, tunaangalia vyuma au tunaangalia kilimo ambacho tunajua kwanza ndiyo uti wa mgongo ili tuwe na ile backward and forward linkage tuweze kuoanisha kwamba kama basi tunataka viwanda priority yetu iko kwenye moja, mbili, tatu. Kwa hiyo, wakulima wetu wawezeshwe katika kilimo hiki na pesa nydingi iwekwe hapo, hasa katika umwagiliaji na ninyi muangalie ili tusitegemee mvua, huvioni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najiuliza hivi viwanda navyo vitakuwa kama Kilimo Kwanza, nchi yetu kwenda kwa slogans tu? Kama tunakwenda kwa slogans hivi tunamdaganya nani. Ningetegemea basi hata Wizara hii ya Fedha na Mipango waite hizi sekta Ministries wakae pamoja wawe focused, waangalie kwamba tunaomba pesa nydingi iwekwe katika sekta hizi mbili, tatu, ili tuweze kupata azma tuweze kufikia lengo letu la viwanda, kinyume cha hapo hii slogan nayo itapita kama ilivyopita ya Kilimo Kwanza. I am sure ukiangalia unaona kilimo kimewekwa pembeni. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenzetu wa Kamati wametuwekea vizuri sana kwamba hii sekta itategemea umwagiliaji, sasa kama umwagiliaji Wizara ya

Maji na Umwagiliaji wameweka mikakati ya kufanya sensa kwamba ni sehemu gani kuna maji mengi yanayoweza kutumika kwa umwagiliaji ili iweze ku-demarcate yale maeneo kwamba yatamwagiliwa na kwa malengo gani, kwamba tuta-produce kiasi gani? Nilishangaa wakati mmoja, nafikiri ilikuwa mwaka jana, Waziri wa Kilimo alivyozungumza, alipokuwa Soko la Kibaigwa kwamba ameshangaa mazao yamekuwa mengi sana na storage hamna, kwa hiyo yapo nje yananyeshewa yanaharibika, Waziri wa Kilimo anashangaa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tunasema tuna upungufu wa chakula, kwa kweli ukiangalia ni utani, ingekuwa hizi Wizara zinaendeshwa na Wapare na Wachaga ningesema hawa ni watani wa jadi, lakini unaona watu tuko serious, tunakaa hapa Waziri anasema ameshangaa mavuno ni mengi hamna pa kuweka, hii inaniambia kwamba hatufanyi kazi kwa kuweka malengo au malengo yetu tunaweka madogo sana, hatuwi *realistic*, hatutumii wataalam wetu kufanya *projections*, matokeo yake tunashangaa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachonishangaza zaidi, wakulima na wafugaji wote wako chini ya Wizara moja na kila siku kuna vita katika wakulima na wafugaji. Hivi hiki Kilimo Kwanza ambacho sasa Kamati hii inatilia mkazo kitakuwaje kama mtu amelima kesho ukiamka wanyama wameingia wamekula mazao yako yote. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, unaangalia Wizara moja mmeshindwa kuja na mikakati ya kuona mifugo yetu itunzweje, kilimo chetu kitunzweje. Bado wafugaji wetu ni wale wa kuswaga, zile *artificial insemination centers* zimekufa wakati ukiangalia hizi Sekta za Kilimo, Ufugaji na Utalii zingeweza kutoa nchi hii katika umasikini. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunaambiwa tuna ng'ombe wengi, viangalie ving'ombe vyetu vilivyokondeana, uliza anatoa lita ngapi per day, tunaringa katika Afrika Tanzania ni ya pili ikifuatiwa na Ethiopia, yet miaka yote hii hatuna mikakati. Unamwambia mfugaji punguza mifugo humpi target, huyu anaafuga 2,000, huyu 10,000, huyu 500, huyu 200, unamwambia apunguze, apunguze kutoka wapi kwenda wapi, akipunguza anapeleka wapi, kama anamuuzia Mheshimiwa Profesa Maghembe ni palepale si ndiyo, mifugo inatoka hapa inakwenda pale, hatuna viwanda vyaa nyama. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa anapunguza anapeleka wapi, unatoa mzigo kichwani unaweka begani ndiyo kupunguza huko? Kibaya zaidi humpi alternative, unaboreshaje ng'ombe wako, tuwe na shamba darasa weka ng'ombe kumi tukuonyeshe jinsi ya kuwaboresha vis-a-vis ng'ombe wako 1,000, mfugaji atawenza kuelewa. Hufanyi hivyo unamwambia punguza, amuuzie nani, kiwanda kiko wapi?

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Wabadilishe kwa debe la mahindi.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Sasa nasema kwa kweli kama nchi yetu inge-concentrate... (Makofii)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante!

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA:** Na kilimo tungekwenda mbali sana. Ahsante sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mgumba.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika hoja hii ya Kamati ya Bajeti. Kwanza niunge mkono hoja ya Kamati ya Bajeti kwa sababu mambo mengi, changamoto ambazo zinaikabili nchi yetu kama Taifa, mengi Kamati imezingatia, kwa hiyo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze sana Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi kwa makusanyo makubwa ya mapato na kubana matumizi kulingana na mapato hayo halisi bila kutegemea misaada mingine. Baada ya pongezi hizo niwe na ushauri mdogo, kwa sababu tumeona pamoja na makusanyo makubwa ya mapato hayo item mbili ndio zinakula; mishahara pamoja na madeni. Kwa bahati mbaya sana madeni mengi ambayo yanalipwa kwenye kandarasi kubwakubwa na nydingi hizi zinatoka nje, maana yake ni nini? Serikali inatumia hizo bilioni zaidi ya 900 kwa mwezi lakini hela zile baadaye zinahama kutoka nchini zinakwenda nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ningeomba ushauri katika hili, Serikali sasa ni vizuri ili kusisimua uchumi ndani ya nchi nao kuwalipa wawekezaji wa ndani ili kwanza wawezee kusisimua uchumi, wakiendelea kufanya biashara wataendelea kutoa ajira kwa wananchi wetu lakini pia mzunguko wa pesa

utakuwepo ndani ya nchi lakini kuendelea kuwalipa na yale madeni ya nje tu maana yake zile hela zinakwenda kuimarisha mzunguko kwenye nchi za wenzetu. Tunajua dawa ya deni ni kulipa lakini tuwe na balance ya sehemu zote mbili. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi tunasema tuna uchumi wa viwanda, ni kweli kabisa tuna uchumi wa viwanda lakini pamoja na uchumi huu wa viwanda Serikali peke yake lazima inaitegemea sana sekta binafsi. Sekta binafsi hizi zingine ziko ndani ya nchi, kwa hiyo tunapowalipa wadeni wa ndani tutakuwa tunawarahisishia kushiriki kwenye uwekezaji wa ndani ya nchi kwenye uchumi wa viwanda. Kwa mfano tu, Serikali leo ikiweza kulipa mifuko ya jamii ambayo wanaidai Serikali mifuko hii itakuwa na uwezo mkubwa wa kuweza kuwekeza kwenye uchumi wa viwanda na sekta nyingine hapa nchini na kutoa ajira na kuimarisha uchumi ndani ya nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, kwenye suala la kilimo; kama ukurasa wa 42 unavyosema kilimo ndio uti wa mgongo, kinaajiri zaidi ya asilimia 70, lakini kwa bahati mbaya sana kilimo hicho hicho ukuaji wake kila mwaka unakwenda chini, sasa hivi tunaambiwa ni asilimia tatu ambayo hata yale makubaliano tu ya Maputo kule tunatakiwa angalau tuchangie asilimia 10, lakini kwa mwendo huu inaonekana bado tuna safari ndefu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wangu kwenye hili, kwa sababu huwezi kutatua matatizo ya kilimo au kilimo kipande bila kutatua matatizo yanayokabili Sekta yenye ya Kilimo, wenzangu wamezungumza mengi lakini lazima Serikali ije na mkakati mzito kwenye kutatua hili tatizo la mipango bora ya matumizi ya ardhi. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri sasa kama zamani wakati wa Mwalimu Julius, ilikuwa inajulikana kabisa mikoa gani ya wafugaji na mikoa gani ya kilimo, kwa sababu hata tunapozungumza matumizi bora ya ardhi maana yake ni kwamba tukatenge ardhi zetu wapi panafaa kwa kilimo, wafugaji wakae wapi, makazi yake wapi. Sasa mpango huohuo uanzie ngazi ya Kitaifa kwanza kwa sababu haiwezekani ukawaweka pamoja wafugaji na wakulima, haiwezekani kukaa pamoja. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, lazima tujue kabisa mikoa gani itatupa tija kwa ajili ya mifugo na mikoa gani itatupa tija kwa ajili ya kilimo. Nitoe mfano, Mkoa wangu wa Morogoro, tumeambiwa Ghala la Taifa, Ghala la Taifa maana yake ninyi mko zaidi kwenye mambo ya kilimo lakini hali inayoendelea kule kama hii mipango bora hatutaizingatia kuanzia ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya

itakuwa ni hadithi. Kwa hiyo, niombe tu hii mipango bora ya ardhi ianze kuanzia ngazi ya Taifa, itangaze kabisa mikoa gani mahsus kwa ajili ya kilimo na mikoa gani mahsus kwa ajili ya mifugo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo katika kilimo, leo kilimo hakivutii wakulima wapya, hakivutii mtu kwenda kuwekeza kwenye kilimo sababu kilimo chetu bado kinategemea mvua, huna uhakika wa kuvuna. Ndiyo maana leo bajeti ya kilimo kwenye mbolea kila mwaka inaongezeka lakini tija inapungua. Kwa nini? Mtu anaweza akapata mbolea, anaweza kupata trekta anaweza kupata mtaji lakini kama hana maji hayo yote ni bure, kama tunavyoona mwaka huu mvua haijanyesha, watu wamewekeza lakini watapata hasara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mfano mzuri ndiyo maana unaona hata Benki ya Kilimo yenye we ina hela zaidi ya bilioni 59 lakini imekopesha bilioni tatu tu kwa sababu anaona kwamba hata akikopesha uhakika wa kulipa hamna. Ushauri wangu katika hili ni vizuri sasa Serikali tujielekeze zaidi katika mipango yetu kuwekeza kwenye maji, hasa kwenye mabwawa. Kwa hiyo, naungana na maoni ya Kamati kuongeza ile shilingi 50 kila lita ili iwe 100 ili Wizara hii iwe na Mfuko wa kutosha wa maji twende kutatua changamoto za maji na kukabiliana na hali halisi inayolikabili Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, sasa hivi tuna ukame, mara nyingi tunakuja na mipango ya kukabiliana na matokeo hatukabiliani na chanzo kilichosababisha ni nini. Sasa hivi tuna tatizo hili la ukame sasa tukawekeze kwenye masuala ya mabwawa ya umwagiliaji ili kilimo chetu kiwe cha uhakika, mtu ye yote akienda kuwekeza kwenye kilimo awe na uhakika wa kuvuna kwa sababu maji ya kumwagilia yapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi hata hizi benki za biashara tutakuwa tumetatua suala la mitaji kwa wakulima kwa sababu watawakopesha kwa sababu wanawafahamu kwamba wana uhakika wa kulipa kwa sababu wana uhakika wa kuvuna katika uwekezaji huo wa kilimo. Hata tukiongeza mbolea, hata tukiongeza madawa kama uhakika wa maji hamna, kama kilimo cha umwagiliaji hamna, hamna benki yoyote – iwe ya kilimo au iwe ya kibiashara ambayo inaweza kuwekeza kwenye suala la kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine kuhusu kukopa zaidi ndani, ndiyo maana Waheshimiwa Wabunge wengi, kuna mmoja alikuwa anazungumza anasema kwa nini sasa hivi hatukopesheki huko nje, kuna sababu gani. Sababu ziko wazi tu, sababu ni kwamba sasa hivi *demand* imekuwa kubwa kuliko *supply*, hata

hao wakopaji uwezo wao sasa hivi nao ni mdogo. Mfano mdogo tu tunauona sasa hivi hata Marekani wenyewe huyu Rais mpya aliyeingia anasisitiza viwanda vyao wawekezaji warudi kuwekeza ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili limeishtua kidogo hata China. China wanasema sasa wanataka kubadilisha badala ya kwenda kuwekeza zaidi nje ya nchi wanaona ni bora kufanya *innovation* kwenye teknolojia yao ili kupunguza gharama za uzalishaji ili waendelee kuzalisha ndani ya nchi zao, maana yake wa-reduce production cost ili waendelee kulinda ajira yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii ni *signal* sio nzuri kwetu tunaposema kwamba tunakwenda kwenye uchumi wa viwanda maana yake *support* kutoka kwa Mataifa makubwa itakuwa ni ndogo kwa sababu haya sasa na wao sasa hivi wataangalia zaidi Mataifa yao kuliko kuja kuwekeza kwetu kwa sababu wanaona kwamba kuja kuwekeza huku kama wanahamisha ajira za watu wao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hii kama Serikali tuihukue na twende kwa tahadhari. Ni vizuri katika hili tukajielekeza zaidi katika yale mambo ambayo tuna uwezo nayo na tuko wazuri katika uzalishaji zaidi kuliko haya ya kutegemea wawekezaji kutoka nje. Hawatapenda kwamba tuendelee kama wao halafu tuje tuendelee kugombania soko lilelile, wao wanapenda waendelee kututumia sisi kama soko badala ya kuwa *partner* wazalishaji wenzao. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, katika suala la hizi milioni 50, ni vizuri kwamba Serikali ikaleta haraka sana, ndani ya bajeti hii kabla haijaisha ni vizuri hizi hela zikafika huko vijijini ili ziweze kwenda kusisimua hali ya uchumi na kuongeza mzunguko wa uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, ni vizuri Serikali tukawa na vipaumbele vichache ambavyo vinalingana na uwezo wetu badala ya kuwa na vipaumbele vingi ambavyo tunaviandika tu, wakati mwingine utekelezaji wake unakuwa hafifu. Ni vizuri tukavichagua vichache tukavitekeleza na kutohana na hali hali sasa hivi – kama alivyosema mwenyewe Waziri wa Fedha – upatikanaji wa mikopo ya masharti nafuu nje imekuwa ni michache sana, mikopo inayopatikana sasa hivi ni ya kibiashara. Kama mikopo inapatikana nje ya kibiashara maana yake itakuwa na masharti magumu na matokeo yake hata tukikopa zaidi itakuwa na riba kubwa na itakuwa ni mzigo mkubwa sana kwa Taifa na vizazi vijavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja ya Kamati, ahsante sana kwa kunipa nafasi. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mgumba. Kwa heshima ya kipekee nimitambue tu Mheshimiwa Hawa Ghasia, Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Bado dakika ngapi? Dakika tano?

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nikushukuru kwa kunipa nafasi nichangie taarifa yetu ya Kamati ya Bajeti. Kwanza nianze kwa kipongeza Serikali kwa kuongeza bajeti ya Serikali kwa upande wa miradi ya maendeleo hadi kufikia asilimia 40. Tunachoomba tu kwamba pesa ziendele kwenda kwa wakati ili miradi itekelezwe kama ambavyo tumeponga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia niipongeze Serikali kwa hatua ya kusaini mkataba kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kati. Reli ya kati ni kama mishipa ya fahamu ya mwili wa binadamu kwa uchumi ya nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuendelea kwa kutegemea bidhaa na malighafi zetu kubebwa na Lori moja moja kutoka Dar es Salaam mpaka Kigoma, Mwanza na kwenda nchi za jirani na hilo hilo lirudi lije lichukue kwa kweli hili haliwezi kutufikisha mbali lakini kwa hatua hii ya Serikali kusaini Mkataba wa kujenga reli tena kwa standard gauge kutoka Dar es Salaam hadi Morogoro kama hatua ya kwanza naipongeza sana na tunaomba vipande vilivyobaki basi vifanyiwe haraka ili mradi huo uweze kukamilika kwa wakati ili kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi wa nchi yetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo ningependa Serikali kulisisitizia ni eneno la EPZA. Kamati ilitembelea eneo la Mheshimiwa Benjamin Mkapa pale Mabibo, kwa kweli kule ndani kuna kazi nzuri sana inayofanyika na kuna ajira nyingi sana zinazotolewa kwa vijana wetu. Bidhaa zinazozalishwa pale ni za ubora wa hali ya juu na za mauzo ya nje ambazo zinatuingizia pesa za Kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kitu kama kile tulitegemea Dar es Salaam pale tuwe na EPZA kama mbili na ikiwezekana angalau kila mkoa tuwe na eneo la EPZA kwa sababu ni eneo ambalo linakuza ajira, linaingiza mitaji, linatuongezea teknolojia kutoka nje. Eneo la Kurasini tayari Serikali ilishalipia fidia kwa hiyo, tunaomba wawezeshwe EPZA kuweza kujenga miundombinu na hivyo kuwavutia wawekezaji kuja kuwekeza katika eneno la EPZA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la tatu, kwa sababu umenipa dakika tano, ningependa kusitiza suala la utekelezaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga. Mradi huu umezungumzwa kwa muda mrefu sana na ni mradi ambao kwa kweli utaleta viwanda mama, viwanda vyta vyuma, viwanda ambavyo vivaleta viwanda vingine. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua iliyofikiwa si mbaya kwa maana kwa upande wa uzalishaji wa umeme kwa kutumia makaa ya mawe sawa, lakini upande wa chuma. Makaa ya Mawe yale na chuma tunategemea kwa kiasi kikubwa yasafirishwe kupitia Bandari ya Mtwara na reli ambayo tayari feasibility study ilishakamilika, upembuzi yakinifu ulishakamilika sasa hii tathmini ya fidia ilishakamilika, kwa hiyo, tunaomba fidia ile iweze kulipwa na ile reli kutoka Mtwara kwenda Mchuchuma na Liganga na matawi yake kwenda Mbamba Bay upewe umuhimu wa hali ya juu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu chuma kile bila reli ile na makaa ya mawe yale bila reli ile kwa kweli hatuna barabara za kuweza mzigo mzito kama ule sana sana barabara zetu zitakuwa ni za kujenga baada ya miaka miwili zimeharibika halafu tunawalaumu waliojenga au waliosimamia kuzijenga lakini ni kutokana na mzigo mzito kwa hiyo nisitisize mradi wa Liganga na Mchuchuma na pia reli ya kutoka Mtwara, Liganga na Mchuchuma vitekelezwe kwa wakati muafaka ili kukuza uchumi wetu. (Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana ulinipa dakika tano nisingependa unigongee kengele, naunga mkono hoja. (Makof)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mwenyekiti. Sasa nahamia kwa wachangiaji upande wa Serikali. Hawa nitakaowataja kwanza tunawapa dakika tano, tano. Naibu Waziri wa Kilimo dakika tano, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali dakika tano, Mheshimiwa Waziri Maliasili na Utalii dakika tano, Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais dakika tano, Naibu Waziri Wizara ya Fedha na Mipango dakika tano. Tunaanza na Naibu Waziri wa kilimo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru ningeomba kuchangia kuhusu hoja ya Kamati na kwanza niseme kabisa kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia sana kuhusiana na masuala ya Kilimo, Mifugo na Uvuvu ambayo ni kielelezo tosha kabisa kuhusu namna suala la Kilimo, Mifugo na Uvuvu liliyvo na kipaumbele kwa Watanzania wengi ndiyo maana Wawakilishi wa wananchi wameweka mkazo katika kulizungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za Wabunge ziko nyingi kwa vyovoyote vile kwa dakika tano sitaweza kuzipitia zote lakini kwa ujumla wake, Waheshimiwa Wabunge wameonesha moja; kwamba kuna haja ya kuongeza bajeti ya kilimo kuliko vile ilivyo sasa ili iweze kuakisi umuhimu wa sekta hii katika jamii. Kimsingi Serikali inakubaliana na hili na nafikiri Waheshimiwa Wabunge tutashirikiana nao tunavyoelekea katika bajeti inayokuja ili kuona kwamba bajeti ya Kilimo inaongezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia sana kuhusu suala la pembejeo katika maana ya ubora, kufika kwa wakati kwa wakulima lakini vilevile kuhusu bei ambayo inaweza ikahimilika kwa wakulima wengi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara imejipanga kukabiliana na changamoto hii ya pembejeo na tunafikiria tuko mbioni kuanzisha utaratibu ambao mbolea inapatikana kwa utaratibu wa *bulk procurement* kama utaratibu ulivyo wa sasa wa mafuta unaofanywa na EWURA. Kimsingi tunaamini kwamba kama tunaweza kuta-subsidies kutoka kwenye source inakuwa ni rahisi Watanzania wote kupata mbolea kwa bei moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile tunaamini kwamba, gharama ya sasa ya juu iliyopo katika mbolea na baadhi ya pembejeo ni suala vilevile linalosababishwa na tozo na kodi ambazo zimebekwa katika bidhaa hizi. Kwa hiyo, vilevile tutaomba Bunge lako, tutakuja na mapendekezo ya namna ya kuondoa kodi, tozo na ada mbalimbali ambazo zinaendelea kuchangia pembejeo iwe bei ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini vilevile Serikali bado ipo kwenye mkakati wa kuhakikisha kwamba mbolea inazalishwa ndani. Tunaamini kwamba bei kubwa iliyopo ya sasa ya mbolea ni suala vilevile la kwamba ni gharama kwa sababu tunaagiza kutoka nje kwa hiyo tukiwa na viwanda vya kuzalisha mbolea ndani tunaamini kwamba itatusaidia kupunguza bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, imezungumzwa vilevile suala la ukame na uhaba wa chakula. Hili tulishalitolea ufanuzi katika Bunge hili lakini niendelee kuwashakikishia Waheshimiwa Wabunge kutokana na tathmini ya kina ambayo Serikali imefanya, Serikali inaamini kwamba tumejizatiti vya kutosha vya kuhakikisha kwamba hamna Mtanzania atakayekufa na njaa na nimhakikishe tu Mheshimiwa Lwakatare ambaye ye ye keshasema watu watakuwa njaa mwezi wa tatu, kwamba, Serikali itahakikisha hili halitokei, tumeweka mikakati ya kufuatilia kuhakikisha Watanzania wanakuwa na usalama wa chakula.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na suala la migogoro kati ya wafugaji na wakulima; Hili nalo limevuta hisia ya Waheshimiwa wengi. Kimsingi kama Serikali tunakubali kwamba hili ni eneo ambalo matokeo chanya na ya haraka yanahitajika kutokea kwa sababu migogoro hii imeongezeka. Tunavyozungumza tayari Serikali ina Tume ambayo inazunguka nchi nzima kupitia migogoro yote ili kuweza kutoa mapendekezo ambayo tunaamini kwamba yakifanyiwa kazi kwa kiasi kikubwa tunaweza tukaondoa migogoro hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia vilevile kuhusiana na suala zima la haja ya kuongeza jitihada katika kufanya kilimo cha uwekezaji. Wizara imelipokea hili tunaamini kwamba ni kweli.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya machache nashukuru sana na naomba kuunga mkono hoja. (Makofi)

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia fursa hii ili niweze kuchangia lakini zaidi nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuchangia hoja hii. Naunga mkono taarifa ya Kamati na ushauri uliotolewa na Kamati ni mzuri sana na moja; wameshauri juu ya umuhimu wa kulipa deni. Ni hoja na ushauri mzuri sana kwa sababu usipolipa deni madhara yake ni makubwa sana mbali ya haya yanayoweza kujitokeza kwa hawa ambao wameikopesha Serikali, lakini pia gharama zinaongezeka pale ambapo wanaotudai wanaweza wakatupeleka hata Mahakamani, kwa hiyo gharama zinaongezeka kwa hiyo ushauri ule ni mzuri, sisi tunaupokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine nililotaka kuchangia ni suala tu la namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge tunajenga hoja hapa. Kanuni zinatukataza wakati wa mijadala kutumia jina la Rais kwa dhihaka katika mijadala au kwa madhumuni ya kushawishi kufikiwa maamuzi fulani. Kwa hiyo, naomba tu nikumbushe Wabunge wanapokuwa wanashiriki kutekeleza jukumu lao la Kikatiba la kuishauri na kuisimamia Serikali wanapojenga hoja, wajenge hoja kwa namna ambavyo pia haikiuki kanuni tulizojiwekea. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tu kusema kwamba kauli za Rais na Viongozi wengine tuzitazame katika muktadha wa yale anayozungumza katika contextual meaning kuliko una-peak tu sehemu fulani halafu unalipotosha kabisa lile kusudi lililokusudiwa. Kwa hiyo, nishauri hivi; tunatambua Katiba imeweka uhuru, haki ya kila mtu kuwa na uhuru wa mawazo na fikra zake, ni jambo la msingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haki hiyo lakini tuitumie vizuri kwa kuangalia muktadha wenyewe wa ile kauli yenyewe, tusipotoshe. Kwa mfano, Mheshimiwa Lwakatare amezumgumza aliyozungumza Rais kuhusu ngono au katerero, amekiri kabisa kwamba yale mambo yapo Bukoba na watu wanaweza kwenda kujifunza kule na kiko Kijiji mahususi kwa ajili hiyo, lakini ukweli ni kwamba Rais alikuwa anazungumzia ngono na katerero? Hapana.

**MBUNGE FULANI:** Kujifunza nini?

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba Waheshimiwa Wabunge tunapotumia haki yetu ya Kikatiba ya kuwa na uhuru wa mawazo na fikra, basi tutoe tafsiri sahihi kwa kauli zinazotolewa na viongozi wa Serikali kwa kuzingatia muktadha wa kauli hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofii)

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Profesa Maghembe.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti napenda nikushukuru sana kwa nafasi hii, mapema kabisa niseme kwamba naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia juu ya utalii na namna ambavyo tunaweza kuuboresha utalii wetu. Nianze tu kwa kusema kwamba utalii wetu unachangia asilimia 17.5 ya mapato yetu yote ya mwaka ya Taifa na asilimia 25 ya fedha zote za kigeni tunazopata. Aidha, inatoa ajira kwa watu laki tano, ajira za moja kwa moja na Watanzania milioni moja wamejiajiri wao wenyewe katika utalii na potential ya kuongezeka ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa sekta ya utalii ikiwa na mchango wake mkubwa huu na ukizingatia kwamba hata mtu anayenunua sukari, unga, misumari kwenye duka la mtaani analipa VAT. Hutegemei kwamba sekta ambayo inachangia karibu moja ya tano ya pato lote la Taifa nchini ifanye biashara hiyo bila kulipa au kuchangia mapato ya kodi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utakumbuka wakati ulipokuwa Mwenyekiti wa Kamati hii ya Bajeti mwezi Juni mwaka 2015 mliwaita wadau wengi sana kuzungumza nao na kuangalia namna ya kupanua wigo wa kodi hapa nchini. Mwezi Juni mwaka 2015 mlikutana na wadau wa utalii na kuwapa taarifa kwamba mmeona kwamba huduma za utalii ni moja ya maeneo ambayo mnafikiria kuyaongeza kwenye wigo wa kodi. Wakati ule Wadau wakaomba mwaka mmoja ili waweze kuijandaa na kweli kwa mwaka ule 2015/2016 wakapewa ahueni hiyo na mwaka 2016/2017 ndiyo kodi hii ikaingizwa kama mapendekezo ya Kamati yetu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa ni-propose hata tabasamu kidogo kwamba Kamati hii imekuwa na mchango mkubwa katika kuiangalia bajeti na kuongeza mapato ya Taifa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, VAT inatumika duniani kote, nchi jirani yetu iliondoa VAT katika kipindi hiki cha mwaka 2016/2017 kwa sababu maalum. Katika mwaka 2013/2014, Watalii walioingia kule walikuwa milioni mbili lakini mwaka 2015/2016 waliteremka wakafika milioni moja nukta tatu. Kwa sababu hiyo wakaona labda wakiondoa VAT watarudisha watalii wafike kiwango kile ambacho kilikuwa nyuma na ninyi mnajua wote kwamba ilitokana na Ugaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka huu wa kwanza wa kutoza VAT hatujaona negative impact ya VAT kwenye idadi ya watalii. Napenda pia niseme kwa sababu muda wenye ni mfupi sana na niwapongeze Waheshimiwa Wabunge...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji)

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. (Makofii)

**MWENYEKITI:** Anafuata Mheshimiwa Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa fursa ya kutoa mchango. Kwanza nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Hawa Ghasia pamoja na Kamati yake kwa kazi nzuri waliyoifanya naunga mkono hoja waliyoitua na mapendekezo waliyoyapendekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wote tunafahamu kwamba Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliongoza nchi yetu hii kwa miaka 24 na tangu ametutoka ni miaka 17 na siku zote bado amebaki kuwa rejea ya masuala mbalimbali ya uongozi wa Taifa letu na kwa kweli amekuwa kama sehemu ya uongozi wa nchi kwa maana ya reference hata akiwa kaburini. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini imekuwa hivyo? Je, ni kwa sababu ameifikisha nchi yetu kule kwenye ndoto kabisa ya maendeleo makubwa ya kiuchumi, hapana. Ni kwa sababu dhamira yake ya kutufikisha huko ilikuwa wazi na ilieleweka pamoja na kwamba hatukufika kule tulikokuwa tunatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais Dkt. Magufuli sasa hivi ana miezi 15 tu ya uongozi wake. Dhamira ya kutupeleka kwenye nchi ya neema hamna mtu ye yeyote anayeweza kubisha katika Bunge hili kwamba ipo. Dhamira iko wazi, ni nzuri na inaeleweka.(Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais wetu sasa hivi na Serikali ya Awamu ya Tano ina miezi 15 tu madarakani kati ya miezi 120 ambayo tunatarajia Rais aiongoze nchi yetu. Leo tunachojadili ni robo tu ya bajeti ya kwanza kamili ya Serikali ya Awamu ya Tano. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo, hamna ubishi kabisa kwamba kuna improvement kwenye kila eneo la utendaji wa Serikali na unapojenga misingi, unapoimarisha misingi ili mbele iwe rahisi kabisa kutengeneza mambo yawe rahisi nafahamu kuna watu watapata shaka watakuwa na uwoga, watapinga. Naamini kwamba nchi hii ni yetu sote na wakati mwingine unasikitika kwamba inapotolewa habari mbaya hapa Bungeni au habari ya kusikitisha, kwa mfano tunaposema Benki fulani imepata hasara nashangaa kuna watu wanapiga makofi kana kwamba hiyo ni habari ya kufurahisha. Nchi hii ni nchi yetu sote, habari ya kusikitisha ni yetu sote. Wawe Wapinzani, wawe watu wa CCM. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tusifike mahali tukaamini kwamba mambo yanapotokea na kunapotokea setbacks basi kuna watu wanapaswa kufurahia. Nchi hii ni yetu sote, watu tunaowaongoza ni wetu sote, hivyo, naamini kabisa kwamba mtu yeoyote mwenye akili timamu hawezi akasimama leo akasema nchi yetu imerudi nyuma badala ya kwenda mbele. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna ndugu amesimama amezungumza kuhusu Zanzibar kwamba kuwe na mazungumzo, tukae, kaka yangu Mheshimiwa Mtulia. Sasa uchaguzi Zanzibar ulikwishafanyika, Serikali ilishapatikana, Serikali halali, imechaguliwa kwa kura halali na ni muhimu kutambua kwamba Serikali ile ni ya Umoja wa Kitaifa kwa sababu kuna vyama vinne ndani ya Serikali ile na Serikali ile iko tayari kuzungumza...

(*Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa  
muda wa mzungumzaji*)

**MWENYEKITI:** Malizia, malizia.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba unilinde muda wangu umeliwa.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuvumiliane tu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Wenzetu watusaidie kwamba tuzungumze na nani kwa sababu CUF ziko mbili, tuzungumze na ipi? (Makofij)

**MBUNGE FULANI:** Kwa upande ule wa Zanzibar.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tuzungumze na ile iliyochukua ruzuku au ile nyingine?

**MBUNGE FULANI:** Zungumza na mtu aliyechaguliwa!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. (Makofij)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

**WABUNGE FULANI:** Buuuuu!

**MWENYEKITI:** Tunaendelea. Waheshimiwa naomba amani, utulivu. Naomba utulivu. Ahsante.

Tunaendelea, Waheshimiwa naomba utulivu. Haya Naibu Waziri Fedha na Mipango.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na naomba nianze kwa kusema naunga mkono hoja iliyowekwa mezani na Kamati yetu ya Bunge ya Bajeti. Nimpongeze Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa dada yangu Hawa Ghasia pamoja na Makamu wake na Wajumbe wote wa Kamati yetu ya Kudumu ya Bajeti kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wakiifanya kwa kutushauri sisi Serikali na kutusimamia. Kwa kweli mnafanya kazi nzuri sana. Hongereni sana. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme machache kwa sababu muda ni mfupi ambao nimepatiwa, naomba nianze na hili ambalo Waheshimiwa Wabunge wengi wameonesha concern yao kwamba Serikali ipunguze kukopa ndani, tunapunguza mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niwaambie Waheshimiwa Wabunge na Bunge lako Tukufu kwamba, Serikali yetu inakopa katika soko la ndani kwa kuzingatia uwezo wa soko lenyewe na kuhakikisha kuwa haipunguzi uwezo wa Taasisi hizi kukopesha Sekta Binafsi na watu binafsi. Hili naomba lifahamike kuna miongozo, kuna vigezo na lazima tufahamu hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wameihuisha pia na kukopa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, lakini naomba pia ifahamike kwamba Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ina taratibu na miongozo ya uwekezaji ikiwa ni pamoja na kupanga kiwango au kiasi cha fedha wanazoweza kuweka katika hati fungani na dhamana za Serikali. Kwa hiyo, kama Serikali tuko makini, hatuwezi kabisa kukopa katika Mifuko hii ya Hifadhi ya Jamii mpaka ikafikia kiwango cha kushindwa kulipa wastaa fu wetu. Tuko vizuri, tuko imara na mifuko yetu inafuata miongozo kila kitu na wala hamna shida katika hili. Niombe tu kuwajulisha kwamba mikopo ya ndani pia ni njia mojawapo ya kuimarisha Sekta Binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inapokopesha ina uwezo wa kufanya hivyo. Kwa hiyo, tukizua na kusema kwamba hapana kwa Serikali tutakuwa tunaiua Sekta yetu Binafsi, tutaua Taasisi zetu ambazo zinaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hilo pia Waheshimiwa Wabunge wameongelea kwamba Mabenki kufanya vibaya kwa sababu hiyo tunakopa, kama nilivyosema mwanzo hapana. Mabenki yetu sasa yanajitathmini yenyewe. Tukumbuke tuliwahi kusema hapa ndani ya Bunge hili kama Serikali yetu kwamba ilifika sehemu mabenki haya yakawa yanatumia pesa ambazo sio za kwake na yakasahau jukumu lao kubwa. Kwanza anapokuja mtu kukopa pale benki anatakiwa afanye tathmini - ilikuwa haifanyiki. Niko Wizara ya Fedha nawasiliana na nafanya vikao na ma-CEO wa mabenki haya, wanaeleza kabisa kwamba sasa mtu aki-apply mkopo wanakwenda kwenye vigezo. Ilifika sehemu wanakopesha bila vigezo na ndiyo maana ya kuongezeka kwa mikopo chechefu. Lazima tuweke uimara katika usimamizi wa sekta yetu ya fedha ili tuweze kutoka vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningependa kulitolea ufanuzi au kuchangia hoja hii ni kuhusu kodi ya majengo kukusanya na TRA. Katika hotuba hii iliyowasilishwa na Kamati yetu ya Bajeti na data tunazoziona ni kwa quarter ya kwanza na katika quarter ya kwanza, Januari mpaka Septemba, TRA hawakukusanya kodi ya majengo na Halmashauri zilipewa maelekezo waendelee kukusanya kodi hii ya majengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, performance tunayoiona ni ya Halmashauri zetu kukusanya kodi ya majengo na ndiyo maana Serikali imeona sasa kama Halmashauri zetu zinakusanya katika *level* hii inaonesha kabisa haziwezi na sasa TRA ichukue kodi hii ili iweze kukusanya. Itakapoletwa taarifa ya nusu mwaka iki-include na quarter ya pili tutaona utofauti mkubwa wa kodi ya majengo ambapo TRA wameanza kukusanya kuanzia mwezi wa Kumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba tuelewe nia ya Serikali na lengo la Serikali yetu ni jema. Halmashauri zetu zilishindwa kufanya vizuri ndiyo maana kama Serikali tumechukua ukusanyaji huu na mtaona tutakapoleta tathmini yetu ya nusu mwaka, kuna utofauti mkubwa katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengi naomba nimalizie kwa kusema katika hili la kufunga biashara nimeona pia Wabunge wengi wameshangilia. Ndugu zangu naomba mfahamu sasa hivi tunarasiusha biashara zetu. Tunaona TRA wanatoa *TIN* mpya, biashara zilizofungwa ni 4,183, naomba tufahamu katika hili. Biashara mpya zilizofunguliwa ni 1,039,554. Kwa hiyo, naomba niseme

katika hili, tutaleta taarifa katika Bunge lako, tunamalizia kufanya tathmini ya ukubwa wa biashara zilizofungwa na ukubwa wa biashara zinazofunguliwa. Kwa hiyo, lazima tuongee tukiwa na data ndugu zangu ili tuweze kuitendea haki Serikali yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. (*Makofij*)

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Waziri wa Fedha na Mipango, dakika kumi.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kushukuru sana kwa kuongoza kikao hiki vizuri, lakini pia kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia. Vile vile niruhusu niipongeze sana Kamati ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia na Makamu Mwenyekiti, Mbunge wa Kalambo kwa kazi nzuri sana wanayofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema kutoka moyoni kabisa, Kamati hii ni very pragmatic, very resourceful na wamekuwa wanatusaidia sana. Serikali nipende kuahidi kwamba itazingatia maoni na mapendekezo ambayo wametupatia katika uandaaji wa bajeti inayokuja na tutaendelea kuzifanya kazi. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nizungumzie mambo tu machache. Kwanza kulikuwa na hoja ya washirika wa maendeleo kutotoa fedha na kwamba sababu zake hazifahamiki. Sababu za washirika wetu wa maendeleo kutotoa fedha ni nyingi sana. Mojawapo kwa kweli ni yale masharti yenyewe ya kutoa fedha. Yako masharti ambayo hatukubaliani nayo na tunaendelea kuzungumza na wenzetu ili watuelewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja nitoe tu mfano; kwa mfano tulikuwa tunaomba fedha kwa ajili ya kuboresha bandari yetu ya Dar es Salaam, lakini moja ya sharti tulilopewa ni kwamba ni lazima sasa TPA wajiondoe kwenye kuendesha Bandari badala yake aje mtu binafsi kuendesha bandari yetu. Hatukubali hilo Waheshimiwa Wabunge na sisi tunafanya kwa maslahi ya Taifa letu. Tumeshakuwa na uzoefu wa kutosha. (*Makofij*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mengine ambayo pia wanatusukuma huko ambayo sio sawasawa, ni kinyume cha mila na desturi za Kitanzania na hatuwezi kuzikubali. Kwa hiyo, hiyo ni mojawapo. Pia kuna ukweli kwamba kuna mabadiliko katika mtazamo wa Serikali nyingi ambazo zimeingia madarakani hususan katika nchi za Ulaya. Tumekuwa na majadiliano sisi bado tunadhani kwamba general budget support ndiyo njia nzuri ya wabia wetu kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wao wamebadili msimamo, wanasesma wapeleke fedha moja kwa moja kwenye miradi. Tulishakuwa huko, tunajua changamoto za wao kupeleka fedha kwenye miradi wanayochagua kwenye mikoa wanayochagua badala ya kutupa sisi kama Watanzania nafasi ya kusema tumezunguwa zaidi huku sisi tupeleke kule. Hata hivyo, tunayajadili na tumeunda Kamati maalum ya wataalam kutoka nje na ndani ambao wanaangalia jinsi *dialogue* yetu inavyokwenda. Naamini kwamba mwezi huu tutakuwa na kikao cha pili, naamini tutafika mahali ambapo tutaelewana vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la msingi Waheshimiwa Wabunge, naomba tena kusitiza, khanga ya kuazima ni tatizo. Lazima tuielekeze nchi yetu kujitegemea kama Baba wa Taifa alivyotufundisha. Hili ni jambo la msingi sana, mnaona tunapata wakimbizi tunahangaika miaka yote lakini wao wakipata wakimbizi kidogo wanakimbiza fedha zao kwa wakimbizi wa upande mwingine. Kwa hiyo, kwa kweli tuielekeze kujitegemea na ndiyo maana tukazanie zaidi kujenga mapato yetu ya ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme mengine haraka haraka. Kwa upande wa takwimu za mfumuko wa bei, wale ambao wana mazoea kuzitazama umegawanyika sehemu mbalimbali. Kuna mfumuko wa bei wa jumla lakini kuna mfumuko wa bei wa chakula lakini pia kuna non food inflation na ukizitazama hizi ziko bayana kabisa kwamba mfumuko wa bei ya chakula daima umekuwa ni mkubwa kuliko mfumuko wa bei wa jumla na sababu kubwa ni kwamba mfumuko wa bei wa Taifa letu unasukumwa zaidi na upatikanaji wa hali ya chakula lakini pia bei za mafuta. Kwa hiyo, hiyo iko wazi tu na nadhani ni mazoea kuziangalia zile takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwa upande wa kuhusu makampuni ya mawasiliano kujisajili katika soko letu la hisa. Kwenye taarifa ambayo niliisoma humu Bungeni, muda haukuniruhusu lakini mkiisoma ile taarifa kuna kipengele nafikiri ni ukurasa wa 15 kinaeleza vizuri juu ya hatua iliyofikiwa kuyataka makampuni yetu ya mawasiliano kujisajili katika soko la hisa kwa mujibu wa sheria. Nitaomba wasome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, limesemwa sana kuhusu Sekta yetu ya Kilimo. Ni kweli *growth* ya Sekta yetu ya Kilimo imekuwa hairidhishi na nimelisema hili mara kadhaa ndani ya Bunge, lakini ni muhimu tuwe *clear*. Ningependa kama ingewezekana kama ulivyo sema wewe, suala hili la uchumi pengine tukapata muda kweli wa kulijadili labda hata kwenye semina au hivi na Wabunge wakaja wakashiriki kwelikweli kwa maslahi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano; kilimo, tukisema bajeti pekee ya kilimo iongezwe tutabadilisha kilimo sio sawasawa. Najua *Maputo Declaration* inataka tupeleke 10% ya bajeti iende kwenye kilimo lakini kilimo kinachosemwa ni nini? Wataalam wanasema ili kilimo kiweze kufanya vizuri unahitaji pia sekta nyingine ambazo sio za kilimo nazo zifanye vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa mfano; tunapozungumzia mbolea, mbolea inazalishwa viwandani, unapozungumzia *performance* ya kilimo lazima uzungumzie upitikaji wa mazao kutoka shambani maana yake ni barabara. Unapozungumzia wataalam wa kilimo maana yake lazima uzungumzie Sekta ya Elimu. Kwa hiyo, ni lazima tuwe waangalifu, sio bajeti pekee ya kilimo. Kuna mambo mengi ambayo ndiyo yanakwenda kuamua *performance* ya kilimo iweje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa yako mengine ambayo ni ya msingi. Bajeti yetu ya umwagiliaji ikoje, bajeti yetu ya utaalam ikoje? *Incentives*, hata za kikodi kule kwenye kilimo zikoje? Lazima tuliangalie kwa upana wake ili kweli tuweze kuja na mkakati mzuri kwa ajili ya kuboresha Sekta ya Kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalisemwa hapa najua Naibu Waziri amelisema kwamba ukuaji wa deni la Taifa, tumekazania zaidi kukopa ndani, kwa hiyo *tuna-crowd out private sector*. Nisisitize tu, Serikali haina maagizo maalum kwamba tulipe wadeni wetu wa nje peke yake. Nililieleza wakati natoa taarifa Bungeni, ni lazima tuwe makini sana na kuhakikisha kwamba hatuachi kulipa halafu madhara kwenye uchumi yakawa makubwa zaidi. Kwa hiyo, *there is a delicate balance that we need to do* na ndicho tunachojaribu kufanya. Madeni haya ndugu zangu, mengine tumewapa taarifa, madeni haya mengine tunayolipa yamekopwa toka uhuru, kwa hiyo, hilo ongezeko linaloonekana ni *cumulative* sio kwamba ni kwa sababu tu imeongezeka katika Awamu hii ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yalisemwa pia kuhusu kwamba tuangalie nchi ili iendelee inahitaji *Sound Fiscal and Monetary Policies, Revenue Policies na Good Governance*. Nafikiri niseme tena, inabidi tuwe waangalifu, *country context* na *specificity* ni muhimu sana. Tanzania yetu ya leo sio Malaysia, wala sio Botswana, wala Korea. Kwa hiyo, ni muhimu sana na wale ambao mnasoma hivi vitabu ni ukweli pia kwa mfano Dkt. Mahathir Mohammed was a dictator! Ndiyo ukweli wenyewe, angalieni South Korea, Park Chu Hi ambaye ndiye aliibadilisha Korea alikuwa *dictator*, kwa hiyo miseme tu kwamba *good governance and stability* ndiyo msingi pekee wa ukuaji wa uchumi katika Taifa. Kwa hiyo, ni muhimu sana tuwe waangaifu na hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lilisemwa pia hapa kwamba pato la Mtanzania linapungua.

(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)

**WAZIRI WA MIPANGO NA FEDHA:** Ni vizuri tusikilizane Waheshimiwa, tunapojadili mambo ya kitaifa...

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, nawasihi tumsikilize Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MIPANGO NA FEDHA:** Pato la Mtanzania linapungua, si kweli! Pato la wastani la Mtanzania mliangalie vizuri, tumetoka kwenye dola 350 sasa tumefika dola 980, lakini ni vizuri kuzingatia *volatility* ya *exchange rate*, kama unatazama tu lile pato la Taifa kwa shilingi, halafu unagawa kwa *exchange rate* kuna miaka ambayo kwa wastani, *exchange rate* yetu imeporomoka na hivyo wastani unaonekana kushuka, lakini *trend* ya pato la Taifa inaongezeka kwa hakika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa mapitio ya mfumo wa kodi, naomba nitumie nafasi hii, kuwaomba sana Waheshimiwa Wabunge kwamba kuanzia mwezi huu sasa tutaanza kujadili pale Wizarani mapendekezo ya wadau wote wa kodi nchini, ambayo wamependekeza wengine wameleta. Hamjachelewa yeyote aliye na mapendekezo namna ya kuboresha mfumo wa kodi awasilishe mwezi huu tutaanza kufanya kikao cha kwanza. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vipaumbele, nilijaribu kulieleza kwenye moja ya vikao vilivyopita, naomba nisisitize sana kwamba kusema juu ya kuwa na vipaumbele vichache ni rahisi sana, lakini kuvitekeleza katika mazingira ya nchi maskini kama Tanzania ni jambo gumu kweli. Nakumbuka nilimtania Mheshimiwa Silinde hapa, nikasema nitaanza kupunguza vipaumbele vinavyogusa jumbo lake lakini ni ukweli tuna mahitaji makubwa kwenye maji, elimu, kila mahali. Kwa hiyo, kuweza kusema kwamba tujikite kwenye eneo moja tu la reli katika mazingira ya Tanzania haitawezekana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Naibu Waziri alieleza juu ya ukusanyaji wa kodi ya majengo, naomba tu niseme kama alivyoeleza kwamba tumeanza kukusanya. TRA imeanza kukusanya mwezi wa Kumi baada ya kukamilisha maandalizi na kuanzia mwezi wa Kumi mpaka Desemba mpaka sasa zimekusanywa sh. 4,762,369,261. Hata baadhi ya miji ambayo inasemekana hamna chochote si kweli, kwa mfano Kinondoni peke yake kwa hii miezi

michache imeshakusanya sh. 1,229,821,142, niseme Arusha Sh. 462, 527, 906, Ilala Sh. 999,193, 088 na takwimu tayari zipo kwa kipindi hiki, kwa hiyo kazi imeanza. Ilikuwa ni muhimu sana kufanya maandalizi stahiki ambayo yanagusa vitu vingi ili tuhakikishe kwamba tunakwenda sawasawa. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MWENYEKITI:** Malizia tu Waziri.

**WAZIRI WA MIPANGO NA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, okay, labda niseme tu moja la mwisho kwamba, kwenye tathmini ya deni la Taifa, tazameni kidogo kwa uangalifu taarifa ambayo niliwaletea. Tuna vile viashiria vya uhimilivu wa deni, ni pamoja na deni la nje, uwiano wake na uuzaji wa bidhaa za nje kwa maana ya *foreign exchange earnings* lakini pia tunaangalia deni la nje uwiano wake na mapato ya ndani. Kwa hiyo, siyo kwamba tunaangalia tu uwiano relative to GDP. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri. Sasa namwita mtoa hoja, namwona Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Kandege, hitimisha hoja hii, una muda usiozidi dakika 30.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kukushukuru kwa fursa nyingine tena, naomba niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote ambao walipata fursa ya kuchangia kwa kuongea walikuwa jumla ya Wajumbe 19 na waliochangia kwa kuandika walikuwa jumla 17, jumla yake ilikuwa ni 36.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ulivyoanza kusema asubuhi, umuhimu wa hoja hii nzito, naamini na wewe mwenyewe ni shahidi leo siku ya Jumamosi nisingependa kupoteza muda mwingi wa Waheshimiwa Wabunge, lakini wewe mwenyewe unaona jinsi ambavyo wametoa msukumo wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla naomba nikumbushe, wewe ni shahidi jinsi ambavyo kulikuwa na kazi kubwa ya uanzishaji wa Kamati ya Bajeti na uanzishwaji wa Sheria ya Bajeti na misingi ambayo ilikuwa imewekwa ili tuondokane na ile hali ambayo Bunge lilikuwa linafanya kama rubber stamping waliita watu hivyo. Tukasema tuondoke hapo, tufike mahali ambapo Bunge litashiriki katika mchakato mzima wa kuandaa bajeti na utekelezaji wake. Ombi ambalo ni vizuri na Serikali bahati nzuri wanasikia, isingependeza tukarudi nyuma tulikokuwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, itakuwa ni vizuri kwanza tukajengea uwezo Ofisi ya Bajeti na sitarajii, maana hili limeanza kujitokeza pale ambapo Bunge linataka kuwa na uwezo wake mzuri sasa kumekuwa na tabia hata ule uwezo mzuri, wale watumishi wazuri ambao wanapikwa na Bunge wanaanza kuhamishwa wanapelekwa upande wa Serikali, haitapendeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vizuri tukawa na uwezo mkubwa, twende na wengine ambao Mheshimiwa Mwenyekiti, ni shahidi ukienda nchi kama Uganda, Kenya inafika mahali ambapo Kamati ya Bajeti, inakuja na bajeti mbadala ili kulinganisha na ile bajeti ambayo inaletwa na Serikali, huko ndiko ambako tunatarajia kwenda. Kwa hiyo, itakuwa si vizuri kama Serikali watatumia fursa ya kuanza kuchukua vile vichwa vizuri ambavyo vinatengenezwa wakapeleka upande wa kwao. Hilo lilikuwa la jumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kulisema hilo na baada ya kutambua Wajumbe waliochangia, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, naomba kwa uchache nishukuru Serikali kwa sababu iko hapa wamesikia na mengi kimsingi na wao wamekiri kwamba ni ya kwenda kuyafanya kazi, nitaje machache na kwa ujumla Waheshimiwa Wabunge waliochangia kwa kuongea kama watapenda niwataje majina lakini kwa kuokoa muda, naomba nisitaje hata wale ambao walichangia kwa kuandika naomba nisitaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna baadhi ya masuala ambayo yamesemwa kwa kiasi kikubwa ni vizuri nikasema. Kimsingi wajumbe wengi wamesisitiza juu ya suala zima la kulipa deni la TANESCO. Sisi sote ni mashahidi, uko umuhimu sana wa kuhakikisha kwamba deni hili linalipwa maana tunaamini Tanzania ya viwanda bila kuwa na uhakika wa umeme hatuwezi kufika. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusiana na suala zima la ushiriki wa private sector (PPP). Si rahisi kwamba masuala yote ya maendeleo tutaiachia Serikali kwa maana ya ile miradi mikubwa. Kwa hiyo, ni vizuri kama ambavyo Waheshimiwa wengi wamechangia kwamba fursa iwepo na itumike kuhakikisha kwamba private sector inashiriki kama injini ya kukuza uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni shahidi, tumekuwa tukiongea muda mrefu tangu ukiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, mapendekezo ambayo yaliletwa Serikalini juu ya kuanza ujenzi wa barabara, kutoka Dar es Salaam kufika Morogoro na kwa kuanzia Chalinze zile njia tatu. Taarifa ambazo zilikuwepo ni kwamba private sector walikuwa wako tayari. Sasa hadithi imekuwa ya muda mrefu ni vizuri sasa Serikali ikaenda kwanza kutenda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na mradi...

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kandege keti kidogo. Waheshimiwa nitumie mamlaka niliyonayo kuongeza muda usiozidi nusu saa ili tuweze kuitendea haki hoja hii. Kwa hiyo, naongeza muda huo, hautazidi nusu saa kuruhusu mtoa hoja ahitimishe na hatimaye muiamue hoja hii. Mheshimiwa Kandege endelea.

**MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA**

**BAJETI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, katika Wajumbe wengi waliochangia yamesemwa maneno kwamba kuna hizi kauli za kutoka kwa Mheshimiwa Rais, anatamka pesa inapatikana. Niombe Waheshimiwa pamoja na nia njema ni vizuri tukaenda kutazama *budget frame* kwa ujumla wake, hiki ambacho kinatamkwa na Mheshimiwa Rais ukienda kwenye bajeti utakuta kipo. Siyo kwamba anaamka tu anatamka halafu pesa inapatikana. Mifumo ya bajeti iko sahihi. Kwa hiyo, ni vizuri kwa nia njema kwa sababu haya ambayo yanafanywa ni kwa ajili ya Watanzania ni vizuri tukafuatilia utaratibu wa bajeti twende kwenye vitabu, turejee tujue hayo ambayo yanatamkwa. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wachangiaji wengi wameongelea kuhusiana na suala zima la kilimo ambalo na Kamati ya Bajeti kimsingi tumesitiza kwamba ili twende kwenye Tanzania ya viwanda ni vizuri uwekezaji ukawekwa wa kutosha kuhusiana na suala zima la kilimo. Bahati nzuri Serikali imesikia, hii habari ya kwamba mvua zisiponyesha mara moja tu tunaanza kuwa na wasiwasi hatuwezi kwenda tukasema ni Taifa la kwenda kwenye uchumi wa kipato cha kati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ziko nyingi, kama mtu hakuchangia hoja asitarajie kusikia hoja yake ikijibiwa, hayo ambayo nayajibu ni yale ambayo yamechangiwa kwa ujumla na yakapewa uzito na bahati nzuri, hiki ninachokisema nimekisomea. Kwa hiyo, sikukiokota mitaani. (Makofij)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto za kibajeti, Wajumbe wengi wamechangia. Wabunge wameainisha kuwa katika taarifa ya Kamati hali ya uchumi kwa mujibu wa taarifa ya kutoka Benki Kuu na mwenendo wa mfumuko wa bei, Serikali inashauriwa kuhakikisha kwamba inakaa chini na kutathmini mwelekeo uliokuwa umetolewa awali na hali ya sasa. Ni vizuri tukaanisha ili tukapata namna ambavyo tunaenenda kama tuko kwenye *right track*. Hili niombe Serikali kujisahihisha si vibaya, tutazame wapi tuna-miss point ili isije ikafika mpaka dakika ya mwisho ndio tukajikuta tume-miss kile ambacho tulikitarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hoja kuhusiana na mafunzo kwa Bunge zima. Imechangiwa na Wabunge wengi ni hoja ya msingi ni vizuri Serikali mkajipanga maana exposure ni jambo la msingi sana. Pamoja na ufinyu wa bajeti lakini ni lazima tuhakikishe kwamba Wabunge wanajengewa uwezo ili wafanye kazi yao ya kikatiba ya kuhakikisha kwamba wanaisimamia na kuishauri Serikali kwa mujibu wa Katiba. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, imeongelewa hoja kuhusiana na Serikali kukopa ndani na sisi Kamati tumeliona, tukaishauri Serikali. Serikali ina muscles za kutosha ina uwezo mkubwa wa kwenda kutafuta mikopo nje, ni vizuri hii mikopo ya ndani tukaiachia sekta binafsi ili wahangaike na hizi fedha ambazo watazipata kwa urahisi. Tumeiomba Serikali iharakishe zoezi la kufanya sovereign rate ili waende kutafuta mitaji huko nje kwa sababu inapatikana. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la shilingi milioni 50 ya kila kijiji, wewe ni shuhuda ulishiriki wakati tunajadili na tukakubaliana kwamba pesa hizi zinazotolewa si pesa ya ruzuku, ni pesa ambayo ni ya mkopo na pesa ya mkopo lazima ujihakikishie kwamba huyu unayemkopesha anaenda kuzirejesha vipi kwa sababu pesa hii ni revolving fund. Tunaiomba Serikali iharakishe mchakato ili pesa hizi zikitolewa zikifika kwa wananchi ziweze kurejeshwa ili wananchi walio wengi, Watanzania wengi waweze kupata fedha hizi. (Makofii)

Mheshimiwa Mwenyekiti, muda hautoshi naomba sasa nijikite katika maazimio ambayo tunaomba Bunge lako liitake Serikali kwenda kuyatekeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu lipokee maoni na mapendekezo ya Kamati kuwa Azimio la Bunge kwa utekelezaji wa Serikali ili taarifa hiyo ije iletwе namna ambavyo Serikali imeteketeleza na kwa kuzingatia ushauri mzuri ambao umetolewa na Waheshimiwa Wabunge kwa kuzingatia pande zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (Makofii)

**MHE. HAWA A. GHASIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Asante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Ahsante Mheshimiwa Kandege.

**MBUNGE FULANI:** Umesomea Uenyekiti.

**MWENYEKITI:** Sasa naitoa hoja hii muiamue.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)  
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kwa  
kipindi cha kuanzia Januari, 2016  
hadi Januari 2017 ilipitishwa na Bunge)

**MWENYEKITI:** Sasa natamka rasmi kwamba maoni na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti yaliyomo kwenye taarifa yake yamepitishwa kama maazimio ya Bunge.

Hongereni sana, nimpongeze sana Mwenyekiti, Makamu na Wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa taarifa hiyo, lakini niwashukuru sana ninyi Waheshimiwa Wabunge kwa ushauri wenu, kwa maoni yenu, katika hoja hii. Tumefanya vizuri, ningelipenda sana nikazie tu kwa upande wa Serikali kama alivyosema Makamu Mwenyekiti, history ya kufika kwenye Kamati hii na kuwa na Sheria ya Bajeti na Ofisi ya Bajeti haikuwa nyepesi. Kwa hiyo, baada ya kufika hapo naomba Bunge na Serikali tusianze tena kuonekana kwamba tunaanza kukinzana. Maana tunajenga nyumba moja. Hizi rasilimali ni rasilimali za Watanzania. (Makof)

Kwa hiyo, Serikali kuitia bajeti inapokuja hapa na kuidhinishiwa na Bunge ni tendo la kikatiba. Sasa inapokwenda kuanza kutumia tuzingatie yale ambayo Sheria ya Bajeti inataka na hasa hii ya kutoa taarifa ya compliance ndio msingi wa utawala bora na kufuatilia hayo. Tunaanza haya, nasema tusichelewe sana maana hamna kitu kibaya kama kuanza kunyoosheana vidole kwamba tunaanza kukiuka sheria, sio kitu kizuri. (Makof)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kuyasema hayo, tutapata nafasi, process ya bajeti haiko mbali kuanza na tumekaribishwa na Waziri wa Fedha next week wanaanza kazi muhimu, wale ambao tuna mawazo mazuri ya kuboresha maeneo haya tutoe mchango wetu. Hata hivyo, Kamati ya Bajeti haifungwi kwa sababu yale ambayo tulifikiria kwa niaba ya Bunge tuliyawasilisha Serikalini siku nyangi lakini tunaweza tukaongeza na mengine.

Hili la deep sea fishing mimi nawaomba sana kwa heshima kubwa kwa Serikali, tusiendelee kuleta lugha mpya. (Makof)

Sasa, niwatakie mchana mwema lakini nina matangazo.

**MBUNGE FULANI:** Semina zipo?

**MWENYEKITI:** Semina zitakuwepo, uongozi wa Bunge upo, lakini na tukiliwezesha Bunge kwa maana ya... si ndio mnaamua ninyi eeh, mlitambue. (Makofi)

Tangazo la kwanza ni kwamba Wajumbe wa Kamati zifuatazo UKIMWI, Kamati ya Bajeti na Kamati ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, wanatangaziwa kuwa leo saa nane na nusu kutakuwa na semina kuhusu afya ya uzazi na watoto wachanga, leo saa nane na nusu. Ni hizi Kamati tatu tu. Mimi nasoma yaliyoandikwa hapa na itafanyika kwenye Ukumbi wa Morena Hotel hapahapa Mjini Dodoma. Semina hii imeandaliwa na Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), Inter-Parliamentary Union na Bunge letu na itafunguliwa rasmi na Spika wetu ambaye ndiye mgeni rasmi, Mheshimiwa Job Ndugai.

Pia pamoja na Wajumbe wa kamati hizi tatu, Wabunge Wanachama wa Vyama vya Idadi ya Watu, Utepe Mweupe...

**MBUNGE FULANI:** Mweusi!

**MWENYEKITI:** Sio mweusi. (Kicheko)

Utepe Mweupe na TAPAC pia wanakaribishwa kushiriki. Hili ndio la kwanza.

Tangazo la pili, hili linatoka kwa Katibu wa Bunge wa CCM, Jasson Rweikiza. Ni tukio muhimu sana na naomba mnisikilize wote. (Kicheko)

Wabunge wote wa CCM, waliojiandikisha na ambao hawakujijandikisha, wanaalikwa katika sherehe za miaka 40 ya kuzaliwa kwa CCM zitakazofanyika kesho saa saba mchana, Dodoma Convention Center ni sherehe za kitaifa wote mnakaribishwa, hata ninyi mnakaribishwa. (Makofi)

Haya ndiyo matangazo niliyonayo hapa.

**MBUNGE FULANI:** Semina ni saa ngapi?

**MWENYEKITI:** Semina ni saa nane na nusu na hii semina inayoanza leo itaendelea tena kesho saa tatu asubuhi pale pale. kwa hiyo, Wabunge wa Kamati zile tatu tu na wale wengine. Kwa hiyo, Wajumbe wa Kamati ya Bajeti.

**MBUNGE FULANI:** Ni ubaguzi huo

**MWENYEKITI:** Sasa haya siyo ubaguzi ni utaratibu tu. Kwa hiyo, baada ya kuyasema haya Waheshimiwa Wabunge na kwa shukrani nilizowapeni, nilisahau kuishukuru Serikali kwa hayo mliyoyasema. Samahani sana nilitaka kusahau, maana ndio reli hiyo, tunaanza vizuri. Waziri wa Fedha umesema na umetoa ahadi nzuri hasa ile kutafuta nafasi ya pamoja, maana tunapokuwa na uelewa wa pamoja kwa masuala haya inasaidia sana, tusiwe na kundi moja la Wabunge wananaufaika, mnarutubisha lakini tukiwa wengi itatusaidia. Ahsanteni sana Serikali kwa hayo. (Makofii)

Kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi. (Makofii)

(Saa 8.04 Mchana Bunge lilahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 6 Februari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)